

# Kudumisha uhusiano kati ya jamii, ufugaji na wanyamapori

## MWONGOZO WA USHIRIKISHWAJI KATIKA KUPANGA MATUMIZI YA ARDHI

AFRICAN WILDLIFE FOUNDATION®
ILRI INTERNATIONAL LIVESTOCK RESEARCH INSTITUTE
GEF
LEAD

# Kudumisha uhusiano kati ya jamii, ufugaji na wanyamapori

## MWONGOZO WA USHIRIKISHWAJI KATIKA KUPANGA MATUMIZI YA ARDHI

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kushirikiana na Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Afrika (AWF), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye mradi uliofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) na Benki ya Dunia (WB)


Roma, 2009

Mtindo ulitumika na uwasilishaji wa maudhui ya kitini hiki hauwakilishi kwa namna yoyote ile maoni ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kuhusiana na masuala ya kisheria au maendeleo ya nyanja yoyote ile na nchi, himaya, mji au mamlaka yoyote, au kuingilia na mipaka yake. Yanapotajwa majina ya kampuni au bidhaa za viwanda, bila kujali kama bidhaa hizo zina haki miliki au la, haimaanishi kuwa bidhaa hizo zimekubaliwa au zimependekezwa na FAO dhidi ya bidhaa kama hizo ambazo hazikutajwa. Maoni yaliyoelezwa katika kitini hiki ni ya waandishi na si lazima yawe ndiyo maoni rasmi ya FAO.

Haki zote zimehifadhiwa. Kudurufu na kusambaza taarifa zilizomo humu kwa madhumuni ya kuelimisha na si kufanya biashara kunaruhusiwa bila kuwa na ulazima wa kupata ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwenye haki miliki, ili mradi chanzo cha taarifa hizo kitajwe wazi. Hairuhusiwi kudurufu kitini hiki kwa madhumuni ya kibiashara bila kupata ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwenye haki miliki. Maombi ya ruhusa hiyo yaelekezwe kwa Chief, Electronic Publishing Policy and Support Branch, Communication Division, FAO Viale delle Terme di Caracalla, 00153 Rome, Italy au kwa barua pepe kwa copyright@fao.org

© FAO 2009

# Utangulizi



Mwongozo huu umeandaliwa ili kusaidia jamii na watunga sera katika ngazi ya jamii na kitaifa kufanya maamuzi na uchaguzi sahihi kuhusu matumizi ya ardhi, biashara, na sera za kitaifa kwa maeneo ya wafugaji, hasa nyika za umasaini na maeneo makame ya Afrika ya Mashariki.

Kitini hiki kinachoeleza mfumo wa kusaidia ufanyaji maamuzi, *Kudumisha uhusiano kati ya jamii, ufugaji na wanyamapori* ni matokeo ya kazi iliyofanywa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Afrika (AWF) na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mradi wa *Mifumo mipya ya kujumuisha mifugo na wanyamapori kwenye maeneo ya malisho yaliyopo pembezoni mwa hifadhi za Taifa katika Afrika - Tanzania* uliofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) na Benki ya Dunia.

Mifugo na wanyamapori vimekuwa pamoja kwa maelfu ya miaka: nyika za umasaini, ambazo ni mojawapo ya maeneo yaliyobakia duniani yenye utajiri mkubwa wa wanyamapori, ni kielelezo sahihi kwamba mikakati ya asili ya ufugaji ni endelevu kwa wanyamapori na mifugo.

Inakadiriwa kuwa kwa sasa asilimia 70 ya wanyamapori waliomo katika mbuga za wanyama za Tarangire na Manyara hutawanyika kutafuta malisho kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi hizi katika vipindi fulani fulani vya mwaka.

Wanyamapori wanatoa mchango kwenye sekta ya utalii ambayo inaziingizia nchi za Afrika Mashariki kiasi kikubwa cha fedha za kigeni. Hata hivyo, migongano iliyomo kwenye sera za kitaifa, ongezeko la watu, mahitaji makubwa ya ardhi, na mabadiliko ya hali ya tabianchi na magonjwa ya mifugo vimechangia kuleta mabadiliko ya hali ya asili ya nyika za umasaini na maeneo mengine ya wafugaji.

Wafugaji ambao miaka iliyopita walikuwa wakihamahama sasa wanaishi sehemu za kudumu na kujihusisha pia na shughuli za kilimo, na pia wakulima wadogo wadogo na wakubwa wanalima maeneo ambayo hapo nyuma yalikuwa ya malisho kwa mifugo na wanyamapori. Mabadiliko haya yanaibua migogoro kati ya wakulima na wafugaji; wanyamapori na watu; na pia wahamiaji na wenyeji. Wastani wa idadi ya mifugo kwa mfugaji inapungua.

Kutokana na mabadiliko hayo, vile vile nchi za Tanzania na Kenya kila moja imepoteza zaidi ya nusu ya wanyamapori waliokuwepo katika miaka 30 iliyopita.

Mradi wa *Mifumo mipya ya kujumuisha mifugo na wanyamapori kwenye maeneo ya malisho yaliyopo pembezoni mwa hifadhi za Taifa katika Afrika - Tanzania* umeyafanyia kazi masuala haya na kuvisaidia



vijiji sita katika nyika za umasaini katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, kuanzisha shughuli za biashara zinazohusiana na wanyamapori, uanzishaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs), utatuzi wa migogoro, na afya ya mifugo. Yote haya yanalenga kuisadia jamii kuboresha maisha yao kwa kutegemea mifugo na wanyamapori.

## MWONGOZO WA KUSAIDIA UFANYAJI MAAMUZI UNAMLENGA NANI?

Mwongozo huu unawalenga wale wote wanaohusika katika matumizi na usimamizi wa maliasili ulioshirikishi. Mwongozo unafaa kutumiwa na watendaji wa halmashauri za wilaya na vijiji, sekta binafsi, na wawakilishi wa serikali kuu, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na mashirika ya maendeleo yanayoshiriki kwenye mipango ya matumizi ya ardhi na usimamiaji wa maliasili.

## MALENGO

Mwongozo huu wa kutoa maamuzi unalenga yafuatayo:

- Kuwawezesha watunga sera na wanajamii kuelewa sababu na jinsi mandhari ya Afrika Mashariki inavyobadilika, na hasa kwenye maeneo ya wafugaji katika Tanzania na Kenya.
- Kutoa mwongozo wa jinsi ya kufanya mipango ya matumizi ya ardhi, kitaifa na hata ngazi za chini.
- Kuchangia mawazo mapya na mitazamo mbadala juu ya uwezekano wa biashara zenye mwelekeo wa uhifadhi katika maeneo yenye mifugo na wanyamapori ili kuboresha maisha ya wakazi wa maeneo hayo.
- Kusaidia kutoa mwongozo kwa jamii, na wawezeshaji kutoka sehemu nyingine, katika mchakato wa kusimamia na kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi; kuanzisha na kuendeleza uhifadhi wa kijamii/jumuiya (hasa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori - WMAs - nchini Tanzania); na kuhakikisha mifugo katika maeneo yenye wanyamapori inakuwa na hali nzuri.
- Kutoa mahali ambapo uzoefu na mafundisho yaliyopatikana kutokana na mradi wa GEF na mingineyo yatawekwa pamoja kwa kumbukumbu na matumizi ya baadaye.

## KITINI CHA KUSAIDIA UFANYAJI MAAMUZI KIMEBEBA MAMBO GANI?

Mwongozo una sura sita zinazotoa mapendekezo, hatua na uzoefu uliopatikana katika jamii nyinginezo zenye changamoto zinazofanana za mabadiliko ya njia mbalimbali za kuendesha maisha (livelihood) kwa kuishi karibu na wanyamapori.

### Sura ya 1: Mipango ya matumizi ya ardhi: utangulizi kwa watunga sera

Sura ya 1 inalenga hasa kuwasaidia watunga sera kwenye ngazi za kitaifa na mikoa kuelewa mabadiliko mbalimbali ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya wafugaji yaliyo na wanyamapori. Inatoa mwongozo wa mipango ya matumizi makubwa, umuhimu wa kutazama hali ya baadaye ki-uendelevu na ki-usawa, na jinsi mifano inavyoweza kusaidia kuonesha mitazamo mbalimbali ya matumizi ya ardhi inavyoweza

**MIFUMO MIPYA YA KUJUMUISHA MIFUGO NA WANYAMAPORI KWENYE MAENEO YA MALISHO YALIYOPO PEMBEZONI MWA HIFADHI ZA TAIFA KATIKA AFRIKA – TANZANIA**

*Mifumo mipya ya kujumuisha mifugo na wanyamapori kwenye maeneo ya malisho yaliyopo pembezoni mwa Hifadhi za Taifa katika Afrika - Tanzania* (2005-2009) ni mradi uliofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) kupitia Benki ya Dunia (WB) na kutekelezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Afrika (AWF), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu umetekelezwa kwenye vijiji sita* vilivyomo kwenye mfumo wa ekolojia wa Tarangire-Manyara uliopo katika wilaya za Monduli na Simanjiro.

Lengo la mradi ni kusaidia katika hifadhi ya bioanuai muhimu kidunia katika mtazamo ulio bora wa ekolojia, utatuzi wa migogoro, uhakika wa chakula na kupunguza umasikini. Lengo kubwa la mradi ni kuchangia katika utungaji wa sera na miundombinu ya kitaasisi inayolenga kupunguza kwa kiwango kikubwa migogoro inayohusiana na nafasi zilizopo za watu kutumia rasilimali wanapoendelea na shughuli za ufugaji, kilimo na kuhifadhi wanyamapori.

Mradi umechambua na kuelewa mabadiliko yaliyotokea kwenye matumizi ya ardhi katika eneo la mradi kwa lengo la kutumia uelewa huu katika juhudi za kukuza mapato ya wadau kutokana na wanyamapori na mifugo. Lengo hili linafikiwa kupitia uendelezaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na uanzishaji wa taratibu za ugawanaji faida kutokana na wanyamapori, kama vile biashara zinahusiana na uhifadhi na kuandaa mwongozo wa kusaidia ufanyaji maamuzi ili kuimarisha fursa za watu kutumia na kusimamia vizuri rasilimali.

* *Vijiji hivyo sita ni Loibosiret, Narakauwo na Loiborsoit "A" katika wilaya ya Simanjiro; na Lolkisale, Naitolia na Mswakini Juu katika wilaya ya Monduli.*

kuibuliwa. Mifano kutoka Tanzania na Kenya inaonesha mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliyokwishatokea na kuimarisha umuhimu wa kulipa kipaumbele suala la kuwepo kwa mipango ya ardhi.



## Sura ya 2: Kujenga picha ya jamii yetu kwa siku zijazo: sababu na jinsi ya kushiriki kupanga matumizi ya ardhi

Sura ya 2 inaeleza jinsi jamii inavyoweza kuwazia na kupanga inavyotaka hali yake iwe katika siku za usoni. Inaonesha jinsi wadau wote wanavyoweza kushirikishwa katika kuweka mpango mzuri wa kutumia ardhi kwa pamoja na hivyo kupunguza migogoro ya kugombea rasilimali. Kwa kuwa kisheria jamii inastahili kufaidika kutokana na shughuli za biashara kwenye maeneo ya hifadhi (kama ilivyojadiliwa baadaye hapa chini), upangaji shirikishi wa matumizi ya ardhi unatoa pia mwanya kwa wadau kujifunza na pia kuwa na sauti katika matumizi ya ardhi yao.

## Sura ya 3: Wanyamapori waweza kukuinua kiuchumi: kuanzisha biashara zinazohusiana na uhifadhi (CBV)

Wakati jamii inapoingia gharama zinazotokana na kuishi karibu na wanyamapori, hali hiyo inakubalika tu endapo jamii hiyo nayo itafaidika kutokana na wanyamapori. Hata hivyo, karibu mapato yote kutoka kwenye sekta ya utalii na biashara zinazohusu asili yamekuwa yakienda kwa makampuni ya utalii na serikalini pekee. Hivi karibuni zimeibuka taasisi zisizokuwa za kiserikali, na wawekezaji, wanaoshirikiana kuhakikisha kuwa jamii iliyopo mahali palipo na uwekezaji kwenye maliasili nayo inafaidika na uwekezaji huo ili kuleta faida kwao kwa kuishi na wanyamapori hao.

Sura ya 3 inaonesha hatua thabiti na mifano ya biashara inayohusiana na uhifadhi ambazo zinaweza kuwa za manufaa kwao.

### Sura ya 4: Jumuiya za Hifadhi za Wanayamapori (WMAs): faida, changamoto na hatua za kuunda Jumuiya

Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) ni hifadhi zinazomilikiwa na jamii. Hii ni njia inayopendelewa na serikali ya Tanzania kuwezesha jamii kusimamia na kufaidika kutokana na wanyamapori wao. Mchakato wa kuanzisha hifadhi hizi ni mrefu na wa gharama kubwa. Hata hivyo, Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori zaweza kuwa za kuvutia iwapo jamii zitapewa haki kusimamia uwindaji wakati leseni za uwindaji zinapotolewa upya mwaka 2009 - au serikali ikikubali kuufanya mchakato kuwa rahisi kuliko ilivyo sasa.

### Sura ya 5: Migogoro kwenye jamii: ushughulikiaji migogoro kwenye maeneo yaliyo na mifugo, kilimo na wanyamapori

Mara zote migogoro huwa haiishi mahali ambapo watu wanashughulika na ufugaji, kilimo, uvuvi, uwindaji, kupokea watalii na kuhifadhi wanyamapori katika eneo hilo hilo. Sura ya 5 inatoa mwongozo wa kuhakikisha uhusiano mzuri unaendelea kuwepo wakati wa kushughulikia migogoro katika jamii. Kwa kiasi kikubwa taratibu za kisasa za kusuluhisha na kushughulikia mogogoro zinazingatia taratibu za jadi zilizopo, na zote zinaweza kutumika kwa pamoja.

### Sura ya 6: Kushughulikia magonjwa ya mifugo karibu na hifadhi za wanyamapori katika Afrika Mashariki

Moja ya changamoto zinazowakabili wafugaji waishio karibu na maeneo yenye wanyama wa porini ni kuwepo mianya ya mifugo au binadamu kushambuliwa na magonjwa yatokayo kwa wanyamapori. Vilevile, mabadiliko ya hali ya tabianchi na ongezeko la mahitaji ya ardhi yanachangia kwenye kuongezeka kwa magonjwa kwenye maeneo ya wafugaji. Sura ya 6 inajadili masuala muhimu na kuainisha baadhi ya mbinu ambazo jamii na watunga sera wanaweza kutumia kupunguza athari za magonjwa.

Shukrani ziwafikie wataalamu wengi na wanavijiji walitoa kwa dhati muda wao, taarifa na mapendekezo kwa kitini hiki.

Kwanza, kwa msaada wa kiutafiti, mwongozo na mwenendo wa utekelezaji, tunawashukuru Henning Steinfeld, FAO-Rome; Cees de Haan; Christophe Crepin, Benki ya Dunia; Vincent Castel, Benki ya Maendeleo Afrika; wajumbe wa kamati ya kusimamia mradi (PSC); Gerald Runyoro wa FAO -Tanzania; na Gerson Mollel na Steven Kiruswa wa AWF, Arusha.

Vile vile tunawashukuru watu binafsi na taasisi zifuatazo kwa mchango wao mkubwa katika kukamilisha kitini hiki: Wafanyakazi wa AWF, hasa Ben Mwongela, James Kahurananga, Josephine Simons, Julius Laiser, Makui Ogeli, na Thadeus Binamungu. Allan Kijazi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Allen Mnyenye wa Maramboi Tented Camp; Cassian Mumbi wa Taasisi ya Tafiti za Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Daudi Melengori, Mwenyekiti wa Olasiti; David Nkedianye, Msosiolojia wa nyika za malisho na jamii, Wanachama wa kikundi cha akina mama cha Esilalei na watumishi; Fred Nelson, Maliasili Initiatives; na John Palangyo ambaye ni Ofisa Maliasili Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

Wengine ni Joseph Lendiye wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduimet; Ranchi ya Manyara, hasa Aaron Luziga na Rama Ngatoluwa; Mara Goldman wa Chuo Kikuu cha Colorado, Kikundi cha akina mama cha Mwada; Noah L. Teveli na Rigobeth Camiti wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge; Raphael Matinda, Mwenyekiti wa kijiji cha Loiborsiret; Seraphino Bichabicha Mawanja, Ofisa Wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli; Shirley Tarawali, Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) na Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF) hasa Enock Chengullah na Sulle B. Emmanuel.

Pia, tunatoa shukrani za dhati kwa wanavijiji kwenye vijiji sita vilivyomo kwenye mradi, na viongozi na watumishi wote kwenye eneo la mradi na hasa vijiji vya Loiborsiret, Narakauwo and Olasiti kwa kutupokea vizuri na kutusaidia tukaweza kuifanya kazi hii.

**Waandaaji wa kitini hiki**
Mohammed Y. Said (ILRI), Isaya Naini na Carole Douglis

**Wahariri**
Carolyn Opio na Pierre Gerber, FAO (Rome)

**Mwandishi Mtaalam/Mhariri**
Carole Douglis

**Michoro na picha**
Claudia Ciarlantini, usanifu na mpangilio;
George Mogaka, michoro

**Wachangiaji wengineo**
Shem C. Kifugo, Fortunata Msoffe, Joseph O. Ogutu,
Jane Wanjiku Gitau, Moses Neselle; Claudia Pittiglio

**Kutafsiri**
Secelela Balisidya

**Wafadhili**
Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT);
Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF);
Livestock, Environment and Development (LEAD) Initiative; Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), na Benki ya Dunia (WB).

[1] Wawakilishi kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Idara ya Takwimu; Taasisi ya Tafiti za Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) na wawakilishi wa Halmashauri za Wilaya za Simanjiro na Monduli.

# Mpango wa matumizi ya ardhi: utangulizi kwa watunga sera




## KWA NINI MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI?

Popote pale watu wanapotumia ardhi, matumizi ya ardhi yanakuwa yamepangwa, kwa kujua au bila kujua.

Watunga-sera na wengine wetu tunapenda kupanga kwa nia nzuri na kwa demokrasia ili mipango ya ardhi ichangie katika kutimiza malengo ya ngazi ya chini na ya kitaifa pamoja na maendeleo vijijini, uzalishaji mali, uhakika wa chakula, uendelevu wa rasilimali na usawa.

Kimsingi, kupanga matumizi ya ardhi ni juhudi za kitaifa, kutoka vijijini, wilayani hadi mikoani wakijumuisha mahitaji ya ngazi ya chini na vipaumbele vya kitaifa (Kisanduku namba 1).

Katika utekelezaji, imekuwa haitiliwi maanani inavyopaswa. Kwa mfano, moja ya malengo ya Serikali ya Tanzania ni kwa wilaya zote kuwa na mipango yake ya matumizi ya ardhi, pamoja na vijiji vyote hadi kufika mwaka 2010. Hata hivyo hadi mwaka 2009 inakadiriwa kuwa ni vijiji 1,000 tu ndivyo vyenye mipango ya aina hii kati ya jumla ya vijiji 8,000.

Hata hivyo kupanga siyo kitu cha mzaha: ni muhimu sana kufikia malengo ya kitaifa pamoja na ngazi za chini. Mfano, madhumuni ya kitaifa yanajumuisha:

- Kuongeza mapato kutokana na mifugo;
- Kuongeza mapato kutokana na wanyamapori kupitia utalii;

### KISANDUKU NAMBA 1: MIPANGO THABITI YA MATUMIZI YA ARDHI

- Inazingatia hali za jamii katika hatua na yanayojumuishwa katika mpango.
- Inazingatia mtazamo wa utamaduni uliopo na kuzingatia elimu ya jamii ya mazingira yaliyopo.
- Inazingatia pia njia za kimila za kutatua matatizo na migogoro.
- Inaelewa kuwa maendeleo ya vijiji ni hatua "zinazoanzia chini-kwenda juu" na zinazojikita kwenye kujisaidia na kujipa majukumu.
- Inakuwa sehemu ya kujadiliana miongoni mwa wadau na sio kuletewa kila kitu kwa ajili ya utekelezaji tu.
- Inaelekeza kwenye kuboresha uwezo wa washiriki katika kupanga na kuchukua hatua.
- Inahitaji uwazi na upatikanaji wa taarifa kwa washiriki wote.
- Inazingatia jinsia na mahitaji ya wadau wote.
- Inaruhusu mabadiliko, inajumuisha mambo yaliyojitokeza na mabadiliko ya hali.
- Inalenga utekelezaji.

*Chanzo:* GTZ, 1999

# Utangulizi



- Kuongeza mazao ya kilimo kwa kuvuna zaidi; na
- Kusaidia njia za kuleta kipato na chakula vijijini.

Madhumuni ya Kenya pia yanasisitiza kuongezeka kwa mapato kutokana na utalii na wanyamapori, kilimo na mifugo.

Kwa kuwa ardhi haiongezeki, ni kupanga kwa uangalifu na kutumia vyema kila sehemu ya ardhi ndiko kunakoweza kutupa matumaini ya kufikia malengo yote ya matumizi ya ardhi.

## KWA NINI SURA HII IPO?

Kwa sasa matumizi ya ardhi mara nyingi yamekuwa yakiangaliwa katika mtazamo finyu na kuzingatia malengo ya mtu binafsi; sera ambazo hazitahamasisha matumizi endelevu; na uhalisia kuliko utafiti.

Sura hii inatoa utangulizi juu ya dhana za msingi na hatua madhubuti za mipango ya ngazi ya juu (macro-level). Sura inasisitiza kuwa mipango ya matumizi ya ardhi ni zoezi lenye kuzingatia mambo mengi ambayo yatafanikisha mpango iwapo yatazingatia:

- Mielekeo ya sasa;
- Fursa za maendeleo zilizopo kwa siku za usoni;
- Mahitaji, kinachopendelewa, na uwezo wa kila mdau; na
- Kuweka pamoja kinachopendelewa kuwekwa katika mpango kutoka ngazi za chini na za kitaifa.

Na inaelezea matokeo ya utafiti juu ya maendeleo ya matumizi ya ardhi katika Afrika Mashariki.

## MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI KATIKA NGAZI YA KITAIFA: BAADHI YA HATUA MUHIMU KWA WATUNGA-SERA

1. Kwanza ni kuangalia hali halisi inayoendelea, wapi, na kwa nini (angalia chini kwa ajili ya mchakato wa mabadiliko kikanda).
2. Halafu tabiri, au hata fikiria, mwenendo wa sasa ukiendelea kwa miaka mitano, kumi, ishirini, hamsini ijayo. Je mabadiliko haya yangeweza kuleta matokeo ambayo tungependa kuyaona?
3. Ni muhimu kujaribu kuweka maono. Ni nini hasa tunachopenda kukiona? Maono ya MKUKUTA ya Tanzania na ya Kenya ya 2030 ni maono katika ngazi ya kitaifa, lakini kuna kazi kubwa zaidi ya kufanya ili kuyaimarisha katika ngazi ya chini, na kuyaratibu ili yafikie malengo yao.
4. Kujenga picha na kuchambua mifano halisi. Kwa usaidizi wa mifano ya komputa inayosaidia kutabiri mienendo, uchambuzi wa hali halisi unasaidia kutathmini vitisho, fursa na vikwazo vya mibadala iliyopo. Hali halisi inaweza kuibua majadiliano ya uwezekano wa ufumbuzi na athari kuanzia ngazi za vijiji, kanda na hata ngazi ya dunia (Kisanduku namba 2).
5. Ni mipango gani na sera zipi zinaweza kutayarishwa ili kupata hali yenye ushawishi chanya juu ya maisha vijijini, uhifadhi na maisha mazuri ya siku za usoni?
6. Tukumbuke kuwa mipango haijatengenezwa kwenye mawe: iko kama mawazo. Yanaweza na ni muhimu yajaribiwe, kuonyeshwa kuwa ni ya kweli au la, na kupitiwa inavyohitajika.

### Maswali muhimu ya kujiuliza wakati tukitafiti juu ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi

Katika karne ya 21, matumizi ya ardhi kwa ajili ya binadamu ndiyo chanzo kikubwa kinachowajibika kwa mabadiliko ya kiekolojia katika ngazi ya kitaifa na dunia. Kujiuliza maswali yafuatayo kunaweza kuwasaidia watunga sera kuelewa jinsi matumizi ya ardhi yanavyobadilika, na wapi mabadiliko haya yanaelekea.

1. Matumizi ya ardhi yanabadilikaje? (Nini kinatokea?)
2. Ni mambo gani ya kimazingira na kiutamaduni yanachangia katika kubadilika kwa matumizi ya ardhi? (Nani anachangia na kwa nini?)


**KISANDUKU NAMBA 2: MWONGOZO UNAOFAA WA KUONESHA MABADILIKO YA UOTO WA ARDHI**

Kati ya mifano inayofaa ya kuonesha mabadiliko ya matumizi ya ardhi, mmoja kati ya hiyo unaweza kuwa mzuri zaidi kwa kupanga mipango mikubwa ya matumizi ya ardhi katika Afrika Mashariki (Etter et al. 2006). Mwongozo huu unaangalia "visababishi" vya mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika maeneo manne: eneo, mandhari, kanda na nchi.

- **Katika eneo la kijiji: mandhari kijiografia, matumizi ya zamani ya ardhi na hali ya hewa ndiyo visababishi vikubwa vya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.**
- **Katika uwanda mkubwa wa mandhari: mfumo wa umiliki wa ardhi, hali ya uoto wa ardhi na ujirani katika maeneo yanayozunguka ndiyo visababishi vikuu.**
- **Katika ngazi ya kanda: ufikikaji na upatikanaji wa huduma na masoko ndiyo visababishi.**
- **Katika ngazi ya taifa: ongezeko la idadi ya watu, sera na mabadiliko ya teknolojia ndivyo vinavyoongoza.**

Kwa kuongezea, visababishi vinaweza kugawanywa katika visababishi vilivyo ndani ya eneo *(endogenous)*: (mfano - udongo, mfumo wa maji, ujirani) na vishawishi kutoka nje *(exogenous)*: (mfano - sera, teknolojia, umbali, gharama za usafiri na masoko).


### Visababishi vya mabadiliko ya uoto wa ardhi, kutoka eneo linalohusika hadi nchi nzima




*Chanzo:* Etter et al. 2006


# Hatua kuelekea mafanikio






*Chanzo:* IEA, 1998

RAMANI 1: RAMANI INAONESHA MTAWANYIKO WA WINGI WA VIUMBE AINA YA MAMALIA KATIKA AFRIKA, KUONESHA IDADI KUBWA YA VIUMBE HAWA KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI NA YA KUSINI




*Chanzo:* FAO, 2000

MCHORO 1: WINGI NA MTAWANYIKO WA WATU KATIKA AFRIKA MASHARIKI KWA MIAKA YA 1960 NA 1990

3. Ni maeneo gani yameathirika na mabadiliko ya uoto wa ardhi? (Ni wapi?)
4. Je mabadiliko ya uoto wa ardhi yanabadilika kwa kasi kiasi gani? (Wakati gani?)
5. Mabadiliko haya yana athari gani kwa maisha ya wafugaji na wanyamapori? (Hiyo husababisha nini?)

Kadiri idadi ya watu na uchumi wa nchi unavyozidi kukua, msukumo kwa matumizi ya ardhi hautapungua katika siku za usoni. Msukumo utaongezeka zaidi hasa kwenye nchi zenye wingi wa bioanuwai, na zenye kiwango kikubwa cha ongezeko la idadi ya watu pamoja na mabadiliko ya kasi ya mandhari.

## Matokea makuu juu ya matumizi ya ardhi na mabadiliko ya matumizi ya ardhi Afrika Mashariki

Watu wanapendelea kuishi kwenye makazi yaleyale kama mamalia wakubwa: mandhari zenye uhakika wa vyanzo vya maji na mvua ya wastani. Kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, makazi na kilimo vinaongezeka kwenye maeneo mazuri zaidi, na wanazidi kujikita zaidi kwenye maeneo tengefu. Katika Afrika Mashariki, hii inamaanisha kuwa makazi na mashamba yanaelekea katika maeneo yenye hali ya ukame ambayo si tu yana wanyamapori wengi lakini yamekuwa makazi ya asili kwa wafugaji (Kisanduku namba 3). Migogoro inaanza pale ambapo watu wanatayarisha ardhi kwa ajili ya kilimo, hivyo kuharibu makazi ya wanyamapori na malisho ya mifugo.

Utafiti wa kina katika kanda (katika maeneo ya vijijini, kutoka ramani za kutumia satelite, mtindo wa kutumia kompyuta) umebainisha taarifa zifuatazo kutaarifu ufanyaji madhubuti wa mipango ya matumizi ya ardhi.

1. Idadi ya watu inaongezeka kwa kasi. Idadi ya watu nchini Tanzania iliongezeka karibu mara tano, kutoka watu milioni 8 hadi watu milioni 38 tangu uhuru. Idadi ya watu nchini Kenya pia ilikua kutoka milioni 8 mwaka 1960 hadi milioni 39 leo: karibu ongezeko la mara tano. Kasi ya ukuaji wa miji mikubwa pamoja na miji midogo na miji midogo ya biashara katika maeneo ya vijiji ni mabadiliko yanayoendana. Wakati ukuaji utakuwa kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na siku zilizopita, idadi ya watu inatarajiwa kukua mara mbili zaidi katika miongo mitatu ijayo.
2. Maeneo ya malisho yanageuzwa kuwa mashamba. Kwa upande mmoja ni kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu na haja ya kuzalisha chakula kwa ajili ya watu walioko mijini, maeneo ya malisho yanageuzwa kwa kasi kuwa maeneo ya kilimo katika maeneo yote ya Afrika Mashariki (maeneo yenye udongo hafifu na ukame wa mara kwa mara yakijumuishwa). Mabadiliko haya pamoja na makazi yaliyomo yanachangia wafugaji, mifugo na wanyamapori kutoweza kuzunguka kutoka eneo moja hadi lingine.

3. Mabadiliko ya matumizi kwenda kwenye kilimo yanaongezeka zaidi kwenye maeneo yenye mvua nyingi, mahali ambapo kilimo ni rahisi na kinaongeza kipato (Ramani 2). Uchambuzi kwa upana wa ardhi unaonesha kuwa katika Afrika Mashariki, kubadilisha ardhi ni kwa kasi kwenye maeneo yaliyo karibu na mito, barabara, miji na mipaka ya hifadhi za wanyamapori.
4. Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha ukame wa mara kwa mara. Ukame na hali nyingine ngumu za hali ya hewa zimekuwa zikiongezeka mara kwa mara, na kufanya aina nyingi za matumizi ya

## KISANDUKU NAMBA 3: MWENENDO WA MATUMIZI YA ARDHI KATIKA ENEO LA MFUMO EKOLOJIA LA TARANGIRE-SIMANJIRO: NINI KINATOKEA? NINI KINAKUJA?

Watafiti walifanya utafiti wa kina wakitumia mbinu za kitakwimu za matumizi ya ardhi ili kuangalia mabadiliko ya miaka therathini iliyopita ya kilimo kisicho na mpangilio katika eneo la mfumo wa ekolojia la Tarangire-Simanjiro (katika Wilaya za Simanjiro na Monduli).

Waligundua kuwa watu wanaweza kugeuza maeneo ya malisho kuwa mashamba kwenye maeneo yanayopata mvua nyingi na/au yaliyo:

- karibu na mji
- karibu na barabara
- karibu na mto
- au karibu na hifadhi ya wanyamapori.

Matokeo mengine muhimu waliyoyatoa yalijumuisha:


- Kilimo kiliongezeka mara tano zaidi kati ya mwaka 1984 hadi 2000 katika eneo la mfumo wa ekolojia la Tarangire-Simanjiro, ambalo kiasili ni eneo la wafugaji na lina wanyamapori wengi (Ramani 3). Hekta zilizolimwa ziliongezeka kutoka kiwango cha 17,000 hadi 88,000 na kiwango cha upanuzi wa maeneo kimekuwa kikiongezeka maradufu kutoka asilimia 0.6 kwa mwaka hadi asilimia 3 kwa mwaka kwa kufikia mwaka 2000.
- Asilimia 35 ya maeneo ya malisho yaliyobaki katika eneo hili la mfumo wa ekolojia kwa sasa lina uwezekano wa wastani, mkubwa au mkubwa sana wa kubadilishwa kuwa maeneo ya kilimo/mashamba katika siku za usoni. Kiwango hicho cha uwezekano ni asilimia 21, 10 na 4.
- Kubadilishwa kwa matumizi ya ardhi tayari kunaleta tishio kwa maeneo matatu maalum wanakopita wanyama wakati wanahama, kati ya maeneo matano yaliyokuwa yamebaki mwaka 2000. Kulikuwa na maeneo kama hayo 9 ya asili yaliyokuwa yanatumika mwaka 1964.
- Idadi ya Nyumbu ilipungua kwa karibu 88% katika kipindi kisichozidi miaka 15 kwenye eneo la mfumo wa ekolojia la Tarangire-Simanjiro, kwa sababu maeneo waliyokuwa wakitumia kuzaliana yaligeuzwa kuwa mashamba (TAWIRI, 2001).
- Kilimo kinaonekana kutokuwa endelevu katika ardhi ya Tarangire-Simanjiro. Kiasi kinachofikia asilimia 70 ya ardhi iliyolimwa mwaka 1984 ilikuwa imetelekezwa mwaka 2000, na karibu eneo lote lililokuwa limelimwa mwaka 2000 lilikuwa jipya. Eneo lililotelekezwa lilikuwa halifai tena kwa mifugo wala mazao (Msofe, et al).
- Hali ya hewa pia sio nzuri kwa kilimo katika maeneo haya. Uchambuzi wa mfumo wa mvua wa muda mrefu ulionesha kuwa ukame mkali hutokea mara moja kila baada ya miaka mitatu ingawa si katika mfumo unaotabirika (Msofe et al). Utabiri wa hali ya hewa na joto wa siku za usoni, na upungufu mkubwa wa kiasi cha mvua katika Afrika Mashariki (Hulme 2001; Thuiller et al., 2006, Ogutu et al 2008), unamaanisha athari nyingine zaidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa wanyamapori katika eneo la mfumo wa ekolojia la Tarangire-Simanjiro.
- Kujirudia kwa ukame na magonjwa kumechangia kushuka kwa mchango wa mifugo katika uchumi baada ya miaka mingi kutokana na kupungua kwa mifugo na kutotabirika kwa mvua kumezidi kuifanya mifugo kutorejea kwenye hali yake ya awali.
- Idadi ya watu imeongezeka maradufu katika kanda hii kwa kipindi cha miaka 25 iliyopita, kumekuwa na ongezeko kwa mwaka la 3.8% kati ya mwaka 1978 na 1988 hadi 5.2% kati ya mwaka 1988 hadi 2002.

Majumuisho ya utafiti ni: mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanachangiwa na sera na mfumo wa umiliki wa ardhi, hali ya uchumi wa jamii (demografia, uchumi mdogo na mkubwa), biofiziolojia na hali ya hewa.

Kurudishia hali ya kutokuwa na kilimo endelevu pamoja na utumiaji haramu wa wanyamapori katika eneo lililofanyiwa utafiti kunahitaji mpango wa matumizi ya ardhi. Kwa kuongezea, miradi ya jamii ya utalii wa wanyamapori ingeongeza kipato na manufaa katika ngazi ya kaya. Maisha endelevu yanahitaji kuwezeshwa kwa haraka.

# Hatua kuelekea mafanikio






*Chanzo:* ILRI, 2007

RAMANI 2: RAMANI ZINAZOONESHA UHUSIANO WA MVUA NA KILIMO KATIKA MAENEO YA HIFADHI

ardhi - hususan kilimo - kuwa ngumu zaidi. Ukame unaongeza matatizo na migogoro iliyopo miongoni na baina ya wakulima, wafugaji, waendelezaji wengine wa ardhi na wanyamapori. Zaidi ya hayo, ongezeko la joto linapunguza zaidi mvua kwenye makazi na hivyo kuendelea kupunguza maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori (Ogutu et al.; 2007; Beehner et al.; 2006).

5. Kwa kusukumwa na mwenendo uliobainishwa hapo juu pamoja na sera za mfumo wa umiliki wa ardhi, wafugaji wa kuhamahama wanaanza kutulia mahali pamoja. Wafugaji waliokuwa wamezoea kuchungia mifugo yao umbali wa mamia ya kilomita kwa mwaka wanalazimika kuchungia katika maeneo maalum na madogo, kwenye kijiji au hata eneo moja katika kijiji, kwa sababu ardhi imebinafsishwa na kugawanywa katika maeneo madogo zaidi. Rasilimali zinaweza zisitoshe katika eneo hilo dogo, kwa hiyo wafugaji wameanza shughuli za kilimo hata kwenye maeneo hayo yenye hali ya ukame ambapo ufugaji wenye kuruhusu kutafuta malisho unabaki kuwa ndio mbadala pekee unaofaa kwa matumizi ya ardhi (ACC 2005, Reid et al 2003). Wafugaji wanaomiliki ardhi pia wanaweza kuongeza kipato kutokana na ardhi kwa kuwekeza katika maendeleo ya ardhi na uzalishaji. Kinachowezesha mabadiliko haya ni uboreshaji wa masoko na miundombinu ya usafiri, mitandao ya taarifa juu ya hali ya masoko, na kufikia huduma ya kifedha (Norton-Griffith na Said).

6. Tofauti na inavyoeleweka, idadi ya mifugo haijaongezeka katika miongo kadhaa iliyopita katika maeneo ya malisho ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Mifugo imehama makao, hata hivyo, pamoja na idadi kuongezeka maradufu katika maeneo yenye mvua za wastani (500-800mm) na kupungua katika maeneo yenye mvua nyingi (Norton-Griffiths na Said, GoK 1995, De Leeuw et al.; 1998).
Kwa mtu mmoja mmoja, mifugo imepungua na hasa

n'gombe. Maisha ya wafugaji yanazidi kuwa magumu siku hadi siku kuhimili, na wafugaji ni miongoni mwa jamii maskini katika Afrika Mashariki.


7. Idadi ya wanyamapori inapungua kwa kasi. Hasa kwa sababu ya mabadiliko yasiyo na mpangilio ya makazi ya wanyamapori kuwa mashamba, Afrika Mashariki imepoteza zaidi ya nusu ya wanyamapori wake katika miaka 30 iliyopita (Norton-Griffiths in press, GoK 1995, de Leeuw et al., 1998). Hali hii inaendelea. Ukweli ni kwamba kwa kukadiria Kenya imepoteza zaidi ya asilimia 70 ya mamalia wote wakubwa katika kipindi cha miaka 30 iliyopita. Kati ya wanyama 12 aina ya wala majani waliofanyiwa utafiti, ni mbuni pekee aliyeonesha kutoshuka kwa idadi katika miongo mitatu iliyopita (Norton-Griffith na Said).

   Nchini Tanzania, takwimu za kuaminika za kisayansi zinaonesha idadi ya wanyamapori kushuka kwa kiasi kikubwa katika hifadhi zote za kitaifa za wanyamapori na maeneo ya mifumo ya ekolojia, zikijumuishwa hifadhi za taifa na hifadhi za wanyamapori. Ukiacha twiga na tembo, mamalia wengine wakubwa wameonesha kupungua idadi toka miaka ya katikati ya 1980. Upotevu huu unatokea pamoja na kwamba asilimia 30 ya ardhi yote imetengwa kwa ajili ya hifadhi za wanyamapori na misitu (TNRF 2008).

8. Kwa sasa, kipato kutokana na wanyamapori hakiwezi kushindana kiuchumi na kilimo. Wanyamapori wamekuwa wakisogezwa kwa ajili ya mabadiliko ya ardhi ya kilimo (Norton-Griffiths et al 2008, Ottichilo et al 2000; Serneel et al 2001). Mchanganuo wa kiuchumi unaonesha kuwa katika Sera ya Mazingira ya sasa, kilimo kinazalisha zaidi kwa hekta moja kuliko wanyamapori hata kwenye maeneo yanayokuwa na idadi kubwa ya watalii (Norton-Griffiths na Said katika Norton-Griffiths et al.; 2008). Bila kubadilisha sera, uchumi utaendelea kufukuzia mbali wanyamapori (Kisanduku namba 4).

9. Hifadhi nyingi za taifa za wanyamapori Afrika Mashariki zinakuwa "visiwa" kwenye bahari ya mashamba (Ramani 3). Ubadilishaji wa ardhi kwa kasi karibu na hifadhi za taifa za wanyamapori mara nyingine inaonesha fursa ya kilimo iliyopo. Lakini pia inaonesha jinsi jamii inavyotamani kuzuia eneo la hifadhi lisiendelee kupanuka na kuingia katika maeneo yao.

   Ulimaji karibu kabisa na mipaka ya hifadhi za taifa za wanyamapori umepunguza mwenendo wa wanyama hawa. Pia inaleta haja ya kuwa na matumizi ya ardhi ambayo yana manufaa kwa jamii na wakati huo huo yanafaa kwa wanyamapori.




*Chanzo:* ILRI, 2007

RAMANI 3: RAMANI ZINAZOONESHA UHUSIANO KATI YA KILIMO NA MAENEO YA HIFADHI KWA MIAKA YA1984 NA 2004

KISANDUKU NAMBA 4: **SIMULIZI YA UHIFADHI MAHIRI KUTOKA NCHINI KENYA**

Hivi karibuni, watafiti walichambua uzalishaji utokanao na ardhi kwa matumizi mbalimbali kwenye ukanda wa Maasai Mara nchini Kenya, kulingana na uoto wa adhi na utafiti katika kaya. Ukanda wa Mara unapata mvua nyingi kuliko eneo la mfumo ekolojia la Tarangire-Simanjiro, hata kama haina mgawanyo sawa. Matokeo yanaonesha kuwa kilimo na ufugaji vinaleta faida zaidi kwa hekta moja kuliko wanyamapori na ndiyo maana tofauti hii ya faida inahamasisha zaidi kuendeleza kilimo kuliko kuhifadhi ardhi. Wanaelezea zaidi juu ya mfumo wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika ukanda wa Mara na maeneo mengine ya Afrika Mashariki (Norton Griffiths et al.; 2008).

Hadi hapo jamii ya vijijini itakapoona wanyamapori wanawafaidisha angalau kama kilimo, wataendelea na kilimo na/au watakodisha au kuuza ardhi kwa watakaoitumia kwa kilimo, ama kwa kilimo cha chakula au cha biashara.

Mifumo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs), biashara zinazohusiana na uhifadhi, na kulipia kwa huduma ya mazingira (PES) ni mbinu za kusawazisha uwanja wa kiuchumi na kuwezesha kuwepo na kuishi kwa shughuli za ufugaji na wanyamapori, hata hivyo mifumo hii miwili inaweza kuishi pamoja (Sura ya 3 na 4 zitaangalia masuala haya kwa undani zaidi).

Katika Ukanda wa Mara, kwa mfano, jamii zinaingia ubia na wawekezaji binafsi kuanzisha hifadhi maalum kama Hifadhi ya Olare Orok (OOC). Ni Hifadhi ya Wanyamapori karibu na Hifadhi ya Taifa ya Maasai Mara, Olare Orok inamilikiwa na wamiliki wa ardhi wa Kimasai wapatao 154, na eneo lina ukubwa wa ekari 23,000. Ilianzishwa mwaka 2006 na inasimamiwa na kampuni ya Olpurkel Ltd, kampuni binafsi iliyoanzishwa na waendeshaji shughuli za kitalii wanne wenye kambi katika eneo la hifadhi hiyo.

Kampuni ya Olpurkel Ltd inakodisha ardhi kutoka kwa OOC kwa mkataba wa miaka mitano na inawajibika kwa usimamizi wa wanyamapori na uendelezaji wa miundombinu, wakati huo huo kuhakikisha kuwa kila mwezi kila mmiliki ardhi inayozidi ekari 150 anapata dola za kimarekani 160. Sehemu ya mkataba pia inaruhusu wamiliki wa ardhi waendelee kutumia hifadhi kwa ajili ya malisho ya mifugo yao wakati wa kipindi cha kiangazi. Hii inawezesha jamii husika kufaidika na uhifadhi wakati huo huo kuendelea na shughuli zao za ufugaji, ambao ndio msingi mkubwa wa kiuchumi wa jamii ya kimasai.

Pia shughuli za ujasiliamali zinazohusiana na uhifadhi zinaongezeka katika Tanzania, zikihamasishwa na kuwepo kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (Angalia Sura ya 4).



*Kulima mazao*

Upotevu wa maeneo ambamo wanyama wanasambaa na kupita utapunguza maeneo ya hifadhi kuwa visiwa vya ki-ekolojia ambapo uhifadhi endelevu wa aina ya wanyamapori unaweza ukashindikana hata kupitia mikakati madhubuti ya usimamizi (Ottichilo et al.; 2000; Newmark 1996).

10. Pamoja na hayo yote, wanyamapori bado ni moja ya rasilimali muhimu ya Afrika Mashariki. Katika nchi ya Tanzania wanyamapori ni kivutio kikubwa cha sekta ya utalii ambapo iliingiza zaidi ya wageni 700,000 mwaka 2007, na zaidi ya dola za kimarekani bilioni 1. Utalii umekuwa sehemu muhimu ya kuboresha na kukuza uchumi katika miongo miwili iliyopita. Wageni nchini Kenya walifika zaidi ya milioni mbili mwaka 2007, na walichangia karibu asilimia 12 ya pato la taifa (GDP).

# Mambo muhimu ya kukumbuka

1 Mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya chini na ya juu zaidi inaweza kusaidia kufikia malengo ya ngazi ya chini na ya kitaifa kwa pamoja. Inaweza kuchangia kwa kina maendeleo vijijini, kuongeza utajiri, kuleta usawa, uhakika wa chakula na uendelevu wa rasilimali.

2 Matumizi ya ardhi yanabadilika kwa kasi Afrika Mashariki katika mfumo usiokuwa na mpangilio, mara nyingi yakiwa na matokeo yenye athari mbaya na yasiyokuwa endelevu. Ubadilishaji wa kasi wa maeneo ya malisho ya wanyamapori na mifugo kuwa mashamba unasababisha: 1) kupungua kwa shughuli za ufugaji kama njia ya kujikimu kimaisha, pamoja na uendelevu wake katika maeneo yaliyo na ukame; na 2) kupungua kwa idadi ya wanyamapori pamoja na umuhimu wake katika uchumi wa taifa. Kuna haja ya kupanga haraka ili kubadilisha mwelekeo huu na kurahisisha ukaaji pamoja wa watumiaji mbalimbali wa ardhi.

3 Katika mazingira ya sera kwa sasa, kilimo ndicho ambacho mara nyingi hutumia ardhi na kuleta faida kubwa katika muda mfupi. Lakini katika maeneo yenye ukame kidogo katika Afrika Mashariki, kilimo kimekuwa si endelevu na kimechangia kuharibu udongo kiasi kwamba sasa si kilimo wala ufugaji unaoweza kuendelea.

4 Sera na hatua zinazoweza kuendeleza jamii za wafugaji pamoja na wanyamapori wanaoishi nao ni kama:

- Kubadilisha sera ili jamii iweze kusimamia na kupata faida kutokana na rasilimali zao, pamoja na wanyamapori.
- Kuruhusu na kuhamasisha jamii wapate faida zaidi na walipwe moja kwa moja kutokana na biashara iliyoendelevu katika ardhi yao.
- Njia nyingine ya kulipwa kupitia huduma ya mfumo wa ekolojia, kama ukodishaji wa hifadhi.
- Elimu na uwezeshwaji ili kuboresha maeneo ya malisho ya mifugo na wanyamapori.
- Kutambua kuwa wafugaji wanahitaji maeneo makubwa ya kutumia kwa ajili ya malisho, na ndiyo njia endelevu zaidi ya maisha katika maeneo yenye ukame.
- Kuwezesha kuwepo kwa njia za mapito ya mifugo na wanyamapori.

Baadhi ya hizi njia zimeongelewa kwa kina katika sura ya 3 na ya 4. Kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya chini angalia Sura ya 2.

Sura ya 1

# Mambo muhimu ya kukumbuka

## FAHARASA

African Conservation Centre (ACC) 2005 Fact Sheet 1.

Beehner, J.C., Onderdonk, D.A., Alberts, S.C., and Altmann, J. 2006. The ecology of conception and pregnancy failure in wild baboons. Behavioral Ecology doi:10.1093/beheco/arl006.

Campbell,D.J., Lusch, D. P., Smucker, T. A., and Wangui, E. E. 2005. Multiple methods in the study of Driving Forces of Land Use and land Cover Change: A Case Study of SE Kajiado District, Kenya. *Human Ecology* **33**: 763-79

de Leeuw, J., H. Prins, H.T., Njuguna, E.C.. Said, M.Y. and de By, R.A. 1998. *Interpretation of DRSRS animal counts (1977-1997) in the rangeland districts of Kenya.* Enschede, The Netherlands: International Institute for Aerospace Survey and Earth Sciences, Enschede.

Etter, A., McAlpine, C., Pullar, D., Possingham, H. 2006. Modelling the conversion of Colombian lowland ecosystems since 1940: Drivers, patterns and rates. Journal of Environmental Management, 79, 74-87.

GOK 1995. *National rangelands report: Summary of population estimates for wildlife and livestock.* Nairobi: Ministry of Planning and National Development (Department of Resource Surveys and Remote Sensing).

GTZ 1999. Land Use Planning, Methods, Strategies, and Tools. Eschborn, Germany, Universum Verlagsanstalt.

Hulme, M. 2001 Climatic perspectives on Sahelian desiccation: 1973-1998. *Global Environmental Change* **11**: 19-29

Lambin, E. F., X. Baulies, N. E. Bockstael, G. Fischer, T. Krug, R. Leemans, and others. 2000. Land-use and land-cover change (LUCC), implementation strategy. IGBP Report 48, IHDP Report 10. Stockholm, Bonn, IGBP, IHDP.

Lamprey, R.H., and Reid, R.S. 2004 Expansion of human settlement in Kenya's Maasai Mara: what future for pastoralism and wildlife? Journal of Biogeography **31**: 997-1032.

Martin-Lopez B, Montes C, Benayas J. 2008. Economic valuation of biodiversity conservation: the meaning of numbers. *Conservation Biology* 22: 624-635.

Msoffe, F., Kifugo, S.C., Said, M., Neselle, M., van Gardingen, P., Reid, R., Ogutu, J., Herrero, M. in prep. Drivers and impacts of land-use change in the Maasai Steppe of Northern Tanzania: An ecological-social-political analysis.

Newmark, W.D. 1996. Insularization of Tanzanian parks and the local extinction of large mammals. *Conservation Biology* **10**: 1549-1556

Nijkamp, P., Vindigni, G., Nunes, P.A.L.D. 2008. Economic valuation of biodiversity: A comparative study. *Ecological Economics 67*: 217-231.

Nkedianye, D. 2003. Testing the Attitudinal Impact of a Conservation Tool Outside a Protected Area: The Case for the Kitengela Wildlife Conservation Lease Programme for Nairobi National Park. MSc. University of Nairobi, Nairobi, Kenya.

Norton-Griffiths, M. 1988. Aerial point sampling for land use surveys. *Journal of Biogeography* 15: 149-156.

Norton-Griffiths, M. and Butt, B. 2006. *The economics of land use change Loitokitok Division, Kajiado District, Kenya.* Lucid Working Paper 34. Nairobi: International Livestock Research Institute.

Norton-Griffiths, M., Said, M.Y., Serneels, S., Kaelo, D.S., Coughenour, M., Lamprey, R.H., Thompson, D.M., and Reid, R.S. 2008. Land use economics in the Mara area of the Serengeti ecosystem. In *Serengeti III: Human Impacts on Ecosystem Dynamics*, ed. A. R. E. Sinclair, C. Packer, S. A. R. Mduma and J. M. Fryxell, 379-416. Chicago University Press.

Norton-Griffiths, M. and Said, M.Y. in press. The future for wildlife on Kenya's rangelands: An economic perspective.

Ogutu, J. O., Piepho, H. P., Dublin, H. T., Bhola, N., and Reid, R. S. 2008. El Nino-Southern Oscillation, rainfall, temperature and Normalized Difference Vegetation Index fluctuations in the Mara-Serengeti ecosystem. *Afr.J.Ecol.* **46**:132-143

OIKOS 2002 Analysis of Migratory movements of large mammals and their interactions with human activities in the Tarangire area Tanzania, as a contribution and sustainable development strategy: Tarangire-Manyara Conservation Project (TCMP)Final Project Report. Istituto Oikos and University of Milan, Italy in collaboration with Tanzania National Parks (TANAPA).

Olff, H and Grant, J 2008. The resource basis of human-wildlife interaction. In *Serengeti III: Human Impacts on Ecosystem Dynamics*, ed. A. R. E. Sinclair, C. Packer, S. A. R. Mduma and J. M. Fryxell, 95-133. Chicago University Press.

Ottichilo, W.K., de Leeuw, J., Skidmore, A.K., Prins, H.H.T. and Said, M.Y. 2001. Population trends of large non-migratory wild herbivores and livestock in the Maasai Mara ecosystem, Kenya 1977-1997. *African Journal of Ecology* **38**: 202-216.

Reid, R. S., Rainy, M.E., Ogutu, J., Kruska, R. L., Kimani, K., Nyabenge, M., McCartney, M., Kshatriya, M., Worden, J.S., Ng'ang'a, L., Owuor, J., Kinoti, J., Njuguna, E., Wilson, C.J. and Lamprey, R.H. 2003. People, wildlife and livestock in the Mara ecosystem: the Mara Count 2002. Nairobi: International Livestock Research Institute.

Reid, R.S., Gichohi, H., Said, M.Y., Nkedianye, D., Ogutu, J.O., Kshatriya, M., Kristjanson, P., Kifugo, S.C., Agatsiva, J.L., Adanje, S.A. and Bagine, R. 2007. Fragmentation of a peri-urban savanna in the Athi-Kaputiei plains, Kenya. In *Fragmentation of Semi-Arid and Arid Landscapes: Consequences for Human and Natural Systems*, ed. K. A. Galvin, R. S. Reid, R. H. Behnke and N. T. Hobbs, 195-224. Dordrecht: Springer.

Serneels, S., Said, M.Y., and Lambin, E.F. 2001 Land cover changes around a//., major east

African wildlife reserve: The Mara ecosystem, Kenya. International Journal of Remote Sensing, **22**:3397-3420.

Serneels, S., and Lambin, E.F. 2001. Proximate causes of land-use change in Narok District, Kenya: a spatial statistical model. *Agriculture, Ecosystems and Environment* **85**:65-81.

Stoner, C.J., Caro, T.M., Mduma, S., Mlingwa, C., Sabuni, G., Borner, M., and Schelten, C. (2006) Changes in large herbivore populations across large areas of Tanzania. *Afr.J.Ecol.* **45**: 202-215.

Tanzania Natural Resources Forum 2008. Wildlife for all Tanzanians: Stopping the loss, nurturing the resource and widening the benefits. *An Information Pack and Policy recommendations.*

TAWIRI 2001. Tarangire Ecosystem: *Wet season Systematic Reconnaissance Flight Count*, May 2001.

Thuiller,W., Broennimann, O., Hughes, G., Alkemades, J. R. M., Midgley, G. F., & Corsi, F. 2006. Vulnerability of African mammals to anthropogenic climate change under conservative land transformation assumptions. *Global Change Biology* **12**: 424- 440.

Verburg 2002 Modeling the Spatial Dynamics of Regional Land Use: The CLUE-S Model. *Environmental Management* **30**:391-405

Western, D., Russell, S. and Mutu, K. 2007. *The status of wildlife in Kenya's protected and non-protected areas.* Paper commissioned by Kenya's Wildlife Policy Review Team and presented at the first Stakeholders Symposium of the Wildlife Policy and Legislation Review 27th To 28th September 2006. Nairobi: African Conservation Centre.

World Resources Institute; Department of Resource Surveys and Remote Sensing, Ministry of Environment and natural Resources, Kenya; Central Bureau of Statistics, Ministry of Planning and National Development, Kenya; and International Livestock Research Institute 2007. Nature's Benefits in Kenya, An Atlas of Ecosystems and Human Well-Being. Washington, DC and Nairobi: World Resources Institute.

# Kujenga picha ya jamii yetu kwa siku zijazo: sababu na jinsi ya kushiriki kupanga matumizi ya ardhi



## KWA NINI TUFANYE MIPANGO SHIRIKISHI YA MATUMIZI YA ARDHI?

Wote tunaiona wazi: watu wameongezeka, miji imekua, mifugo imeongezeka, mashamba mengi zaidi .... Vilevile uharibifu zaidi wa ardhi, uharibifu wa misitu, mmomonyoko wa udongo .... Migogoro mingi zaidi kati ya wakulima na wafugaji, wachimba madini na wafugaji, wanyamapori na watu ....

Mahitaji yetu ya kutumia ardhi yanaongezeka wakati wote, lakini eneo la ardhi haliongezeki. Tutafanyaje ili tuwe na matumizi mazuri na ya kuridhisha ya ardhi tuliyonayo, katika mazingira ya hali ya tabianchi na maliasili, pamoja na tamaduni zetu, njia tunazotumia kumudu maisha, matarajio na ndoto za jamii yetu?

Kujibu swali hili ndilo lengo la kupanga matumizi ya ardhi. Na kwa sababu ardhi ni ya msingi kwa jamii, mpango wa matumizi ya ardhi unakuwa bora pale tu jamii inaposhiriki kikamilifu kwenye mchakato. Hapo ndipo linapokamilika suala la "ushirikishwaji" kwenye mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi, yaani LUP.

*"Binadamu tunaongezeka. Lakini ardhi haiongezeki. Kwa hiyo tunapaswa kupanga matumizi ya ardhi ili iendelee kutosha kwa mahitaji yetu."*

*Seraphino Bichabicha Mawanja, Ofisa Wanyamapori, Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Tanzania*

## UMUHIMU WA SURA HII

Sura hii imeandaliwa:

- Kukufahamisha yale yanayotarajiwa wakati wa mchakato wa kupanga matumizi ya ardhi.
- Kukupa uzoefu kutoka kwa jamii nyinginezo na pia kutoka kwa wataalamu wa kupanga.
- Kukupa ari ya kujadili masuala yanayohusu matumizi ya ardhi hata kabla ya kuuanza mchakato huo, ili kuwezesha ushiriki mkubwa wa jamii.

### Sura yenyewe

- Inaangalia hatua za mchakato ambapo ushiriki wa jamii ni muhimu sana.
- Maelekezo yaliyomo katika sura hii yanapaswa kutumiwa kwa pamoja na mwongozo wa serikali, ambao unabainisha kwa undani masuala ya kitaalam na kisheria juu ya upangaji wa matumizi ya ardhi. Tazama Kiambatanisho 3, Jedwali 2, cha ngazi zilizokubalika za kupanga matumizi ya ardhi nchini Tanzania.

## KUPANGA MATUMIZI YA ARDHI KUTAISAIDIAJE JAMII?

Mpango Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi (PLUP) ni mchakato unaomhusisha kila mmoja kwenye jamii, pamoja na wataalamu husika. Mpango huu unahusisha kufanyika mikutano mingi katika kipindi

# Utangulizi



kipatacho mwaka mmoja au zaidi. Kwa ujumla, mpango wenyewe unaleta faida nyingi, za muda mfupi na mrefu.

Mpango Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi unaisaidia jamii:

- kutatua migogoro ya matumzi ya ardhi iliyopo – na kuzuia migogoro kama hiyo kutokea siku za baadaye.
- kuwafanya wakazi wakae pamoja kufikiria jinsi ya kuboresha hali ya baadaye, na kuanza kuiandaa.
- kupata umiliki wa ardhi na hati miliki za ardhi ambayo jamii inaimiliki kimila.
- kuboresha faida zinazoweza kupatikana katika kila eneo la ardhi, kutegemea na aina yake.
- kutumia ardhi, maji, wanyamapori na maliasili nyinginezo katika njia inayokubalika, ya uwazi,

## INAWEZEKANA? MTAZAMO KUTOKA KIJIJINI...

Kijiji cha Loiborsiret, kilichopo wilaya ya Monduli, ni moja kati ya vijiji sita Kaskazini mwa Tanzania vilivyotekeleza Mpango Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi katika miaka michache iliyopita. Wakati mchakato wa Mpango Shirikishi wa Matumizi ya Adhi ulipoanza, migogoro ilikuwa inaibuka:

- kati ya wafugaji juu ya kupungua kwa sehemu za malisho pia maji;
- kati ya wakulima na wafugaji kuhusu wapi pa kulima na wapi pa kulisha mifugo;
- kati ya wale wanaojihusisha na uhifadhi na wale ambao mifugo yao ilikuwa ikishambuliwa na simba;
- kati ya wanaofanya utalii wa kupiga picha na wale wa utalii wa uwindaji;
- kati ya wazawa kijijini na wageni kutoka sehemu nyinginezo; na
- Kati ya kijiji kimoja na vijiji jirani na pia hifadhi za wanyamapori, juu ya mipaka.

Kwa kipindi cha miaka miwili, wanavijiji wamefanya kazi kwa bidii wakishirikiana na timu ya watendaji, wataalamu wa mipango, wanasayansi, wasuluhishi wa migogoro na wawezeshaji kutoka kwenye mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

Wawakilishi wa wanavijiji pamoja na wataalamu waliunda timu shirikishi ya kusimamia matumizi ya ardhi (PLUM) ambayo ndiyo iliyoongoza mchakato.

Timu ya PLUM na wanajamii wengine:

- walitatua migogoro sugu iliyokwisha dumu kwa muda mrefu, wakati mwingine wakisuluhisha vikundi vilivyokuwa vinakinzana;
- waliainisha na kuweka wazi mipaka ya kijiji hivyo kuwezesha mchakato kusonga mbele;
- walifanikisha wanavijiji kupata hati za kumiliki ardhi – wakianza na wajane ambao ni kati ya wanajamii walio dhaifu;
- walisaidia vijiji kukubaliana juu ya sehemu za kulima, kulisha mifugo kwa mwaka mzima, malisho wakati wa kiangazi, makazi, biashara, na eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, ambayo nayo itakuwa ni eneo la peke yake; na
- walitunga sheria ndogo na kukubaliana namna ya kuzisimamia, ikiwa ni pamoja na kulipa faini au adhabu nyinginezo kwa kukiuka makubaliano ya mipaka ya maeneo yaliyotengwa kwa kila shughuli.

Siyo kwamba kila mtu alifurahia mpango huo, lakini kikubwa wanachokiona ni uhakika wa usalama, usawa na matumaini mapya juu ya mustakabali wa ardhi yao kwa siku zijazo. Wanasema kwa kiasi fulani mafanikio haya yanatokana na mchakato wenyewe ulivyoendeshwa na pia ule utaratibu wa kutatua migogoro kwa kushirikisha jamii.

Yafuatayo ni baadhi ya maoni ya washiriki wa mpango shirikishi

***“Tunafaidika kutokana na mipango mipya wa matumizi ya ardhi kwani imepunguza migogoro inayohusiana na ardhi. Vilevile, kutokana na mafunzo, watu sasa wanajua sheria za ardhi. Hata wanafunzi nao sasa wanafundishwa sheria za ardhi shuleni.”***

*Mwenyekiti wa Kijiji*

***“Kinachonifurahisha zaidi kwenye mchakato wa mpango wa matumizi ya ardhi ni ule ugawaji ardhi kwa kufuata umiliki wa kijadi – kuanzia maeneo yanayomilikiwa na wajane, kwa sababu wao wanaathirika zaidi.”***

*Mwanakijiji*

***“Watu hawawezi tena kuvamia ardhi na kuitumia vibaya kwa kuwa ardhi yote katika kijiji imegawanywa kwenye matumizi mbalimbali. Kama mtu atataka sehemu ya ardhi, kijiji chote kitajua. Watalazimika kufuata taratibu zilizowekwa ili anayetaka ardhi aweze kupewa.”***

*Mwanakijiji kijana*

iliyoendelevu kwa kadiri siku zinavyokwenda mbele na yenye manufaa.

Kumbuka kuwa, hapa nchini Tanzania sheria yetu inaitaka jamii kupanga mpango wa matumizi ya ardhi endapo jamii itapenda:

- kuanzisha na kusimamia Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) au msitu wa jamii.
- kuanzisha biashara zinazomilikiwa na jamii zinazohusiana na wanyamapori na maliasili nyinginezo.

*"Mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji ni mchakato wa kutathmini na kupendekeza njia mbalimbali za matumizi ya maliasili ili kuboresha hali ya maisha ya wanakijiji."*

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji nchini Tanzania, 1998*

## NI NANI ANAHUSIKA KWENYE MPANGO SHIRIKISHI WA MATUMIZI YA ARDHI?

Viongozi wa kijiji, viongozi wa wilaya, wajumbe wa wizara yenye dhamana ya mipango, pia wanaweza kuwepo wawezeshaji wa taasisi zisizokuwa za kiserikali.

Na muhimu zaidi: wana jamii, aidha "wanakijiji," "wanachama wa ranchi ya pamoja" au "wakazi wa kawaida". Katika Sura hii, neno "wanakijiji" litatumika kumaanisha wakazi wote waliomo kijijini.

Uhusishwaji ni muhimu si tu kwa wale wenye madaraka au elimu, au utajiri, au wanaume, au wazee, bali ni watu wanaowakilisha makundi yote kwenye jamii: wanawake wazee, wanawake vijana, wanaume wazee, wanaume vijana, matajiri, wakulima, wafugaji .... (Tazama Jedwali namba 1).

Kwa kawaida mchakato utaongozwa na timu ya Usimamizi wa Matumizi Shirikishi ya Ardhi (PLUM). Timu hii inajumuisha viongozi wa kijiji na wawakilishi wa makundi mbalimbali ya jamii kwenye kijiji, na vile vile inaweza kujumuisha wataalamu wa masuala ya udongo, mimea na maliasili; wataalamu wa mipango; watendaji wa serikali; na wataalamu wengine kadiri itakavyohitajika.

Wakati wa mchakato, jamii itaunda Kamati ya Kijiji ya Kusimamia Matumizi ya Ardhi (VLUM) ili isaidie kwenye kutekeleza na kuendeleza usimamiaji wa matumizi ya ardhi kama ambavyo jamii itakuwa imekubaliana. Wanavijiji wenye utaalamu kijijini wataajiriwa na kufundishwa juu ya mbinu za usimamiaji wa matumizi ya ardhi.

Taasisi zisizokuwa za kiserikali na wafadhili wanaweza kuwapatia wajumbe wa PLUM na VLUM, wataalamu waliochaguliwa kijijini na watu wengine mafunzo juu ya jinsi ya kuboresha matumizi ya ardhi, sheria, uwezeshaji na mambo mengine mbalimbali juu ya usimamizi wa matumizi ya ardhi. Wanaweza vile vile kusaidia kutafuta utaalamu kutoka nje ya kijiji ili kuisadia jamii ifikie malengo yake.

## NI MASUALA GANI MUHIMU, YATOAYO MWONGOZO WA KUPANGA MATUMIZI YA ARDHI?

- **Ufanisi.** Tumia kila sehemu ya ardhi kupata manufaa makubwa iwezekanavyo. Kwa mfano, unaweza kuwa unataka kulima. Lakini katika eneo kame, udongo unaweza usikupatie mazao mengi, lakini ukaweza kupata mapato mengi kutokana na shughuli nyinginezo katika eneo hilo, kama ufugaji au utalii wa wanyamapori. Katika sehemu nyingine ambapo mvua ni nyingi, kilimo kinaweza kuwa cha manufaa zaidi.
- **Uendelevu.** Pamoja na uhusiano wake na ufanisi, uendelevu unamaanisha kwamba ardhi ibaki na uwezo wa kuzalisha kwa vizazi vingi. Kwa mfano, kilimo si endelevu iwapo udongo ni wa aina inayoharibika baada ya kulimwa kwa mwaka mmoja au miwili. Ardhi ya aina hiyo inaweza kuwa na manufaa kwa muda mfupi lakini manufaa hayo yasiwe ya muda mrefu na hata kuweza kuiharibu ardhi isifae kwa matumizi mengineyo baadaye.
- **Usawa.** Zingatia mawazo yote na mahitaji. Kupanga kunapaswa kuleta manufaa kwa wote: maskini, matajiri, wanawake, wanaume, watoto, wazee, vijana, wageni, kaya ambazo wakuu wake ni wanawake ...
- **Utoaji maamuzi ulio bora katika jamii.** Ukifanyika vizuri, mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi unasaidia kutatua migogoro na kuimarisha utaratibu wa kufanya maamuzi kwenye ngazi ya jamii. Matokeo haya yanapingana na upangaji wa kizamani, uliokuwa unafanywa na wataalamu kutoka nje na kuletwa tu kwenye jamii na hivyo mara nyingi jamii kutozijali na kutozizingatia.

## HIVYO PA KUANZIA NI WAPI?

Ufuatao ni mtiririko na shughuli za kawaida zilizomo kwenye mpango shirikishi. Inawezekana kutumia baadhi yake au zote. Vilevile zinaweza kutumiwa katika mpangilio wowote. Mtiririko huo unaweza kutumika kwa teknolojia tofauti tofauti (kwa mfano, kuchora kwa mkono ramani ya maliasili ikilinganishwa na ile inayoweza kuchorwa kwa teknolojia ya hali ya juu kama kompyuta).

# Utangulizi



JEDWALI NAMBA 1: MGAWANYO WA MAJUKUMU KISHERIA KWENYE SHUGHULI ZA MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI KATIKA NGAZI MBALIMBALI


| Ngazi | Jukumu | Shughuli |
|---|---|---|
| Ngazi ya Wilaya (Halmashauri ya Wilaya) | • Ina mamlaka ya kuunda Kamati ya Wilaya ya Kusimamia Ardhi, itakayosaidia katika kusimamia ardhi.<br>• Itaanzisha, kuongoza na kusimamia Halmashauri za Vijiji katika mchakato wa mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi. | • Kusimamia masuala yote na shughuli za ardhi katika wilaya, kwa mamlaka yaliyotolewa na Mkuu wa Wilaya kama kugawa ardhi kwa ajili ya makazi, biashara na huduma za jamii.<br>• Kuwagawia wakulima maeneo yasiyozidi eka 100 kwa ajili ya kilimo.<br>• Kuunda timu ya wilaya ya kusimamia matumizi ya ardhi na timu ya PRA itakayofanya kazi vijijini. |
| Ngazi ya kijiji | a) Timu Shirikishi ya Kusimamia Matumizi ya Ardhi. | • Itaanzisha na kuongoza mchakato wa mpango shirikishi na utekelezaji wake kijijini. |
| | b) Mkutano Mkuu wa Kijiji ndicho chombo kikuu cha kufanya maamuzi kwenye ngazi ya kijiji. | • Inapitisha mambo yote yanayokuwa yamekubalika katika kijiji. |
| | c) Halmashauri ya Kijiji ina jukumu la kusimamia ardhi yote ndani ya mipaka ya kijiji (mamlaka ya kiutendaji).<br>• Imepewa mamlaka ya kuunda kamati ya VLUM ili isaidie katika kupanga matumizi ya ardhi.<br>• Imepewa mamlaka kutayarisha sheria ndogo za kijiji. | • Kutoa hati za haki za umiliki wa kimila.<br>• Kutunza regista ya ardhi ya kijiji. |
| | d) Kamati ya VLUM | • Inafanya kazi na timu ya PLUM.<br>• Kumsaidia Mwenyekiti wa Kijiji kuanda mikutano, kuwahamasisha wanakijiji, kuainisha na kutatua migogoro ya ardhi, kuandaa mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi, sheria ndogo na kadhalika. |
| | e) Viongozi wa Kitongoji | • Kuandaa mikutano kwenye vitongoji na kuwasiliana na pia kupeleka mawazo na mapendekezo kwenye VLUM na Halmashauri za Vijiji. |
| | f) Wakuu wa koo na Viongozi wa Vijiji | • Wana jukumu muhimu la kukutanisha wanaotofautiana, kusuluhisha migogoro juu ya mipaka, umiliki na haki za watumiaji ardhi. |
| | g) Wataalamu waliochaguliwa Kijijini | • Wanapata mafunzo wakiwa kazini juu ya jinsi ya kuwasaidia wanavijiji wengine katika kutumia matumizi ya ardhi yaliyopendekezwa kama timu ya PLUM haipo. |
| | h) Wadau wengine muhimu (taasisi zisizokuwa za kiserikali, mashirika ya kijamii, wafadhili, n.k.) | • Huvisaidia vijiji kwenye huduma za jamii, masuala ya jinsia, mafunzo kuhusu mazingira, kuhamasisha jamii, miradi ya mikopo, mipango ya matumizi ya ardhi, n.k. |

Kwa namna yoyote ile zitakavyoandaliwa, shughuli hizi zinasaidia jamii katika:

- Kuainisha maliasili waliyonayo na matatizo yanayohusiana nayo
- Kuchanganua jinsi matatizo yalivyoibuka na jinsi yanavyoweza kutatuliwa
- Kuchagua njia nzuri zaidi za kutatua matatizo kwa misingi ya mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi, kama yalivyoainishwa hapo juu
- Kutekeleza maamuzi, kupata taarifa za kitaalam zinazohitajika kutoka ndani na nje ya jamii
- Kutoka kwenye kupanga na kutatua matatizo ya papo kwa papo kuelekea kwenye mpango wa muda mrefu wa kusimamia ardhi.

*KUPANGA MAPEMA KUNAMAANISHA KUWA NA UWANJA MPANA WA KUCHAGUA KATI YA FURSA NYINGI ZINAZOWEZEKANA*

***Jinsi upangaji unavyofanywa mapema ndivyo uwanja mpana wa matumizi unavyoweza kupatikana. Ukipanga mapema unaweza kuwa na fursa kumi tofauti. Utakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kurekebisha au kubadili mpango, utapunguza zaidi migogoro pia. Kuchelewa kupanga kunamaanisha kuwa na uwanja finyu wa kufikiria. Tayari kutakuwa na mambo ambayo yamekwishatokea, mengine hata usiyoyataka, lakini tayari yanakuwepo. Jinsi unavyozidi kuchelewa kupanga, ndivyo unaongeza uwezekano wa mgongano wa maslahi.***




*Mzee maarufu kijijini akimkaribisha mjumbe wa timu ya PLUM*

## HATUA YA KWANZA: KUANDAA NA KUJENGA PICHA YA MATUMIZI YA ARDHI[1]

### Unda na kufundisha timu za PLUM na VLUM.

Anza kwa kuunda timu ya PLUM, ambayo itakuwa na wawakilishi kutoka vikundi vyote vyenye maslahi kwenye ardhi. Hawa watakuwa kiunganishi kati ya uongozi wa kijiji na wilaya na pia wataalamu wanaoweza kusaidia. PLUM itaanza kukutana na jamii kujua mawazo yao. Kwa kuongezea, watakuwa pia wanaunda kamati nyinginezo, kama za PRA na timu ya kijiji ya kusimamia matumizi ya ardhi.

Timu za PLUM na VLUM, pamoja na wataalamu kutoka wilayani watapata mafunzo juu ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, mipango shirikishi, kutengeneza ramani ya matumizi, usimamizi wa matumizi ya ardhi na utatuzi wa migogoro. Wanaweza kwenda kwenye safari za mafunzo ili kujifunza kutoka kwenye uzoefu na changamoto ambazo jamii nyingine zimekutana nazo, na hivyo wanaweza kuja kuzisimulia kwenye jamii yao, ziwe ni zile za kufurahisha na hata zile ambazo si za kufurahisha.

Jambo muhimu zaidi ni kwa timu za PLUM na VLUM pamoja na wenyeji kuunda "darasa la jamii": kundi ambalo limejikita katika kufuatilia na kufahamu kinachotokea, kile ambacho jamii inapenda kuona kinatokea, na jinsi ya kufanikisha kufikia walicholenga. Katika kufanikisha hilo, nyenzo mbalimbali zitatumika, kuwahusisha jamii kutoa mawazo yao, kutatua matatizo na kupanga mipango ya baadaye iliyo bora zaidi.

### Zoezi la kuchora ramani ya kijiji: Nini kinaonekana kwenye ardhi ?

Ramani, hata ambazo siyo rasmi, zinarahisisha kufikiria na kuongea juu ya matumizi mbalimbali ya ardhi.

Tembea kijijini ukiwa na wanakijiji, au angalau simama chini ya mti mahala fulani kijijini na uwape nafasi wanakijiji kuainisha vitu mbalimbali wanavyoviona. Ni mambo gani yanayotokea kwenye ardhi na ni yapi yaliyo katika mwelekeo wa kubadilika?

Timu ya PLUM inaweza kuihamasisha jamii kuchora ramani isiyo rasmi ikionesha yale wanayoyaona. Ijapokuwa sio rasmi, ramani kama hizi ni muhimu. Mawe au mistari kwenye udongo vinaweza kutumika

[1] Awamu zilizotajwa katika sehemu hii zinahusu Ngazi za Upangaji kwenye Ngazi ya Kijiji kama ilivyoandaliwa na Kamisheni ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi (TNLUPC). (Inapatikana kwenye http://www.nlupc.co/tz/aboutus.php.) Hata hivyo, zimehaririwa kidogo na mpangilio wake kubadlishwa katika sehemu chache ili kuwezesha kuingiza kwenye sehemu hii utafiti uliofanyika na mtazamo ngazi ya jamii, na kukazia mchango wa jamii kwenye mchakato.
Ngazi ya kwanza inaongelea zaidi juu ya hatua zilizojadiliwa na TNLUPC: Hatua 1: Maandalizi na mafunzo; Hatua 2: PRA; na Hatua 3: Tafiti za ziada.

# Hatua kuelekea mafanikio



**UZOEFU KUTOKANA NA SAFARI YA MAFUNZO**

Timu za PLUM na VLUM kutoka kijiji cha Loiborsiret zilitembelea mradi wa Mbomipa, ambao umefanikiwa kukamilisha mpango wa matumizi ya ardhi. Baadhi ya mambo waliyojifunza ni haya yafuatayo:

1. Katika mradi wa Mbomipa kuna kitalu cha uwindaji. Malipo ya uwindaji - ambayo yanaweza kuyazidi sana yale ya utalii wa kupiga picha - yanakwenda moja kwa moja kwenye serikali kuu, ingawa sehemu ya mapato hurudishwa katika wilaya baadaye. Mbomipa waliona kuwa na Jumuiya ya Hiafdhi ya Wanayamapori (WMA) kunaweza kuwa na manufaa sana kwani kijiji kinaweza kuwalipisha wawindaji moja kwa moja. Waliweza kuanzisha WMA na kuzishawishi kampuni za uwindaji kukisaidia kijiji katika miradi ya maendeleo: barabara yenye urefu wa kilometa 121 kutoka Iringa hadi kijijini. Inaelekea kuwa hili lisingeliwezekana bila ya kuwepo taratibu za WMA.
2. "Soko la wanyamapori". Wanakijiji wanaweza kuwinda kisheria kwenye ardhi yao kupitia mpango wa "uwindaji wa wenyeji". Wakishawinda, wanaweza kuuza nyama ya wanyamapori na ngozi kwenye soko huria. Mbomipa imetumia mapato yaliyotokana na uwindaji wa wenyeji kujenga shule ya msingi na ya sekondari.


kuonesha mambo fulani fulani. Ramani zinaweza vile vile kuchorwa kwenye karatasi. Baada ya kuzijadili na kurekebishwa, zinaweza kuwekwa rangi au kushonwa kwenye vitambaa (kwa namna hii zinaweza kudumu na kukunjwa/kukunjuliwa na kutumiwa mara nyingi). Baadaye ramani hizi zinaweza kusahihishwa na wataalamu. Hata hivyo zile zinazochorwa na jamii bado zina umuhimu mkubwa wakati wa kupanga.

Wanaume na wanawake wanaweza kuandaa ramani tofauti, kwa sababu rasilimali wanazotumia mara nyingi huwa tofauti.

## Ramani za jamii zaweza kuonesha yafuatayo:

*Maliasili*

- Mipaka ya kijiji
- Mito, maziwa na vyanzo vingine vya maji
- Ardhi chepechepe (ardhi oevu)
- Malisho
- Malisho wakati wa kiangazi




*Mfano wa ramani iliyochorwa kwa mkono ya kijiji cha Naitolia – Wilaya ya Monduli*

- Malisho ya wakati wote wa mwaka
- Mazao yaliyopandwa
- Sehemu zilizo kame zaidi
- Sehemu zenye mvua nyingi/unyevu mwingi
- Misitu na matumizi yake
- Sehemu zenye mimea ya mitishamba
- Sehemu za ibada au shughuli maalum za kimila
- Sehemu zenye uzio
- Sehemu ambazo wanyamapori hukutana


*Miundombinu*

- Makazi
- Maduka
- Masoko
- Barabara
- Shule
- Makanisa
- Kliniki au huduma nyingine za afya
- Taasisi zisizokuwa za kiserikali au taasisi nyingine

*Migogoro*

- Sehemu zenye rasilimali zinazogombewa. Zinaweza kuwekewa alama ya "x".

# Hatua kuelekea mafanikio


Wanakijiji wakikusanya taarifa wakati wa kutembea kijijini kwa ajili hiyo

*Mienendo ya shughuli za kijiji/wanakijiji: (hii yaweza kuonyeshwa kwenye ramani hiyo hiyo au nyingine)*

- Maeneo ambapo wageni kutoka nje ya kijiji huja
- Maeneo ambayo wanakijiji hutoka nje ya mipaka ya kijiji chao wakifuata maliasili (kama malisho wakati wa kiangazi, au maji). Onesha kwa mishale uelekeo waendao watu kama patakuwa nje ya ramani inapoishia
- Mahali wanapopelekwa ng'ombe katika majira tofauti ya mwaka
- Mahali wanapohamia wanyamapori kwa mfano mahali wanapokwenda kwa kuzaa

**Kutembea kijijini.** Kuangalia mandhari kwa karibu. Wakati wa kutembea kijijini ili kuona kila kitu kwa karibu, wanakijiji waorodheshe kila kitu wanachokiona watembeapo wakifuata mstari ulionyooka, sambamba na maeneo mengine ambayo wameshafanya matembezi ya aina hiyo. Wanaweza kuorodhesha mambo fulani fulani kwa undani, kama palipo na miti ya umaarufu fulani, au mimea ya mitishamba. Wanaweza pia kuongeza mambo ya kiuchumi au fursa wazionazo, na pia vikwazo vinavyohitaji kuondolewa ili fursa hizo zitumike (Tazama Jedwali namba 2).

## Kuchora ramani na kupanga kama nyenzo za kuhakikisha kunakuwa na usawa

Wakati wa kujadili ramani, fikiria ni nani anafanya nini na nani anahitaji nini. Kwa kuzingatia usawa, jadili majukumu

**JEDWALI NAMBA 2: MFANO WA TAKWIMU ZILIZOKUSANYWA WAKATI WA KUTEMBELEA KIJIJI NA KUONA MAMBO KWA UKARIBU KUPITIA NJIA NNE HUKO LOIBORSIRET**

| | Kitongoji 1 | Kitongoji 2 | Kitongoji 3 | Kitongoji 4 |
|---|---|---|---|---|
| Uoto wa ardhi | • Miti ya asili<br>• Majani mafupi | • Miti ya asili<br>• Majani mafupi | • Miti na majani mafupi | • Miti mifupi na majani |
| Huduma za kiuchumi | • Mashamba<br>• Mifugo | • Mashamba (mahindi na maharage)<br>• Mifugo | • Kilimo (mahindi)<br>• Mifugo | • Uchimbaji madini<br>• Kilimo<br>• Mifugo |
| Makazi | • Yamesambaa kwenye eneo kubwa | • Yamesambaa kwenye eneo kubwa | • Yamesambaa kwenye eneo kubwa | • Yako katika msongamano |
| Huduma za jamii | • Barabara<br>• Bwawa la maji | • Barabara<br>• Bwawa la maji | • Mashine mbili za kusaga nafaka<br>• Barabara, soko, bwawa la maji | • Kanisa, shule, Msikiti, mashine ya kusaga nafaka, maduka, kisima cha maji na barabara |
| Fursa zilizopo | • Bwawa la maji<br>• Ardhi kwa kilimo<br>• Wanyamapori | • Josho la kuogesha mifugo, miti ya kujengea<br>• Soko, bwawa la maji<br>• Ardhi kwa kilimo<br>• Wanyamapori | • Bwawa la maji<br>• Wanyamapori | • Vito<br>• Uchimbaji madini |

waliyonayo watu tofauti, na jinsi hali ya maliasili inavyohusiana na majukumu hayo (na, kinyume chake, nani aliye na muda wa kusimamia vizuri zaidi maliasili).

- Ni rasilimali zipi zipo kwa wingi au zinaongezeka? Kwa nini?
- Hali hii inawaathiri vipi wanaume, wanawake, wanakijiji, hata na wahamiaji?
- Ni rasilimali zipi ni kidogo au zinazopungua? Kwa nini?
- Hali hii ina athari gani kwa makundi mbalimbali ya watu?
- Kwa sasa inachukua muda gani kuteka maji ikilinganishwa na miaka iliyopita?
- Inachukua muda gani kuokota kuni?
- Mifugo inachungwa wapi, katika misimu tofauti ya mwaka?
- Je inawapasa wanaume kutembea mwendo fulani wanapokwenda machungani? Ni umbali gani na ni wakati gani? Unaweza kulinganisha vipi na ilivyokuwa siku zilizopita?
- Je watu huenda mara kwa mara katika vijiji jirani ili kutumia rasilimali za huko (mfano maji na malisho)? Je, watu kutoka vijiji jirani huja kutumia raslimali za kijiji chako? Kama hali iko hivyo, fikiria kupanga pamoja na vijiji hivyo.

### Mpangilio wa shughuli za siku

Njia nyingine maarufu ni ya kuangalia shughuli zifanywazo kwa siku (Mchoro namba 1). Kwa kutumia kundi la wanawake, na kundi la wanaume, angalia saa zote za siku na kuona kila kundi linavyotumia muda wake. Waweza kuangalia matumizi ya muda kwa siku za kipindi cha masika na siku za kipindi cha kiangazi. Kalenda ya kila siku yaweza kutumika:

- Kuibua majadiliano kuhusu masuala ya kijinsia kwa kulinganisha matumizi ya muda kwa wanawake na wanaume; wasichana na wavulana na jinsi tofauti hizi zinavyoathiri kazi, afya, elimu na mambo mengine.
- kuchanganua usahihi wa muda shughuli hizi zinapofanyika.
- Kujadili shughuli mpya na zinavyoweza kuwa na matokeo fulani kwa muda unaotumika na makundi mbalimbali.
- Kufikiria njia za kuleta usawa katika kutekeleza majukumu na kusimamia rasilimali.

## HATUA YA PILI: KUPIGA PICHA JUU YA HALI YA BAADAYE NA KUANGALIA FURSA ZAKE[2]

### Mabadiliko huja bila kujali kama tuko tayari au la

*Mabadiliko hayakwepeki. Yanakuja na hayawezi kuzuilika.*
*Lakini tunaweza kusimamia jinsi yanavyoathiri maisha yetu ili yasiharibu masuala yetu ya kijamii au rasilimali zetu.*
*Tukiyasimamia, kuna uwezekano mkubwa wa kutotuletea migogoro mingi.*
*Kama hutaweza kuyamudu mabadiliko, yanaweza kuharibu mihimili unayoitegemea katika kumudu maisha yako. Usipopanga, jiandae kwa migogoro mingi na mengi yatakayokushangaza – ambapo mengi yake hayatakuwa ya kupendeza.*

*David Nkedianye*
*Mwanasosholojia wa nyika za malisho na jamii*
*Kenya*

### Tabiri mwenendo wa sasa. Iwapo mambo yataendelea kama yalivyo sasa....

- Kama mabadiliko yaliyojitokeza kwenye kuchora ramani na majadiliano yanaendelea kutokea, ni migogoro ipi yaweza kujitokeza katika miaka mitano ijayo?
- Ni mabadiliko yapi ya ajira/kazi na majukumu yatajitokeza kwa wanaume? Kwa wanawake je? Je kwa wasichana? Na kwa wavulana je?
- Jamii yako yaweza kuonekanaje katika miaka mitano ijayo? Katika miaka kumi? Na katika miaka ishirini?
- Nani watafaidika kutokana na mabadiliko hayo?
- Nani watakaopata shida kutokana na mabadiliko hayo?
- Je hii ni hali ambayo mngependa itokee kweli?









### Ndoto...

Ungependa jamii yako iwe katika hali gani katika miaka mitano ijayo? Miaka kumi je? Miaka ishirini je?

Makundi mbalimbali kwenye jamii yanaweza kuja na "picha ya ndoto" zao za hali wanayotaka ya kijiji chao kiwe nayo siku za usoni. Wanaweza kuweka vitu kama njia mbalimbali muhimu wanayoitegemea katika

[2] Awamu ya Pili inahusiana na hatua ya 4 kwenye NLUPC – Mpango na usimamiaji shirikishi wa Kijiji wa matumizi ya ardhi



| Muda | Baba | Mama | Mvulana | Msichana |
|---|---|---|---|---|
|  | • kuamka<br>• kukagua ng'ombe<br>• kusimamia kazi | • kuamka<br>• kuandaa chai na chakula | • kuamka<br>• kutibu mifugo wagonjwa | • kuamka<br>• kukandika kuta au bati |
|  | • kunywa chai<br>• kupanga kazi | • kuchota maji, kufanya usafi | • kunywa chai | • kunywa chai<br>• kumsaidia mama |
|  | • kuangalia mifugo, kuwanywesha maji | • kusafisha banda la mifugo<br>• kuokota kuni na kuchota maji | • kuangalia ng'ombe<br>• kuwanywesha mifugo maji | • kuokota kuni au kuchota maji |
|  | • kurandaranda kijijini<br>• kujumuika na wengine hadi saa 9 jioni | • kuuza kazi za mikono (kama shanga na bangili)<br>• kuandaa chakula, kuosha vyombo, kukusanya kuni | • kuangalia mifugo au kupumzika | • kuwaangalia watoto wadogo au kupumzika |
|  | • kukagua ng'ombe warudipo toka machungani | • kupokea na kuhesabu mifugo | • kuwarudisha mifugo nyumbani | • kumsaidia mama katika shughuli zote |
|  | • kupumzika<br>• kujumuika kwenye viburudisho, kuongea na kupokea wageni | • kukamua ng'ombe | • kuangalia ndama | • kuosha vyombo |
|  | • kupumzika<br>• kula | • kupika na kupakua chakula | • kula<br>• kupumzika | • kula |
|  | • kulala | • kuosha vyombo | • kulala | • kumsaidia mama |
|  | • kulala | • kulala | • kulala | • kulala |
| Jumla ya saa za kazi | 7 | 16 | 9 | 14 |

MCHORO NAMBA 1: MFANO WA KALENDA YA KILA SIKU IKIONESHA MATUMIZI YA RASILIMALI NA MAJUKUMU KIJINSIA

# Hatua kuelekea mafanikio



## KUMBUKA... WAULIZE WAZEE HALI ILIKUWAJE MIAKA ILIYOPITA.

- Ni kipindi gani hali ilikuwa nzuri? Ni kitu gani kiliifanya iwe nzuri?
- Ni kipindi gani kilikuwa kigumu zaidi? Ni kitu gani kilikifanya kiwe kigumu?
- Vipindi hivyo vilikuwa vizuri, au vibaya, kwa kila mtu?
- Ni akina nani walifaidika nacho na nani walioumia zaidi?
- Ni kitu gani kimebadilika na kuwa kizuri jinsi miaka ilivyoendelea kupita?
- Ni kitu gani kimebadilika na kuwa kibaya jinsi miaka ilivyoendelea kupita?
- Ni kitu gani ambacho makundi tofauti kwenye jamii yangependa kiendelee kubaki katika hali ile ile au ni kipi wangependa kiachwe?

**Nyakati.** Kwa mtazamo mwingine wa kuangalia mabadiliko ya masuala ya maliasili kwa kipindi fulani, ainisha mtiririko wa matukio kwa nyakati tofauti ukionesha matukio muhimu. Mfano uliopo hapa chini unaonesha migogoro ya maji, ingawa matukio mengine yanaweza kuoneshwa pia na uhusiano wake na usimamizi wa maliasili kuelezwa.

- Matukio haya yalichangiwaje na maliasili na yalichangiaje usimamiaji wa maliasili?
- Hatua zilizochukuliwa na jamii kutatua matatizo hayo zilisaidia kwa kiasi gani?
- Je, inawezekana zikawepo na hatua nzuri zaidi za kumaliza tatizo au kuna njia nyingine tofauti?

### Baadhi ya matukio kwa nyakati fulani kijijini

| | 1960 | 1964 | 1969 | 1967 |
|---|---|---|---|---|
| TUKIO | Ukame | Migogoro kati ya Wamasai na Wabarbaig | Ukame | Ukame |
| MATOKEO YA TUKIO | Upungufu wa chakula na vifo vingi vya mifugo | Watu tisa walikufa wakati wa mapigano ya kikabila wakigombea maji katika kijiji cha Emboreet | Upungufu wa maji | Upungufu wa chakula, vifo vingi vya mifugo na ardhi kuvamiwa |
| UFUMBUZI | Yalipandwa mahindi yanayokomaa kwa muda mfupi<br>Mifugo iliuzwa kwa wingi | Wabarbeig walifukuzwa kijijini | Visima vitatu vilichimbwa | Visima vya maji vilichimbwa |

kumudu maisha yao, miundombinu, upatikanaji wa maji, miti na maliasili nyinginezo, wanyamapori...

Yawezekana wazee wangependa ionekane kama ile miaka mizuri ya nyuma. Inawezekana vijana waliosoma wanaweza kupenda kitu kipya kabisa.

Ndoto zote ni sahihi: Wape moyo kila mmoja kushiriki kwenye kuzipambanua. Si zote zitakazowezekana kuwepo lakini kuzifahamu kutakuwa ni habari muhimu katika kupanga.

Hata hivyo, jadili tu jinsi mambo yanavyoweza kuwa iwapo ndoto hizo zitakuwa kweli.

### Fikiria fursa zilizopo. Mara nyingi jamii zina fursa nyingi kuliko zinavyofikiri.

Sasa ni wakati wa kuangalia fursa ulizonazo ili kuboresha njia mbalimbali za kuleta kipato zinazotegemewa na jamii kumudu maisha, katika namna inayoruhusu ardhi kuwa endelevu.



Wanawake wa kimasai wakichora ramani pamoja na muwezeshaji

- Kama jamii inathamini mifugo, waweza kupenda kuangalia kwa undani mbegu zilizoboreshwa na vijishamba vya malisho, namma ya kunenepesha mifugo na kuiuza kwa bei ya juu. Ufugaji wa namna hii unahitaji ardhi ndogo kuliko ufugaji wa kienyeji, hivyo yaweza kusaidia kupunguza mahitaji ya ardhi.
- Uhakika wa chakula ni suala muhimu? Basi waweza kuangalia suala la kilimo mseto - miti na mazao - aina ya kilimo ambayo inafaa hata kwenye maeneo makame. Kwa kuchagua aina za miti kwa uangalifu, waweza kuotesha mboga za majani na miti kwa ajili ya chakula (kama matunda), kuni, ujenzi, na hata malisho, kwenye ardhi hiyo hiyo.
- Usalama wa maji ni tatizo? Inaweza ikabidi kuangalia uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa madogo yatakayokusanya maji mvua ikinyesha.
- Mna wanyamapori wengi? Iwapo ndivyo, basi biashara inayohusu utalii wa mazingira inaweza kuwa njia muafaka.
- Je zipo fursa nyingine ambazo jamii ingependa kuzifanyia kazi ?
- Vipaumbele viwekwe katika fursa zipi?
- Vikwazo gani vinapaswa kutafutiwa ufumbuzi ili vipaumbele tulivyopanga vifanikiwe ?

Kwa mfano, kuboresha ufugaji, yawezekana kuhitaji madume bora. Yawezekana kuhitaji utaalam kutoka nje ya jamii katika kuanzisha vijishamba vya malisho.

Kuboresha kilimo, unaweza kuhitaji mbegu bora, msaada katika kujifunza namna ya kutunza udongo, mfumo wa umwagiliaji maji mashambani ...

*"Katika kijiji fulani tunaweza kuhitaji haya yote - eneo la utalii, sehemu za malisho ya kiangazi na zile za malisho ya dharura, kilimo. Hata hivyo, kwa kawaida, kilimo hupangiwa ardhi iliyo nzuri, na ufugaji kupewa ardhi isiyo na rutuba, ambako hakuna unyevu mwingi, majani ni kidogo, na magonjwa ni mengi. Jambo moja kubwa ni kwamba, watu wanahitaji taarifa nzuri kuhusu kilimo. Kwa nini kutumia eka 100 kwa shamba ambalo huwezi kulihudumia ipasavyo? Kwa nini usitumie tano tu ukazishughulikia vizuri? Maafisa ugani wanaweza kusaidia sana katika suala kama hili".*

*Moses Neselle*
*Daktari wa Mifugo na Ofisa Mipango Jamii*

## HATUA YA TATU: KUSHUGHULIKIA VIPAUMBELE[3]

### Tengeneza Mpango wa Jamii wa Utekelezaji (CAP)

Ni masuala yapi makubwa ya maliasili yanahitaji kipaumbele katika kuangaliwa?

Malisho yaliyoharibiwa? Migogoro ya wanyamapori? Upungufu wa maji? Migogoro ya mipaka?

Unapoendelea kuhamasisha kwa ajili ya mpango wa matumizi ya ardhi wa muda mrefu, kuangalia kwa haraka baadhi ya vipaumbele vya kijiji kunaweza kuleta maboresho yanayotakiwa na kuipa jamii imani na msukumo katika mchakato mzima wa kupanga (Tazama Jedwali namba 3).

Masuala yako ya kipaumbele yanaweza kuwa ni pamoja na shughuli za kuingiza kipato; kuboresha afya ya mifugo; kupunguza tofauti katika muda unaotumika na makundi mbali mbali au ardhi au rasilimali nyingine; kuboresha huduma za shule; kupunguza migogoro ... jamii nyingi zinaona umuhimu wa haraka wa kupanda miti kusaidia katika kuhifadhi unyevu ardhini, kuzuia mmomonyoko wa udongo, na kuhifadhi vyanzo vya maji. Wengine wanapenda kuboresha nyika za malisho kwa kupanda majani bora kwa malisho au miti

[3] Mpango kazi wa Jamii umeelezewa kwenye hatua 2 ya NLUPC

**JEDWALI NAMBA 3: JINSI KIJIJI KIMOJA KILIVYOPANGILIA VIPAUMBELE VITAKAVYOINGIA KATIKA MPANGO WA JAMII WA UTEKELEZAJI**

| Lengo mahsusi | Nafasi |
|---|---|
| Ongeza eneo linalolimwa kwa kaya kutoka eka 1 hadi eka 4 | 1 |
| Ongeza uzalishaji wa maziwa kutoka ½ lita hadi lita 6 kwa ng'ombe mmoja | 2 |
| Ongeza uzalishaji wa mahindi kutoka magunia 6 kwa eka hadi magunia 10 | 3 |
| Ongeza uzalishaji wa maharagwe kutoka magunia 3 kwa eka hadi magunia 6 | 4 |
| Ongeza uzito wa mnyama ambaye hajachinjwa kutoka kilo 125 hadi kilo 200 | 5 |
| Ongeza milo anayokula mtu kwa siku kutoka miwili ya sasa hadi mitatu | 6 |
| Ongeza uzalishaji wa asali kutoka mizinga 243 hadi 400 | 7 |

inayorutubisha ardhi kwa kuongeza naitrojeni kwenye udongo.

Hapa ni baadhi ya hatua za kufuata katika kuandaa Mpango wa Jamii wa Utekelezaji kuhusu changamoto zinazopashwa kushughulikiwa haraka.

- Orodhesha maeneo ya kushughulikia.
- Yaorodheshe kwa vipaumbele.
- Andaa mpango wa kazi kwa shughuli zilizopendekezwa.
- Amua ni nani anafanya nini.
- Kubaliana muda wa utekelezaji.
- Onesha maeneo ambayo jamii inaweza kuhitaji msaada kutoka nje.

Kwa mfano, huko Loiborsiret, migogoro ya mipaka na kijiji jirani na pia hifadhi ya wanyamapori ilihitaji kusuluhishwa kabla mchakato wa mpango wa matumizi ya ardhi kuendelea. Timu ya majadiliano kuhusu mpaka iliundwa na ikaweza kusuluhisha mgogoro huo baada ya mikutano kadhaa ya majadiliano.

Mgogoro na hifadhi ya wanyamapori ulihitaji usuluhishi na msuluhishaji kutoka nje. Ila palikuwa na faraja kubwa: kijiji kilipata tena ardhi iliyokuwa ikigombewa na ramani kuchorwa upya zikionesha mipaka sawasawa (tazama sura ya 5 inayohusu Usimamizi wa migogoro).

Loibosiret kulikuwapo na tatizo la ukosefu wa usawa wa kijinsia, hali ambayo ilikuwa ikiingiliana na usimamiaji wa maliasili na masuala mengine ya kimaisha katika kijiji: wanawake walikuwa wakifanya kazi kwa saa 16 kwa siku na hawakuwa na muda wa kujishughulisha na shughuli mpya. Jedwali Namba 1 (Kiambatanisho 3) linaonesha kwa ufupi jinsi kijiji kilivyopanga kushughulikia usawa wa kijinsia pamoja na baadhi ya mambo mengine.

## HATUA YA NNE: KUPATA HABARI ZAIDI NA KUKAMILISHA MPANGO[4]

### Pata msaada wa wataalamu

Wakati unatekeleza mambo ambayo jamii imeyapa kipaumbele kwenye Mpango wa Jamii wa Utekelezaji, upangaji wa muda mrefu unaendelea. Na utahitajika msaada wa wataalamu kutoka nje.

- Itabidi kijiji kiainishe mipaka yake. Hata hivyo, utajuaje kwa uhakika mahala pa kuweka mawe ya mipaka?
- Watu wanaweza kuwa wanahitaji miti mingi kwa ajili ya kuni, ujenzi, malisho, kivuli.... Ni aina gani za miti inayofaa zaidi kuipanda mahali inapotakiwa?
- Yawezekana kuna anayetaka kuanzisha shamba la maua, ambalo atafanyia umwagiliaji. Hili litaleta athari gani kwenye upatikanaji wa maji kijijini, kwa mtazamo wa kiasi na uwezekano wa uharibifu?

Huu ndio wakati ambao msaada wa watalamu kutoka nje unapotakiwa. Mashirika yasiyo ya kiserikali, serikali, au wataalamu washauri watafanya utafiti wa kisayansi kuongezea taarifa zilizopatikana kwenye michoro na ramani vilivyoandaliwa na jamii.

Kwa mfano, wapima watahakikisha kuwa mawe ya kuonesha mipaka yako panapotakiwa. Wataalamu wa udongo na wanasayansi wengine watachambua aina za udongo na kubaini mwenendo wa mvua na hali ya hewa kuona kama kilimo kitakuwa chaguo zuri. Wataalamu wa wanyamapori wanaweza kuisaidia jamii kuhesabu idadi ya wanyamapori waliopo na mienendo yao, ili kusaidia katika kupunguza migogoro baina ya watu na wanyamapori sasa na hapo baadaye. Wanasayansi za jamii wanaweza kufanya tafiti na pia kuwahoji watu kwenye kaya na jamii. Wachoraji ramani wataandaa ramani inayotambulika kisheria ikionesha mipaka, umbile la nchi, maliasili na matumizi ya sasa ya ardhi.

*"Tunachojaribu kufanya ni kuongeza uzalishaji kwenye ardhi iliyopo iwe mara mbili au tatu. Kwa namna hii tunaweza kupunguza ardhi iliyolimwa lakini tukaongeza mavuno. Huko Emboreet tumekuwa tukitumia njia sahihi: mbegu zinazofaa, zinazostahimili ukame, kupanda*

[4] Awamu hii inahusiana na hatua ya 4 kwenye NLUPC - Mpango na usimamizi shirikishi wa matumizi ya ardhi

*mapema kabla ya mvua hazijaanza kunyesha. Ofisi ya kijiji inauza mbegu bora za mahindi, mbaazi na choroko kwa bei nafuu. Mwanzoni, hakuna aliyekuwa anakimbilia kununua mbegu, ila sasa, katika mwaka wa tatu, watu wanazikimbilia. Zinavumilia na mavuno yake ni mazuri kutegemea kiasi cha ardhi uliyonayo. Vile vile hili limewezesha kubakiza ardhi kwa malisho na matumizi mengineyo."*

*Moses Neselle*
*Daktari wa Mifugo na Ofisa Mipango Jamii*

## Tengeneza mpango halisi wa matumizi ya ardhi

Kwa sasa, kila mmoja atakuwa amekwishafahamu mengi kuhusu ardhi, fursa na vikwazo na vipaumbele vya jamii. Uko tayari kutengeneza mpango wa matumizi ya ardhi.

Mpango utakuwa na ramani inayoonesha sehemu za matumizi kama:


- Machunga wakati wa msimu wa mvua
- Vijishamba vya malisho au miundombinu mingine kwa ajili ya mifugo
- Machunga wakati wa msimu wa kiangazi
- Machunga ambayo vile vile yanatumiwa na wanyamapori
- Kilimo
- Makazi mapya
- Kuokota kuni
- Kupanda miti
- Maendeleo ya kitaasisi
- Msitu wa jamii au Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Mpango utaelezea pia jinsi jamii ilivyokubaliana kusimamia ardhi; kuendeleza malisho na maeneo ya kilimo. Kwa mfano, kuzuia mmomonyoko, kupunguza migogoro kati ya binadamu na wanyamapori, kuendeleza vyanzo vya maji ..... Yaweza pia kuonesha aina za biashara ambazo jamii inataka ziwepo.

*KUPANGA NI KAZI NGUMU LAKINI YENYE KUWEZESHA*

***Kujadiliana kuhusu miaka iliyopita, miaka ya sasa na ijayo, kunawezesha. Kama watu wanakubaliana juu ya upande mmoja au mbili wapendako kuelekea, ni vizuri. Wanajisikia vizuri.***

*David Nkedianye*
*Mwanasosholojia wa nyika za malisho na jamii*
*Kenya*




*Ramani ya mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji cha Loiborsiret, mwaka 2004*

## HATUA YA TANO: MASUALA YA KISHERIA[5]

### Sajili mpango

Mpango wa matumizi ya ardhi ni wa kisheria, unaowabana watumiaji. PLUM itahakikisha kuwa mpango huo umo katika namna inayokubalika kiserikali na unasajiliwa kwenye mamlaka husika.

### Kubaliana juu ya sheria ndogo mlizojiwekea

Sheria ndogo ni chombo muhimu cha usimamizi shirikishi wa matumizi ya ardhi. Zinatoa nafasi ya kisheria ya kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano kuhusu matumizi ya ardhi. Baada ya jamii kukubaliana, zinabidi zipitishwe na ofisi za serikali kuhakikisha kuwa hazipingani na mahitaji ya vijiji vingine.

Sheria ndogo zinachanganua, kwa mfano, mifugo inapoweza kuchungwa kwa wakati gani na pia watu wanapoweza kujenga makazi yao au kulima mashamba (kama ilivyokubalika kwenye mpango wa matumizi ya ardhi). Kwa sababu sheria ndogo ndizo zinabana kisheria, pia zinabainisha faini zitakazolipwa sheria hizi zikivunjwa.

### Pata hati za umiliki wa ardhi

Moja kati ya faida za mchakato katika kupanga ni kwamba inawasaidia mtu mmoja mmoja, familia na hata kundi la watu kupata hati ya haki ya kumiliki ardhi kimila. Halmashauri za vijiji zinatoa hati hizi kwa kusaidiana na timu ya PLUM.

[5] Kuandikisha na sheria ndogo zimejadiliwa katika Hatua ya 4 na ya 6 kwenye TNLUPC.

# Hatua kuelekea mafanikio



Huko Loibosiret, shirika moja lisilo la kiserikali lilisaidia katika kuweka mipaka kwenye ardhi ya wanakijiji, ikianzia maeneo 15 yanayomilikiwa na wajane, yaliyokuwa kipaumbele kwa kijiji.

### Anzisha Ofisi ya kijiji ya kumbukumbu

Kila mtu anapasha kuwa na nafasi ya kuona ramani, mipango na hati miliki. Kwa hiyo kamati za kupanga na kusimamia, na pia mamlaka za vijiji, zinapaswa kuwa na Ofisi ya kijiji ya kumbukumbu.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji atakuwa msimamizi wa:

- utunzaji kumbukumbu za mabadiliko yote yanayohusu umiliki wa ardhi na matumizi yake;
- kutoa taarifa za mabadiliko kwenye Halmashauri ya Wilaya; na
- kutoa taarifa juu ya matumizi ya ardhi na umiliki kama itatokea migogoro.

Huko Naitolya, mradi uliokuwa unafadhiliwa na GEF, uliojulikana kama "Mifumo mipya ya kujumuisha mifugo na wanyamapori kwenye maeneo ya malisho yaliyopo pembezoni mwa hifadhi za taifa katika Afrika - Tanzania", ulisaidia uanzishaji wa ofisi ya kijiji ya kumbukumbu za ardhi kwa kukipatia kijiji samani na mahitaji ya ofisi hiyo.

## HATUA YA SITA: ANZA KUTEKELEZA MPANGO… NA ENDELEZA ARI[6]

Timu za PLUM na VLUM zitafanya kazi na maofisa ugani na mamlaka nyinginezo na wataalamu kuandaa rasimu ya utekelezaji wa vipaumbele vya mpango wa matumizi ya ardhi.

Baada ya hapo shughuli za PLUM zitakuwa zinaelekea kuisha na hivyo VLUM kufikia mwisho wake pia. Hata hivyo, PLUM itasaidia kwanza kuandaa jinsi ya masuala iliyoyaanza yatakavyoendelelezwa. Hili laweza kuhitaji tathmini zaidi na undani wa ufumbuzi wa matatizo ambayo yatakuwa hayajatatuliwa. Jedwali namba 2 (Kiambatanisho 3) linatoa mfano.

### Ajili na kuwafundisha mafundi waliopo kijijini

PLUM itasaidia pia katika kuajili na kusimamia mafunzo-kazini ya mafundi waliopo kijijini. Mafunzo yaweza kuwa juu ya sheria na haki za ardhi, masuala ya mazingira, na usimamiaji wa migogoro juu ya raslimali.

Kuanzia hapo, mafundi hao watakuwa ndio wataalamu kwenye jamii, ambao watakisadia kijiji kuendelea na kupanua shughuli mbalimbali juu ya usimamizi wa matumizi ya ardhi. Kwa kushirikiana na wanakijiji wengine, mafundi waliopo kijijini wataanza kuutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi.

### Fanyia tathmini mambo yaliyofanikiwa na mahitaji yaliyobaki

Baadhi ya shughuli za mwisho za timu ya PLUM itakuwa ni mikutano ya kijiji ya:

- kuangalia ni mafanikio yapi yamefikiwa kwenye usimamiaji wa matumizi ya ardhi: matumizi ya maliasili yameboreshwaje na pia uzalishaji? Kuna chochote ambacho hakikwenda sawasawa? Ni mambo gani yamefanyika vizuri?
- kuangalia uwezo wa wanakijiji na taasisi zilizopo kuweza kuendelea na shughuli hii.
- kukubaliana nani atahusika na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya masuala ya usimamizi wa matumizi ya ardhi.
- kuandaa mpango wa kujenga uwezo kulingana na mahitaji.
- Ikibidi iunganishe jamii na wataalamu walio nje.

Kwa mfano, wadau wa maendeleo huko Simanjiro waliunda Mtandao wa Ardhi wa Wilaya ya Simanjiro kuwasaidia wadau kubadilishana mawazo, kusimamia mfumo wa ekolijia inayopatikana katika vijiji zaidi ya kimoja, na kutetea matumizi ya sera za ardhi zilizo nzuri.

Moja ya mambo ambayo mtandao wa ardhi ulishughulikia ni migogoro ya binadamu na wanyamapori. Taarifa iliyopatikana kutoka AWF, katika kipindi cha 2004 mpaka 2008, wananchi wilayani waliwaua simba 148 kufuatia simba kuua mifugo. Mtandao wa ardhi unajaribu kuzisaidia jamii nyingine kuanzisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori ili jamii hizo ziweze kupata mapato kutokana na wanyamapori waliopo kwenye ardhi zao kuliko kubakia kupata hasara zisababishwazo na wanyamapori hao (Tazama Kisanduku namba 1).

### Shughuli ziendelee

Timu ya PLUM iondokapo, juhudi za jamii za kusimamia matumizi ya ardhi zitaongozwa na timu ya kijiji ya kusimamia matumizi ya ardhi (VLUM) na mafundi wa kijiji, kwa kushirikiana na jamii na viongozi.

Mikutano ya mara kwa mara itawasaidia wanajamii wote kupitia tena mipango, kufahamu maboresho, kuangalia changamoto mpya na kukumbuka mambo chanya waliyojifunza tangu mwanzo wa mchakato wa kupanga matumizi ya ardhi.

**Jamii imefanya kazi kubwa kufikia hatua hii. Hakikisha kutilia mkazo – na kufurahia – mafanikio yaliyopatikana!**

[6] Hatua hii inashabihiana na hatua za 5 - Utekelezaji na 6 - Majumuisho kwenye TNLUPC

KISANDUKU NAMBA 1: **KULINDA MASHAMBA: MIGOGORO BAINA YA WATU NA WANYAMAPORI KWENYE ENEO LA MRADI**

Ili kuelewa vizuri masuala ya migogoro iliyopo kati ya binadamu na wanyamapori, mradi ulifuatilia migogoro ya namna hiyo katika vijiji vitatu vya Lolkisare, Naitolia na Loibosiret A mwaka 2006.

Mwaka huo, asilimia 25 ya mashamba yote yaliyokuwa yamelimwa na kuhusishwa kwenye utafiti huo yaliharibiwa na wanyamapori. Uharibifu ulikuwa mkubwa kwenye mashamba madogo ambayo kaya zinayalima kwa ajili ya kujipatia chakula kuliko mashamba makubwa. Wanyamapori walioharibu mashamba mara kwa mara ni tembo, pundamilia na nguruwe mwitu. Uharibifu mkubwa ulisababishwa na zaidi ya aina 3-4 za wanyama hao kwa kila tukio.

Kwa nyakati nyingine, tembo walishambulia maghala ya chakula, mifumo ya maji na kusababisha mauaji ya watu.

Njia za kuzuia uharibifu ambazo si za kutisha kama kuweka uzio wa mimea, nyaya za umeme na zile zilizotengenezwa kienyeji hazikufaa sana kulinganisha na zile za kutishia, hasa kwa wanyama wakubwa. Ukweli ni kwamba uzio ni kama kazi bure kwa wanyama wakubwa, hasa tembo.

Utafiti ulibaini kuwa mlinzi akitumia njia za kutishia kama vile moto, kelele, moshi, n.k. - anafanikiwa zaidi kulinda mashamba.

*Chanzo:* Pittiglio, 2009



# Hatua kuelekea mafanikio

# Mambo muhimu ya kukumbuka

1 Kufanya mpango wa matumizi ya ardhi ngazi ya jamii kunaweza:

- kusuluhisha na kuzuia migogoro;
- kutilia mkazo na kuangalia uwezekano wa kushughulikia suala la kutokuwepo usawa kwenye mgawanyo wa ardhi kijinsia na kati ya makundi mbali mbali yanayotegemea njia mbalimbali kwa kipato na chakula;
- kusaidia jamii ifikirie njia mpya au zilizoboreshwa za kutegemea kama njia za kuleta kipato ili kumudu maisha;
- kupanga shughuli zilizochaguliwa kwenye maeneo ambapo zinafaa zaidi kuwepo, na
- kuwezesha jamii kukaa pamoja kufikiria hali yao ya baadaye kwa pamoja.

2 Mpango wa matumizi ya ardhi unafanya kazi vizuri unapofanyika kwa ushirikishi wa hali ya juu - ukihusisha kwa ukamilifu sekta zote kwenye jamii katika kutazama mienendo, kuwazia hali ya baadaye, kuainisha masuala muhimu, na kufanya maamuzi. Mazoezi kadhaa ya ushirikishwaji yanaweza kuwa ya muhimu katika juhudi hizi: kuanzia kwenye kuchora ramani na kukumbuka; kuota na kuwazia siku za usoni; hadi kwenye makongamano na ziara za mafunzo.

3 Kuomba ushauri kwa watu na kuwahusisha kila mara kunaweza kusaidia kukwepa kufikia maamuzi yasiyo sawa kama kupanga mifugo kuwa kwenye ardhi isiyofaa na ile yenye magonjwa (tazama Sura ya 6).

4 Mpango wa jamii wa utekelezaji waweza kuchochea ushughulikiaji wa haraka wa mambo yaliyopewa kipaumbele kama kuzalisha kipato na uharibifu wa ardhi, wakati jamii na wataalamu wanaendelea kushughulika na masuala ya muda mrefu.

5 Mpango wa matumizi ya ardhi unawawezesha watu kufikiria njia mpya za kujipatia kipato na kutafuta msaada kutoka nje unapohitajika (Sura ya 3).

Sura ya 2

# Mambo muhimu ya kukumbuka

## KIAMBATANISHO 1
## AKRONIMI

| | |
|---|---|
| **AA** | Authorized Association |
| **CAP** | Community Action Plan |
| **COB** | Community Based Organization |
| **CBLUP** | Community Based Land Use Planning |
| **DC** | District Councils |
| **DLAC** | District Land Advisory Committee |
| **GMP** | General Management Plan |
| **JAP** | Joint Action Plan |
| **NLUPC** | National Land Use Planning Commission |
| **O&OD** | Opportunities and Obstacles to Development |
| **PLUM** | Participatory Land - Use Management |
| **PORI** | Partnership Options for Resource Use Innovations |
| **PRA** | Participatory Rural Appraisal/Participatory Resource Assessment |
| **RMZP** | Resource Management Zoning Plan |
| **SWOT** | Strength, Weaknesses, Opportunities and Threats |
| **URT** | United Republic of Tanzania |
| **VA** | Village Assembly |
| **VAC** | Village Adjudication Committee |
| **VLUM** | Village Land Use Management Committee |
| **VLUP** | Village Land Use Plans |
| **VEO** | Village Executive Officer |
| **VCs** | Village Councils |
| **VTs** | Village Technicians |
| **WDC** | Ward Development Committee |

## KIAMBATANISHO 2
## MAELEZO YA MANENO

**Jiwe la mpaka.** Alama kwenye udongo ikionesha mahala ambapo watu mbalimbali wanapafahamu na wanapatambua kama mpaka kati ya sehemu mbili au vijiji viwili. Wapima hutumia mawe ya zege au pini za chuma kuonesha mipaka (NLUPC, 1998).

**Sheria ndogo.** Sheria ndogo za ngazi ya kijiji zinaweza kutungwa na halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli zake kwa mamlaka yaliyotolewa na sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 1982 (sehemu za 164-176) (NLUPC, 1998).

**Hati ya Kimila ya Haki ya Miliki ya Ardhi.** Ni hati inayoainisha haki ya kumiliki ardhi itolewayo kwa mmiliki na watumiaji wa ardhi hiyo kulingana na taratibu za kimila kuhusu ardhi. Sheria ya Ardhi ya Kijiji (1999) inatoa mamlaka haya kwa Halmashauri ya Kijiji na Mkutano wa Kijiji kwenye vijiji vilivyoandikishwa (NLUPC, 1998).

**Mpango wa Jamii wa Utekelezaji (CAP).** Unaonesha mtiririko wa shughuli na matumizi ya rasilimali kama zilivyopangwa na jamii inayotaka kufikia malengo fulani. Kwa ujumla, mpango wa utekelezaji unajumuisha malengo, mikakati, na shughuli za kufanya ili kufikia malengo. Unaainisha pia vitu vinavyotakiwa kwenye utekelezaji, unaonesha vile vile nani atatoa vitu hivyo vinavyotakiwa, kipindi cha muda ambamo malengo yatafikiwa, vigezo vya kupima mafanikio wakati wa kufuatilia utekelezaji (NLUPC, 1998).

**Kamati ya pamoja ya mipango.** Ni taasisi inayoundwa na wajumbe kutoka vijiji ambavyo vina nia kufanya makubaliano ya matumizi ya pamoja ya ardhi. Hii yaweza kuwa ardhi yote kwenye vijiji vinavyohusika au eneo lenye mambo ambayo vijiji vyote husika vina nia inayofanana juu ya mambo hayo na hivyo kuwa na kamati ya pamoja (NLUPC, 1998).

**Makubaliano ya matumizi ya pamoja ya ardhi.** Katika hali ambayo rasilimali ardhi iliyopo, kama eneo la malisho, misitu, vyanzo vya maji, na kadhalika, ipo kwenye mipaka ya maeneo muhimu kwa vijiji zaidi ya kimoja, vijiji husika vinaweza kuamua kuungana na kuandaa mpango wa kusimamia kwa pamoja rasilimali hiyo. Makubaliano kama hayo yanajulikana kama makubaliano ya matumizi ya pamoja ya ardhi (NLUPC, 1998).

**Kusajili ardhi.** Inamaanisha kuingiza kwenye rejista, kumbukumbu ya haki walizonazo watu binafsi, vikundi vya watu, makampuni, na kadhalika. Mara nyingi sababu ya kusajili ardhi kwenye vijiji ni kuongeza usalama na kupunguza migogoro juu ya mipaka ya vijiji (NLUPC, 1998).

**Wadau.** Ni watu binafsi na makundi ya watu wenye nia (wenye dau) katika suala fulani, yaani, mchakato wa maendeleo. Katika mtazamo wa PLUM, wadau ni pamoja na wote wale wenye nia kwenye rasilimali ardhi iliyomo kijijini kufuatana na mipaka yake (NLUPC, 1998).

**Kijiji.** Kijiji ni kile kilichoandikishwa kwenye sheria ya Serikali za Mitaa, namba 7 ya mwaka 1982 (NLUPC, 1998).

**Mkutano Mkuu wa kijiji.** Unajumuisha watu wote ambao ni wakazi wa kijiji kinachohusika na ambao wana miaka 18 au zaidi. Mwenyekiti wa kijiji ndiye mwenyekiti wa mkutano mkuu na Mtendaji wa Kijiji ndiye Katibu wa mkutano mkuu wa kijiji. Mkutano mkuu wa kijiji ndio wenye mamlaka ya juu ya masuala yote ya kutunga sera kwenye kijiji na inahusika na uchaguzi wa Halmashauri ya Kijiji (NLUPC, 1998).

**Halmashauri ya kijiji.** Hiki ni chombo cha serikali ya kijiji ambacho kimepewa mamlaka yote ya utendaji kuhusu masuala yote ya kijiji. Inaundwa na wajumbe waliochaguliwa miongoni mwa wajumbe wa mkutano wa kijiji waliochaguliwa katika mkutano wa kijiji. Ina wajumbe 25 wanaounda kamati tatu za kudumu: fedha na mipango; usalama; na huduma za jamii na uchumi, na pia idadi fulani ya kamati ndogo (NLUPC, 1998).

**Ardhi ya kijiji.** Ni ardhi yote iliyomo ndani ya mipaka ya kijiji kilichosajiliwa, ambapo Halmashauri ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji vimepewa mamlaka ya kusimamia (WWG, 2004). Ardhi ya kijiji inamaanisha ardhi ambayo imekubalika kuwa ardhi ya kijiji chini ya na kulingana na kipengele 7 cha sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na inajumuisha ardhi yote iliyohamishiwa kwenye kijiji.

**Mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi.** Huu ni mpango wote wa kijiji unaoonesha jinsi rasilimali za kijiji zitakavyotumika ili kufikia malengo yaliyokubalika. Kwenye PLUM, mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji unaandaliwa kwa kuwashirikisha wadau wote na taasisi zao, ili mpango huo uoneshe nia za wahusika wote na uwezo wao kiuwiano. Mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi unachangia katika juhudi za kuleta maendeleo kwenye matumizi ya maliasili, kama kilimo, ufugaji, makazi, maji, misitu, wanyamapori, na maendeleo ya jamii (NLUPC, 1998).

## KIAMBATANISHO 3
## TAARIFA MUHIMU

JEDWALI NAMBA 1: **SEHEMU YA MAPENDEKEZO YA MPANGO KAZI WA JAMII WA KIJIJI CHA LOIBORSIRET (CAP)**

| Malengo mahsusi | Fursa | Vikwazo | Shughuli mahsusi | Rasilimali zinazotakiwa | Gharama Elekezi (TZS) | Viashiria |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1. Kupunguza saa ambazo wanawake wanafanya kazi kwa siku kutoka 16 hadi 8 ifikapo mwaka 2008.** | • Maksai<br>• Majiko sanifu/ bora | • Matumizi mabaya ya maksai<br>• Kutokuwepo majiko mapya | • Kuandaa mipango<br>• Kutoa mafunzo juu ya majiko rahisi yenye gharama nafuu<br>• Jamii kutumia teknolojia rahisi | • Karatasi, peni nk<br>• Mfundishaji<br>• Vifaa vya kufundishia<br>• Posho<br>• Usafiri | 36,000 | Idadi ya saa |
| **2. Kuongeza idadi ya rasilimali wanazomiliki wanawake kutoka 2 hadi 5 ifikapo mwaka 2008.** | • Sera ya wanawake | • Sera ya wanawake haitumiki kama ilivyotarajiwa | • Mikutano ya kijiji juu ya matumizi ya sera hiyo<br>• Mafunzo kwa vikundi na Serikali ya Kijiji kuhusu sera hiyo<br>• Kuitekeleza sera | • Karatasi, peni nk<br>• Mfundishaji<br>• Vifaa vya kufundishia<br>• Posho<br>• Usafiri<br>• Sera | 36,000 | Idadi ya rasilimali wanazomiliki |
| **3. Kushughulikia migogoro ya ardhi kijijini** | • Mipango ya matumizi ya ardhi vijijini<br>• Miundo ya VLCs kwa migogoro ya ardhi<br>• Wataalamu wa ardhi wa wilaya<br>• Kuwepo kwa timu za PLUM na VLUM | • Sheria ndogo za vijiji bado kukamilishwa na kupitishwa<br>• Migogoro ya ardhi na kijiji cha Narakauwo na Hifadhi ya Wanyamapori ya Tarangire<br>• Migogoro ya ardhi kati ya watu binafsi | • Kukamilisha na kutumia sheria ndogo<br>• Kufundisha VLC na VT juu ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi na haki juu ya ardhi<br>• Kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya VLUPs | • Mipango ya matumizi ya ardhi<br>• Rasilimali watu | | • Kuanza kutumia mipango ya matumizi ya adhi kama makubaliano yalivyo<br>• Idadi ya migogoro ya ardhi<br>• Idadi ya migogoro ya ardhi iliiliyoshughulikiwa |
| **4. Kushughulikia na kuzuia migogoro kati ya watu na wanyamapori** | • Uwepo wa wanyamapori wengi<br>• Sheria na taratibu zilizopo | • Migogoro kati ya watu na wanyamapori (kushambulia, kuambukiza magonjwa, na kushambulia mazao) | • Anzisha maboma ya Wamasaai ya kiasili<br>• Anzisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori | • Rasilimali za wanyamapori<br>• Wafundishaji juu ya uhifadhi | | • Idadi ya CBVs zilizoanzishwa<br>• Kugawana faida zitokanazo na biashara za pamoja zihusianazo na wanyamapori |

## JEDWALI NAMBA 2: MUHTASARI WA HATUA NA SHUGHULI ZA PLUM

| Hatua | Matokeo | Shughuli |
|---|---|---|
| 1. Maandalizi (Ngazi ya Wilaya) | • PLUM imeanzishwa kwenye ngazi ya Wilaya na rasilimali watu wamehamasishwa | • Kuunda timu ya kupanga matumizi ya ardhi |
| | • Mpangokazi na mpango wa utekelezaji imeandaliwa<br>• Taasisi husika zimehamasishwa | • Kuandaa mpango wa utekelezaji na kuhamasisha taasisi zinazohusika |
| | • Kupatikana ufahamu wa kutosha kwa ajili ya zoezi la kupanga | • Kukusanya na kuchambua takwimu |
| | • Mpango mzuri wa kufanyia kazi<br>• Mpango kukubaliwa na taasisi zinazohusika<br>• Fedha, mahitaji mengine na watendaji kupangwa | • Kuandaa mpango wa utekelezaji kazi katika vijiji vilivyopewa kipaumbele |
| 2. PRA kwa ajili ya usimamizi wa matumizi ya ardhi | • Wataalamu ngazi ya wilaya kupangwa (timu ya PRA)<br>• Halmashauri ya kijiji imehamasishwa<br>• Jamii kijijini imehamasishwa<br>• Kamati ya VLUM imeundwa na kutambulishwa majukumu yake | • Kuunda timu ya PRA<br>• Mkutano wa utambulisho wa Halmashauri ya Kijiji<br>• Ziara zaidi za utambulisho<br>• Mkutano mkuu wa kijiji na kuunda kamati ya VLUM<br>• Maelezo mafupi kwa kamati ya VLUM |
| | • Uelewa wa kutosha kuhusu kijiji | • Kukusanya takwimu kijijini<br>• Kupanga vipaumbele vya matatizo na fursa zilizopo |
| | • Mpango mzuri wa utekelezaji ambao unawakilisha mawazo ya wadau<br>• Jamii kuifahamu PLUM na imehamasishwa kuitekeleza | • Kuandaa mpango wa kazi wa jamii kwa ajili ya usimamiaji matumizi ya ardhi ya kijiji |
| 3. Tafiti za ziada | • Taasisi kijijini zimehamasishwa<br>• Wataalamu ngazi ya wilaya wamepangwa | • Kukutana na Halmashauri ya kijiji na kamati ya VLUM<br>• Kujiandaa kwa ajili ya tafiti za ziada |
| | • Hati ya ardhi ya kijiji, inayoipa halmashauri ya kijiji mamlaka ya kisheria kushughulikia masuala ya ardhi na PLUM<br>• Migogoro ya ardhi na vijiji vya jirani imesuluhishwa | • Kuainisha mipaka ya kijiji<br>• Kuweka alama muhimu za mipaka ya kijiji<br>• Kuandaa ramani ya mipaka ya kijiji |
| | • Rasimu ya ramani ya kijiji<br>• Masharti kwa ajili ya usimamizi wa ardhi yametimizwa | • Utafiti juu ya ardhi kwa ajili ya kuandaa rasimu ya ramani ya kijiji |
| | • Ramani ya matumizi ya kijiji iliyopo sasa<br>• Uelewa wa kutosha kwa kuandaa mpango wa kina wa utekelezaji wa matumizi ya ardhi | • Kutathmini matumizi ya sasa ya ardhi<br>• Tafiti za ziada za hali ya kilimo na uchumi<br>• Tafiti za ziada za kilimo-ekolojia |
| 4. Uendeshaji wa Mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi | • Mpango wa kupunguza migogoro ya ardhi, matumizi mazuri zaidi ya rasilimali na hali iliyoboreshwa ya uhakika wa ardhi | • Kutengeneza rasimu ya kina ya mpango wa matumizi ya ardhi |
| | • Migogoro ya ardhi imepunguzwa<br>• Uhakika wa arhi umeongezeka<br>• Maamuzi ya wanawake juu ardhi yameongezeka<br>• Mgawanyo wa ardhi unaoridhisha zaidi | • Kuweka mipaka, kuchora ramani na kurasimisha maeneo ya jumuiya<br>• Kuweka mipaka, kuchora ramani na kurasimisha maeneo ya binafsi |
| | • Mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji, ulioandikwa vizuri, ukijumuisha mawazo ya wadau | • Kukamilisha mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji, mikakati ya kusimamia maliasili na michoro ya ramani ya matumizi ya ardhi iliyokubalika |
| | • Kijiji kina uwezo wa kushughulikia chenyewe masuala yahusuyo ardhi<br>• Makubaliano yahusuyo umiliki wa ardhi na usimamizi wa matumizi ya ardhi yanatekelezwa | • Kuanzisha rejista ya kijiji ya kumbukumbu za ardhi<br>• Kutoa hati za umiliki ardhi wa kimila<br>• Kutunga sheria ndogo |

*(Inaendelea)*

JEDWALI NAMBA 2: **(Inaendelea)**

| Hatua | Matokeo | Shughuli |
|---|---|---|
| 5. Utekelezaji wa hatua sahihi za usimamizi wa ardhi | • Wataalamu wa wilaya na kata wamepangwa<br>• Taasisi za kijiji zimehamasishwa kuhusu hatua hii | • Maafikiano kati ya maofisa ugani wanaohusika na wataalamu wengine yamefikiwa<br>• Kukutana na halmashauri ya kijiji na kamati ya VLUM |
| | • Masuala ya usimamizi wa ardhi yamechambuliwa kwa undani zaidi na fursa kuainishwa | • Usimamiaji wa ardhi wa ziada |
| | • Jamii imehamasishwa<br>• Mpangokazi umetayarishwa ili utumike kuchukua hatua bora zaidi za usimamizi wa ardhi | • Mkutano mkuu wa kijiji<br>• Mikutano katika ngazi za vitongoji |
| 6. Kujumuisha hatua zote kuelekea kutekeleza mpango | • Jamii inapanga, inatekeleza na kufuatilia hatua zilizokubalika<br>• Mafundi wa kijiji wamepangwa na kufundishwa | • Kupanga na kutekeleza mambo yaliyokubalika<br>• Mafundi wa kijiji kuendelea kufanya kazi, lakini wakipatiwa mafunzo ya mara kwa mara |
| | • Uelewa wa kutosha wa taasisi za kijiji na timu ya PLUM kupanga mchakato wa kutekeleza mpango | • Tathmini ya mchakato wa PLUM katika kijiji na uwezo wa jamii na taasisi zake kuendelea kutekeleza mpango |
| | • Majukumu ya wadau kuainishwa vizuri na kukubaliana namna ya kuendeleza PLUM | • Kukubaliana na kurasimisha majukumu ya wadau katika PLUM<br>• Mkutano mkuu wa kijiji |
| | • Mawasiliano mazuri kati ya kijiji na taasisi za wilaya | • Kufuatilia |

## Sheria na sera zinazohusiana na kupanga matumizi ya ardhi nchini Tanzania

Zifuatazo ni baadhi ya sera zinazohusiana na kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi:

### Mwongozo wa usimamizi shirikishi wa matumizi ya ardhi nchini Tanzania (1998)

Mwongozo wa usimamizi wa matumizi ya ardhi, ulioandaliwa na Tume ya Taifa ya Kupanga Matumizi ya Ardhi, unatoa utangulizi na kurasimisha upangaji na usimamizi shirikishi wa matumizi ya ardhi kwenye ngazi ya kijiji. Mwongozo, ulioandaliwa kwenye ngazi zipatazo sita, waweza kurekebishwa kulingana na hali halisi na mahali utakapotumiwa.

### Sera ya Taifa ya Ardhi (1997)

Sera hii inalenga kuhakikisha taratibu thabiti za miliki ya ardhi, kuhamasisha matumizi mazuri ya ardhi, na kuwezesha maendeleo endelevu. Malengo mahsusi ni pamoja na:

- Kuwezesha kuwepo usawa katika kupata na kutumia ardhi kwa wananchi;
- Kuhakikisha kuwa haki juu ya ardhi – hasa haki za kimila za wamiliki wadogowadogo – zinafahamika vizuri na kuzingatiwa kisheria.

### Matamko yaliyomo katika sera ya ardhi yanayozungumzia mipango na utawala

a) Mpango wa matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji. Sera inaeleza kuwa mchakato wa kupanga matumizi ya ardhi ngazi ya kijiji itarahisishwa ili kuharakisha utekelezaji wake. Itakuwa imeegemea kwenye vigezo vifuatavyo:

- Mpango wa matumizi ya ardhi utafanywa kwa njia iliyo shirikishi kwa kuwahusisha wadau. Mchakato wa kupanga utatanguliwa na tafiti ili kubaini utaratibu uliopo wa kumiliki ardhi, mienendo ya matumizi ya ardhi, na uwezo wa ardhi;
- Mipango ya matumizi ya ardhi itaandaliwa na Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri za Vijiji;
- Mpango wa kijiji wa matumizi ya ardhi utatumiwa kama chombo cha utekelezaji wa sera katika kuboresha matumizi na usimamiaji wa ardhi; na

- Mipango ya vijiji ya matumizi ya ardhi itatoa mwongozo kwa shughuli za ugani kwa kilimo, ufugaji, wanyamapori, uvuvi na hifadhi ya mazingira.

b) Maeneo ya matumizi ya ardhi yanayoingiliana. Usimamizi wa wanyamapori waweza kuingiliana tu na ufugaji, na si kilimo au matumizi mengineyo ya ardhi.

c) Muundo wa kitaasisi. Ili kupunguza migogoro na masuala yasiyo sahihi kwenye kusimamia ardhi, sera ya ardhi inatamka kwamba "Waziri wa Ardhi atakuwa ndiye pekee mwenye dhamana juu ya masuala ya ardhi. Ambapo itatakiwa atoe mamlaka kwa mtu mwingine, patakuwa na utaratibu uliowazi kufuata ngazi za uwajibikaji."

### Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji namba 5, zote za 1999.

Kwa pamoja, sheria hizi mbili zinaeleza juu ya kusimamia ardhi, ikiwemo kutatua migogoro ya ardhi.

Kulingana na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999) sehemu ya 8(1): Halmashauri ya kijiji, kulingana na maelezo ya sheria, itakuwa na wajibu wa kusimamia ardhi ya kijiji. Halmashauri ya kijiji itafanya shughuli za kusimamia kulingana na taratibu zitumiwazo na wadhamini kusimamia mali kwa niaba ya wafaidika, iwapo halmashauri ya kijiji ni mdhamini na wanakijiji na watu wote wanaoishi kwenye kijiji hicho wakiwa wafaidika chini ya udhamini wa ardhi ya kijiji. Katika kila mkutano wa kawaida wa kijiji, halmashauri ya kijiji itatoa ripoti na kupokea mapendekezo kuhusu

### JEDWALI NAMBA 3: MWONGOZO JUU YA TAKWIMU ZA KUKUSANYA KWA AJILI YA MPANGO WA KIJIJI WA MATUMIZI YA ARDHI

**Habari za ujumla**
- Mahali
- Mwinuko
- Kufikika (barabara, umbali)
- Miundombinu sahihi
- Mipaka ya utawala

**Hali ya hewa (kwa mwaka, mgawanyo na viwango vinavyozidi hali ya kawaida)**
- Mvua
- Kiwango cha joto
- Kasi ya upepo
- Kiwango cha unyevu unaotoka kwenye mimea na mazingira kwa njia ya kuvukizwa
- Kipindi cha kukua

**Udongo**
- Sura ya nchi (miinuko)
- Mmomonyoko
- Rutuba ya udongo
- Vikwazo kutokana na masuala mengine yanayohusiana na udongo

**Masuala ya maji**
- Mito na vijito
- Mfumo wa maji taka
- Kina cha maji ya ardhini

**Uendelevu wa ardhi**
- Kufaa kwa ardhi katika matumizi mbalimbali: mimea, malisho ya mifugo, misitu, n.k.
- Uwezo wa ardhi
- Kiasi cha mifugo kiwezacho kulishwa kwa ardhi iliyopo

**Matumizi halisi ya ardhi**
- Kilimo: mazao makuu
- Mifugo
- Misitu
- Uoto wa asili
- Matumizi mengine

**Elimu Jamii/huduma za kijamii**
- Masuala ya watu: idadi ya watu kwa kila kijiji na kwa kuangalia umri na jinsia
- Mahitaji ya ardhi
- Kuwepo kwa migogoro mikubwa (hasa ya matumizi ya ardhi)
- Uhamaji ndani na kati ya mikoa
- Mwenendo wa upangaji makazi
- Hali ya majengo ya kuishi
- Hali na aina ya huduma za elimu na afya (shule na zahanati)
- Huduma nyingine za jamii: maduka, maghala, upatikanaji maji, mashine za kusaga nafaka, n.k.
- Kuwepo kwa taasisi, na ufanisi wake: taasisi za kiserikali, za kijamii na kidini, pamoja na zisizo za kiserikali
- Ufanisi wa uongozi wa kijiji

**Sera na sheria zinazohusiana na usimamiaji ardhi**
- Sheria, sera, miongozo, n.k. zinazohusu ardhi, maji, mifugo, misitu, wanyamapori, makazi, utalii, n.k.
- Sheria ndogo za usimamizi wa ardhi

**Miradi inayoendelea kijijini**
- Miradi ya kisekta
- Miradi inayohusisha mambo mengi kwa pamoja

**Matumizi ya sasa ya ardhi na mipango ya maendeleo**
- Wilaya, Tarafa
- Kijiji
- Nchi, kanda, mkoa

**Uchumi**
- Kiwango cha hali ya maisha
- Vyanzo vya kipato
- Mwenendo wa matumizi
- Kilimo na mifugo
- Upatikanaji wa pembejeo za kilimo
- Upatikanaji wa nguvukazi
- Masoko
- Eneo la shamba
- Umiliki wa ardhi na taratibu za umiliki wake

usimamizi na masuala ya utawala wa ardhi ya kijiji. Katika kutumia mamlaka iliyopewa ya usimamizi, halmashauri ya kijiji itakuwa na mamlaka ya kuingia kwenye makubaliano na kijiji kinginecho na kuwa na makubaliano ya matumizi ya pamoja ya ardhi kwa matumizi ya kikundi kimoja au zaidi. Sheria ya Ardhi (1999) Sehemu 11 (1).

### Sera ya Taifa ya Wanyamapori (1998)

Sera ya serikali kuhusu wanyamapori inalenga kuhusisha wadau wengi zaidi katika uhifadhi wa wanyamapori - hasa jamii za vijijini, sekta binafsi, na jamii ya kimataifa. Sera hii inatoa nafasi kwa jamii kuanzisha na kusimamia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kwenye njia za mapito ya wanyamapori, njia wapitazo wakati wa kuhama, na maeneo ya wazi kati ya vijiji na hifadhi. Kuunda Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kunawezesha vijiji kusimamia, kutumia, na kufaidika kutokana na wanyamapori waliopo katika ardhi yao. Jamii zinaweza kanzisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kupitia kwenye mipango ya vijiji vyao ya matumizi ya ardhi.

## KIAMBATANISHO NAMBA 4
## FAHARASA

**Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ.)** 1999. *Land Use Planning: Methods, Strategies and Tools*, GTZ, Eschborn.

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT).** 1998. T*he Wildlife Policy of Tanzania.* Dar es Salaam: Government Printer.

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT).** 2001. *Community-based Forest Management Guidelines.* Dar es Salaam, Forestry and Beekeeping Division.

**Mwelekeo wa NGO (MWENGO).** 2001. *Land Issues in East and Southern Africa: An Overview*, Volume 1: Southern Africa, MWENGO, Harare.

**National Land Use Planning Commission of Tanzania Website,** *planning guidelines:* http://www.nlupc.co.tz/aboutus.php

**United Republic of Tanzania (URT).** 1997. *The National Land Policy, Second edition,* Ministry of Lands, and Human Settlement Development, Dar es Salaam.

**United Republic of Tanzania (URT).** 1998a *Guidelines for Participatory Village Land Use Management in Tanzania,* First Edition, National Land Use Planning Commission, Dar es Salaam.

**United Republic of Tanzania (URT).** 1999a *The Land Act No. 4,* Ministry of Lands, Housing and Human Settlement, Dar es Salaam.

**United Republic of Tanzania (URT).** 1999b *The Village Land Act No. 5,* Ministry of Lands, Housing and Human Settlement, Dar es Salaam.

**United Republic of Tanzania (URT).** 2007 *The Land Use Planning Act,* Ministry of Lands, and Human Settlement Development, Dar es Salaam.

# Wanyamapori waweza kukuinua: kuanzisha shughuli za biashara zihusianazo na uhifadhi

# Utangulizi





Itakuwaje ukiweza kubadilisha tatizo kubwa – hali ambayo inakugharimu fedha, muda na kukuumiza – ukaifanya kuwa biashara ya kushamiri ikakuingizia kipato badala ya kuwa kero?

Iwapo wanyamapori wengi wanarandaranda katika ardhi yenu ya jamii; iwapo ufugaji au kulima chakula ni vigumu au haiwezekani kwa sababu ya wanyamapori; iwapo jamii yenu ipo pembezoni mwa hifadhi ya taifa au kwingineko ambako wageni huja kwa wingi .... basi mwaweza kuwa mmekalia fursa ya kuwa na biashara nzuri sana.

## FURSA ILIYOPO

Kila mwaka mamilioni ya wageni kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni hutembelea maeneo yenye wanyamapori wengi barani Afrika. Kwa watu wengi ni ndoto ya maisha na wako tayari kutumia fedha zao nyingi kwa matembezi kama haya. Wengine hujikuta "wamenogewa" katika suala hilo na hurudi mara kwa mara, wakitaka kwenda kwenye maeneo "mapya", ambayo hayajatembelewa sana.

Zaidi ya watalii 700,000 waliitembelea Tanzania mwaka 2007 na kwa pamoja wakatumia zaidi ya dola za Marekani bilioni moja. Wapo wanaokadiria kuwa ifikapo mwaka 2010 watalii kuja Tanzania watafikia milioni moja na watatumia kiasi cha dola za Marekani bilioni moja na nusu.

Mtandao wa safari za utalii wa kaskazini -unaojumuisha Mlima Kilimanjaro, Ngorongoro, Tarangire na Mbuga ya Wanyamapori ya Manyara na wilaya zinazozunguka maeneo haya – hupata kiwango kikubwa cha watalii wa kimataifa. Hawa ni pamoja na wale wanaokuwa kwenye safari zao za kwanza na watalii wazoefu wanaotaka kufika kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi yenye kambi zilizojificha ili kuona mambo mapya.

Nchi jirani ya Kenya imekuwa ikikuza sekta yake ya utalii kwa muda mrefu zaidi kuliko Tanzania; katika mwaka 2007 ilipata watalii milioni mbili ingawa mwaka 2008 idadi ya watalii ilipungua ghafla kutokana na machafuko yaliyotokea baada ya uchaguzi mkuu. Kulingana na taarifa ya Waziri wa Utalii wa Kenya, utalii umekuwa sekta inayokua kwa kasi kubwa zaidi kwenye uchumi wa nchi hiyo, kwa makadirio ya asilimia 13 kwa mwaka. Inatarajiwa kuwa hali itabadilika na kuwa nzuri. Utalii unachangia karibu asilimia 12 ya pato la taifa kwa kuingiza kiasi cha Shilingi za Kenya bilioni 65.4 (zapata dola za Marekani milioni 840) mwaka 2007.

## JAMII YAWEZA KUFAIDIKA VIPI?

Kwa hakika, baadhi ya kampuni za utalii, serikali, na wajasiriamali wanapata fedha nyingi kutokana na wanyamapori. Lakini, kwa kiasi kikubwa, jamii inayoishi katika maeneo yenye wanyamapori wanakuwa hatarini na kushuhudia uharibifu badala ya kunufaika.

Katika kusaidia kufikia malengo ya maendeleo vijijini, na pia kuhakikisha kuwa wanyamapori wanadumu milele, jamii nyingi na mashirika yanaangalia jinsi ya kuwa na shughuli za biashara zinazohusiana na asili au uhifadhi.

Vyovyote itakavyoitwa, biashara zinazohusiana na uhifadhi hazitaifanya jamii yako kutajirika ila waweza kuisaidia kukua kiuchumi na kutoa rasilimali za kuwekeza kwenye huduma muhimu za jamii.

Kwa kuongezea, miundo mipya inaibuka ya kufidia jamii moja kwa moja kwa ajili ya "huduma za mazingira" – ambazo mara nyingi zinamaanisha kuzingatia utaratibu wa kusimamia ardhi ambao jamii imeutumia tangu miaka mingi iliyopita (Kisanduku namba 1).

## KUWA MBUNIFU

Biashara za jamii zinazohusiana na wageni (CBV) haziishii tu kwenye kambi na nyumba za wageni. Wageni nao wanahitaji vitu vya kuwaburudusha na kuwafurahisha na pia kupata uzoefu wa mambo yenye uhai kama kuendesha ngamia na kwenda kwenye machunga na wafugaji, kujifunza ngoma za kienyeji, kutengeneza shanga, kuishi katika nyumba za wenyeji hata kujitolea kwenye mashule au miradi ya ujenzi.

Sio lazima CBV ziwe na uhusiano wa moja kwa moja na utalii. Uchongaji vinyago, kurina asali, kilimo-misitu, ufugaji wa vipepeo, ufugaji wenye tija zaidi, "utafutaji wa aina fulani za wanyama au mimea" - kuziuzia kampuni haki ya kutafiti mitishamba kwa ajili ya utengenezaji dawa au vipodozi - mradi wowote ambao utategemea maliasili, kuhimiza utunzaji wa maliasili na kuinufaisha jamii, ni mradi sahihi.

Jamii nyingi zina uwezekano wa, na mianya mingi ya CBV. Itasaidia iwapo wana-jamii wako tayari kuwazia kuliko yale ambayo yamekwishajaribiwa - na kupata msaada kuwezesha biashara kutokea.

KISANDUKU NAMBA 1: **MALIPO KWA HUDUMA ZA MAZINGIRA**

Watunza mazingira na watunga sera wanaendelea kufikiri kuwa inabidi jamii za vijijini zilipwe kwa ajili ya "mfumo wao wa ekolojia" au "huduma za mazingira" wanazotoa. Kwa maneno mengine, kama jamii ya kijijini inahifadhi chanzo cha maji na mito, lazima wafaidike.

Kama wanafanya juhudi kutunza msitu badala ya kuuchoma mkaa, lazima wafaidike. Kama wakiushinda ushawishi wa kuuza ardhi kwa ajili ya mifugo kwa wakulima, lazima wafidiwe sawa na kiasi ambacho wangepata kwa kuuza.

Baadhi ya asasi zilizoko Afrika Mashariki hivi sasa zimeanza kuchukua hatua za kuilipa jamii kwa kuishi na mifugo yao na wanyamapori kwa pamoja kama walivyokuwa wanafanya kwa siku zilizopita – bila kujishughulisha na biashara yoyote.

**Malipo kwa kijiji cha Terrat , Tanzania**

Mmoja wa mifano ya malipo kwa huduma za mazingira ni ule wa kijiji cha Terrat, katika wilaya ya Simanjiro, Tanzania – eneo muhimu la wanyamapori karibu na mbuga ya Taifa ya Tarangire. Ikiongozwa na Kampuni ya Utalii ya Dorobo na shirika lisilo la kiserikali liitwalo Ujamaa Community Resource Trust, pamoja na kampuni nyingine za utalii na Mradi wa Tembo wa Tarangire Terrat, mfumo huo unatoa manufaa ya pesa kwa Terrat ili kijiji kiendelee kuhifadhi ardhi ambayo tayari wanaitunza kama mahali ambapo kiasili ni malisho ya kiangazi.

Ushirika huo unailipa Terrat malipo yapatayo Shilingi za Kitanzania milioni tano kwa mwaka. Kwa malipo hayo kijiji kimekubali kuzuia kulima, kuchoma mkaa, na uwindaji haramu wa wanyamapori kwenye eneo hilo. Zaidi ya hapo, kijiji kiliwaomba waendesha utalii kuwalipa mabwana wanyamapori wanne ili kusimamia na kuona kuwa uwindaji haramu hautokei. Mkataba huo, uliotiwa saini Desemba 2005, unasimamiwa na bodi ya usimamizi ya kijiji yenye wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji kufanya kazi kwa miaka mitano.

Shilingi za Kitanzania milioni 15 ambazo kijiji kimekwishazipata mpaka sasa zimewekezwa katika ujenzi wa shule ya msingi na sekondari mpya. Jumla ya mapato si makubwa – yapata dola za Marekani 4,500 – kiasi ambacho jamii inaweza kuzitumia kulingana na vipaumbele vyake.

**Mpango wa hifadhi kwa kukodisha, Kitengela, Kenya**

Kusini mwa Nairobi ipo Hifadhi ya Wanyamapori ya Nairobi ambayo huko nyuma ilikuwa imezungukwa na ardhi ya malisho inayomilikiwa kwa pamoja ambamo wanyamapori walikuwa wakirandaranda wakati wa mvua. Kwa sasa hifadhi hiyo imo kwenye hatari ya kuwa kisiwa cha mfumo wa ekolojia isiyokuwa endelevu – eneo kubwa la wanyamapori wafugwao – kwa sababu ya kugawagawa ardhi kwenye vipande vidogo vidogo vya watu binafsi, kulima na kujengea uzio, kuanzishwa viwanda, kukuzwa kuwa mji, kuwepo uchimbaji madini, na thamani ya ardhi inapanda.

Kwa kutambua kuwa mfumo wa ekolojia na kutegemea ufugaji kwa kuleta kipato na chakula kunapungua, wadau pamoja na serikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na taasisi za binafsi walianzisha Mpango wa Hifadhi ya Kukodisha. Hasa hasa, mpango huu wa kukodisha unahusu kuikodisha ardhi kutoka kwa kaya za wamasai kwa ajili ya kuhifadhi – wakiwalipa dola la za Marekani 4 kwa eka moja kwa mwaka kwa kukubaliana kuwa hawatawekea uzio, hawatalima wala kuuza ardhi hiyo.

Kwa kuanzia na eka zipatazo 100 mwaka 2000, mpango huu sasa una eka zipatazo 11,500 na kuchangia kaya zipatazo 100 kwenye kumudu maisha yao.

Mpango unaziwezesha kaya kupata fedha na hapo hapo kubaki na mifugo yao.

Mpango huu vile vile unawalinda wahusika kutoingia kwenye migogoro. Katika kiangazi cha mwaka 1999-2000, jamii ya Kitengela ilipoteza zaidi ya nusu ya mifugo yao. Katika kipindi hicho, mapato kutokana na mpango wa kukodisha yalifikia asilimia 80 ya mapato yote ya kaya zinazoshiriki kwenye mpango huu – huu ni msaada mkubwa.

Malipo yanatolewa kwenye sherehe za jamii zinazokuwa zimelengwa kuangukia wakati wa malipo ya karo/ada za shule, na mara nyingi zinalipwa kwa wanawake. Mpango wa kukodisha unafadhiliwa na kusimamiwa na mtandao wa mashirika yanayoongozwa na Mfuko wa Taasisi ya Wanyamapori Afrika na pia unahusisha Kenya Wildlife Service, Global Environmental Fund, na Friends of Nairobi National Park.

Mpango unalenga kuhifadhi eka 60,000 ambazo zitatosha uhamaji wa wanyamapori wa msimu wa kutoka na kuingia kwenye hifadhi.

Sura ya

3

# Utangulizi

# Hatua kuelekea mafanikio





*Kunenepesha ng'ombe kwenye shamba la malisho ya kunenepesha*

## HAT UA YA 1: PATA MSAADA UNAOUHITA JI

Inahitaji uzoefu na akili kuchagua, kuanzisha, kusimamia na kuitangaza biashara kwa mafanikio. Kwa hiyo jamii kwa kawaida hushirikiana na wawezeshaji, au "watu wa kati," ambao wanaweza kuwasaidia katika mchakato.

Mtu wa kati anaweza kuwa taasisi isiyokuwa ya kiserikali, serikali ya mtaa, washauri binafsi, au hata biashara – ili mradi ana uzoefu katika masuala ya CBV, na nia ya dhati katika kuhakikisha kunakuwa na uhakika kuwa anachokushauri kinalenga katika njia za kuleta kipato na chakula na uhifadhi. Mtu huyu wa kati vile vile, ataweza kutafuta uzoefu wa wataalamu wengine kuboresha wazo la biashara. Kwa pamoja watatoa taarifa na hamasa juu ya uhifadhi, faida na hasara za biashara fulani fulani, na mchakato wa kuanzisha biashara kama hiyo.

Mtu wa kati na wataalamu wengine wataisadia jamii:

- kutafiti ardhi na kufanya mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi;
- kuainisha raslimali ambazo jamii yaweza kuzitumia kuanzisha biashara yenye kuleta faida;
- kufikiria aina za biashara ambazo zitasaidia zaidi jamii kunufaika kwa muda mrefu;
- kuelewa na kutimiza matakwa ya kisheria, ikiwa ni pamoja na kupata hati miliki na vibali, kuandaa tathmini ya athari kwa mazingira, na kufanya majadiliano kuhusu mikataba;
- kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, mipango ya kugawana manufaa, mipango ya biashara, tathmini ya athari kwa mazingira, na usimamizi na ufuatiliaji wa mipango;
- kutoa mafunzo ya biashara na utalii, na pia mafunzo ya mabwana wanyamapori;
- kuhimili na kutatua migogoro;
- kutafuta na kujadiliana na washirika wa biashara, au "wawekezaji", kama inawezekana. Washirika wa biashara watahusika na kuandaa na kusimamia biashara – wakiilipa jamii kwa kutumia ardhi na raslimali nyinginezo; na.
- kufuatilia mipango yote kuhakikisha kuwa inafuatwa.

### TAASISI ZINAZOWEZESHA UENDELEZAJI WA CBV KATIKA NCHI ZA AFRIKA MASHARIKI

Mpango uitwao Kenya Wildlife Service Outreach unasaidia sana kwenye shughuli kama hizi nchini Kenya, kama ifanyavyo Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ya Tanzania (TANAPA) hapa Tanzania. Taasisi zisizo za kiserikali zenye uzoefu kwenye biashara zinazohusiana na uhifadhi katika Afrika Mashariki ni pamoja na zifuatazo:

- African Conservation Centre, www.conservationafrica.org
- African Wildlife Foundation, www.awf.org
- Frankfurt Zoological Society, www.zgf.de.German aid, GTZ, www.gtz.de/en
- Wildlife Conservation Society, www.wcs.org, na
- World Wildlife Foundation, www.worldwildlife.org.

## HATUA YA 2: ELEWA UNACHOTAKA KUKIANZA

Kila mmoja kwenye jamii anapaswa kujua anachotarajia kutoka kwenye biashara inayotegemea rasilimali inayomilikiwa na jamii. Mtu wa kati atasaidia kuhamasisha. Hata hivyo, mwishowe, ni jamii ambayo itakuwa sehemu ya biashara hiyo, wakipata manufaa na pia kujitoa. Hivyo, kila mmoja anahitaji kuwa na taarifa na kujua manufaa, madhara na jinsi biashara inavyokwenda.

Yafuatayo ni baadhi ya mambo unayoweza kutarajia na inaweza kuwa vizuri kuyajadili kwenye mikutano ya jamii:

### Mchakato unaweza kuwa mrefu na mgumu

Mchakato unajumuisha kukamilisha orodha ndefu ya mambo yanayohitajika kukamilishwa kisheria. Waweza kutakiwa kuandikisha ardhi yako, kupanga mpango wa matumizi ya ardhi (angalia sura ya 2), kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (angalia sura ya 4), na kutatua migogoro mipya au ambayo imekuwepo kwa muda mrefu (angalia sura ya 5). Vile vile unaweza kuhitaji kutafuta na kujadiliana na washirika wako (Sura hii).

Bila shaka shughuli hizi na nyinginezo zitahitaji mikutano mingi ya jamii, na mikutano na watumishi/wataalamu, watu wa kati, na wataalamu wa mazingira na biashara, wanaoweza kuwa washiriki wa biashara, na wengineo.


### Utalii ni biashara yenye changamoto, iwezayo kuleta hasara

Hata kama mngejenga hoteli ya kitalii ya kuvutia sana ulimwenguni, yenye mandhali ya kuona wanyamapori inayovutia sana, bado idadi ya wageni inaweza kuanguka kwa ghafla. Mambo ambayo yanatokea mbali na biashara yako yanaathiri idadi ya watu wanaosafiri: vita, mashambulizi ya kigaidi au hofu ya tukio kama hilo, matatizo ya kiuchumi ... Mwenendo wa utalii ni wa kuongezeka – kadiri ya asilimia 4 kwa mwaka nchini Tanzania – lakini matukio fulani fulani yaweza kuleta hali ya kusikitisha katika baadhi ya miaka. Jamii iko tayari kukabiliana na hali ya mapato inayobadilika badilika?

### Jamii yako itapata manufaa muhimu, na baadhi ya watu watapata ajira... lakini hawatatajirika

Kuieleza jamii kuhusu matarajio ya kweli juu ya biashara tangu mwanzo kutaweza kusaidia kuepusha watu kukata tamaa na migogoro baadaye wanapoona mambo hayaendi kama walivyotarajia.

Ni rahisi kuwa na matarajio yaliyo juu sana. Mapato kutoka kwenye hoteli ya kitalii inayofanya vizuri, kwa



*Utalii wa kupanda miamba*

mfano, yanaweza kuwa ya juu – lakini, hata hivyo, mapato hayo hayawezi kuzifanya kaya binafsi kutajirika.

Fikiria hoteli ya kitalii yenye mapato mazuri na inaweza kuipa jamii dola za kimarekani 30,000. Kama kiasi hicho kitagawanywa kwa vijiji sita, kila kijiji kitapata dola za kimarekani 5,000 tu.

Kama kijiji kina kaya 1,000, kugawana dola za kimarekani 5,000 kwenye kaya hizo kunamaanisha kuwa kila kaya itapata dola 5 tu.

Kaya haiwezi kufanya mambo makubwa kwa dola 5. Lakini dola 5,000 ni suala jingine. Kiasi hicho kinaweza kuwa mchango mkubwa kwenye maisha ya jamii. Kinaweza kusaidia kuezeka shule, kujenga madarasa, kuweka mahitaji kwenye zahanati, na kuchangia mahitaji ya shule au chuo. Kinaweza pia kuisadia jamii kuwekeza kwenye mbegu bora za mifugo au kilimo-misitu – kutegemea na mpango wao wa matumizi ya ardhi.

Kwa hiyo, jamii nyingi huchagua kutumia mapato kwenye miradi inayomfaidisha kila mmoja kwenye jamii.

### Hata hivyo, yawezekana bado zipo fursa nyingine za kuongeza kipato cha kaya

Kutegemeana na rasilimali zako, makundi yanaweza kukuza vyanzo vingine vya mapato, ambayo yatakwenda moja kwa moja kwenye kaya. Kwa mfano:

- Ufugaji nyuki. Mashirika mengi yanasaidia makundi kwenye jamii kuzalisha asali na mazao mengine



*Mradi wa jamii wa kufuga nyuki*

yatokanayo na ufugaji wa nyuki. Au, iwapo biashara ya utalii imekomaa, biashara hiyo inaweza kusaidia katika kuuza asali, nta na mazao mengine ya nyuki (Tazama kisanduku namba 2).

- Kazi za mikono. Vikundi vingi vya wanawake vimefanikiwa kuongeza pato la kaya kwa kuuza shanga, vikapu, vyungu, au kazi nyingine za mikono. Mtu wa kati na/au mshiriki wa biashara anaweza kuwasaidia wanawake kuboresha mitindo na mbinu za biashara, hivyo washiriki kupata malipo mazuri zaidi kutokana na juhudi zao. Wanaweza kuuza bidhaa zao moja kwa moja au kwa kuwaunganisha wazalishaji na wanunuzi watarajiwa – kama maduka au hoteli kwenye miji mikubwa (kisanduku namba 3).



*Wamasai wakicheza ngoma – mradi unaoweza kuanzishwa*

KISANDUKU NAMBA 2: **KUFUGA NYUKI, KUOKOA MISITU**

"Kwa sasa nyuki ni mifugo kama mbuzi na ng'ombe", anasema mwanachama wa kikundi cha kufuga nyuki cha Sangaiwe.

Kikundi cha Sangaiwe ni kimoja kati ya vile vilivyoanzishwa na kupewa mafunzo na TAWIRI. Kikundi kinajihusisha na kukusanya na kuuza asali, nta, na bidhaa nyingine zitokanazo na nyuki, shughuli ambazo ni moja ya namna jamii inavyonufaika na kutunza mazingira na miti: Kijiji kilianzisha vyote viwili: msitu wa hifadhi na hifadhi ya nyuki. Matokeo yake ni kuwa nyuki wanachavua, si tu mimea ya porini bali hata pia mimea ya kupandwa.

Kikundi kilianza mwaka 2008 na kinatarajia kupata mavuno yake ya kwanza mwaka 2009. Kwa kulinganisha na uzoefu kutoka kwenye vikundi vingine vya namna hii, wanachama wanaweza kujipatia dola 2.00 hadi 2.50 za kimarekani kwa lita moja.

Changamoto bado zipo kwa vikundi ambavyo TAWIRI ilivipatia mafunzo, hasa kwenye biashara, kwa sababu mara nyingi wanauza kwa madalali ambao wanachukua sehemu kubwa ya faida.

Nchini Kenya, Shirika la Honey Care Africa limewasaidia watu zaidi ya 9,000 vijijini katika nchi nzima kupata kipato zaidi, kwa kuwapatia vitendea kazi, mafunzo, kuwaunganisha na watoa mikopo, na uhakika wa bei nzuri kwa wafuga nyuki.

- Mauzo zaidi ya ng'ombe. Miradi ya majaribio inaendelea kuona kama inaweza kusaidia jamii kuongeza kipato kutokana na mauzo ya ng'ombe, kwa kutumia mbegu bora na kunenepesha mifugo katika mashamba maalum kwa kunenepesha.

Zipo namna nyingine zaidi, kutegemeana na maarifa yaliyopo kwenye jamii na maliasili zilizopo (tazama kisanduku namba 4).

## Fedha hizi utazifanyia nini? Kuandaa mpango wa kugawana manufaa

Utatumiaje mapato yatokanayo na biashara inayohusiana na asili? Jamii chache zimepata fedha za kutosha kulipa kaya moja moja kutokana na biashara. Hata hivyo, kiasi kikubwa – kipatacho dola za kimarekani 40,000 au zaidi, si ya kushangaza – huenda kwa jamii zinazowekeza kwenye biashara ya uhifadhi kwenye nchi za Kenya na Tanzania.

Hata kipato kinapokuwa kimegawanywa kwa vijiji vingi, kipato kinakuwa kikubwa kuliko vile kijiji kinavyokuwa

### KISANDUKU NAMBA 3: UTENGENEZAJI SHANGA HUKO ESELALEI: UHUSIANO WA MANUFAA NA ASASI ISIYO YA KISERIKALI

"Tungeliuza maziwa kama yangelikuwapo maziwa au kusaga ugoro wa kunusa na kuuuza ili kupata karo ya shule. Lakini tulikuwa fukara sana", anasema Noormegiroo Ngayai, Mwenyekiti wa Kikundi cha Akina mama Naisha kilichopo Eselalei.

"Halafu tulianza kusimama kando kando ya barabara kusubiri watalii wakija watupige picha kisha watulipe. Uongozi wa kijiji ulianza kutuuliza: "Kwa nini watoto wenu wanasimama barabarani badala ya kwenda shule?"

"Wazee walitusaidia kuunda kikundi, na Mbunge akaja kututembelea na akatupatia Shilingi za kitanzania 100,000 tununue mbuzi."

Hiyo ilikuwa mwaka 1999. Walipokuja kuunganishwa na AWF mwaka 2001, wanawake zaidi ya 20 kwenye Kikundi cha Akina Mama Naisho walikwishajaribu karibu kila kitu walichofikiri kingewasaidia kulingana na jina la kikundi chao, limaanishalo "matunda" kwa kiswahili. Mbuzi walisaidia ila hawakutosheleza. Kikundi kilijaribu kuuza shanga, lakini hazikuwa zimetengenezwa vizuri kiasi kwamba hata waongozaji watalii hawakutaka kuwapeleka kwao.

AWF iliangalia fursa iliyopo ya kuuza bidhaa zao za kazi za mikono na kuwapata wataalamu wa kukifundisha kikundi juu ya kusanifu, mitindo, na namna ya kudhibiti viwango, na pia kuwafundisha kigodo lugha ya kiingereza na utaalam wa biashara.

Mwaka 2003, kwa maombi ya kikundi chenyewe, AWF iliwajengea banda la biashara na sehemu ya kuoneshea biashara zao kandokando ya barabara. Bidhaa zikionesha jina la mtengenezaji wake zilining'inizwa kwenye kuta za banda. Picha nazo ziliwekwa zikionesha jinsi bidhaa hizo za kienyeji zinavyotumika kimila, kwa mfano kama mkanda wa mchunga mifugo, kitambaa cha shingoni cha akina mama, au kielelezo cha mtu kuwa na madaraka (mheshimiwa). Likiwa na madirisha makubwa, mapambo ya chuma na choo kwa ajili ya wateja, kituo kinawavutia wapita njia kusimama na kununua bidhaa zilizopo.

Baada ya banda kujengwa, pato la mwezi la kikundi lilipanda kwa wastani wa karibu asilimia 1,000, ingawa mabadiliko yanakuwepo kati ya msimu mmoja na mwingine. Hiyo inajumuisha na ada anayolipa mgeni akitembelea banda lao kwa gari, ambayo ni dola za kimarekeani 20.

"Awali tulikuwa tukiwaomba waume zetu na wazee watoe hela ya watoto. Siku hizi hatuombi tena", anasema Ngayai.

Baadhi ya wageni wanavutiwa na shughuli hizi kiasi cha kutaka kuuza bidhaa husika katika nchi nyingine. Mwaka jana kikundi kilipokea oda kutoka Earth Birthday Project huko kusini magharibi mwa USA ya shanga 12,000. Mwaka huu Naisho imeteuliwa kushiriki kwenye Maonesho ya Wanawake Wajasiliamali huko Barcelona kwenye mkutano wa dunia wa IUCN. Mshiriki mmoja aliuza bidhaa zenye thamani ya dola za kimarekani 1,250 ndani ya juma moja.

Pamoja na kusaidia kupata mahitaji ya familia, kikundi kwa sasa kinaweza kuchangia kwenye shughuli za jamii kama ujenzi na miradi ya maji.

Lakini mafanikio yanabadilika. Kwa ajili ya mafanikio yao, makundi mengine ya akina mama yameiga bidhaa za kikundi cha Naisho na namna ya kutangaza biashara zao. Hali hii imesababisha ushindani mkali, na wanakikundi wa Naisho wana wasiwasi wa biashara yao kupungua.

Hii ni hali ya kawaida ambayo humtokea kila mjasiliamali mwenye mafanikio. Unaweza kuwa na wazo lolote la kukisaidia kikundi kuanzisha biashara nyingine, au kuzalisha bidhaa tofauti, ili kiendelee kuwa mbele ya washindani wake?

---

kimekadiria. Kwa hiyo itabidi jamii ikubaliane na mpango wa kugawana mapato, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- Nani atasimamia mapato?
- Uwazi utahakikishwa vipi?
- Mapato yatagawanywaje?
- Unayo orodha ya vipaumbele vya jamii, ambavyo vitapewa fedha hizo? (kama shule, zahanati, kuwalipia wanafunzi karo kama za chuo kikuu, maji, afya ya mifugo ...)?
- Utafuatiliaje mapato ili kuhakikisha kuwa yanakwenda kule palipokubaliwa?

## HATUA YA 3: WEKA ALAMA MIPAKA YAKO

Ni muhimu kuwatumia watafiti wenye utaalam ili mipaka sahihi ya ranchi, vijiji, maeneo ya hifadhi, malisho ya mwaka mzima, malisho ya kiangazi, makazi, n.k. yaeleweke vizuri kwa wote. Weka alama za mipaka kama mawe – ambayo yametengenezwa kwa zege – au vitu vingine ambavyo si rahisi kuvihamisha. Tazama Sura ya 2 kwa taarifa zaidi kuhusu mpango wa matumizi ya ardhi na kusajili ardhi.

### KISANDUKU NAMBA 4: FIKIRIA KUWEKEZA KWENYE UZALISHAJI CHAKULA AU SHUGHULI NYINGINE ZA KIUCHUMI

Pamoja na miradi ya kijamii, fikiria jamii kuwekeza kwenye shughuli nyingine za kiuchumi, hasa uzalishaji wa chakula. Maeneo mengi ambamo kilimo na ufugaji vinafanywa kwa pamoja yanapata mvua kidogo. Na udongo wake usiokuwa mzuri unaweza kuchoka katika muda mfupi wa mwaka mmoja au miwili ya kulimwa kienyeji.

Lakini kuna aina mpya nyingi za kilimo, hasa cha "kilimo-misitu", kinachowezesha kuzalisha mazao mengi kwenye eneo dogo, na hapo hapo kurutubisha udongo na wakati huo huo kuhifadhi unyevu. Kilimo-misitu kinaweza kuzalisha vyakula vikuu, jamii ya karanga, malisho, kuni, miti ya kujengea, na miti shamba kwenye eneo hilo hilo kwa sababu mimea inapangwa vizuri kwa kufuata mazao ya mizizi, kabeji, na mahindi na hata miti midogo na mikubwa. Unatakiwa uchaguzi makini wa miti irutubishayo udongo wakati mizizi inasaidia kutunza unyevunyevu.

Kilimo-misitu kilichopangwa vizuri chaweza kuchukua eneo dogo kiasi hata cha kuliwekea uzio. Kwa zoezi la kupanga matumizi ya ardhi, utakuwa umekwishajua ni wapi pasipandwe mimea (yaani katikati ya njia za tembo).

Tembelea tovuti hii www.worldagroforestry.org kwa ajili ya habari zaidi. Kwa habari zinazohusu kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo na matumizi mengine, wasiliana na Southern and Eastern Africa Rainwater Harvesting Network, http://www.searnet.org

## HATUA YA 4: ANGALIA RASILIMALI ULIZONAZO. WAZA KWA UPANA NA TENGENEZA "NDOTO YA ORODHA" YA FURSA ZA BIASHARA

*MANENO YA BUSARA*

***Kitu muhimu kuliko vyote kwenye jamii ni kujua rasilimali walizonazo. Rasilimali hizi zitatoa mwongozo juu ya aina ya biashara unayoweza kufanya. Jirani zako wanaweza kuwa na hoteli ya watalii – lakini yawezekana eneo lenu ni dogo sana. Hata hivyo, panaweza kuwepo mimea au ndege wa aina ya pekee, mimea yenye maua yavutiayo nyuki. Mandhari ni rasilimali pia: inaweza kuwa kama maporomoko, na mlima au ziwa lenye mvuto kutazama. Hata ukaribu na kivutio kunaweza kuwa na thamani: mko karibu na barabara? Mko karibu na hifadhi ya wanyamapori, au kwenye eneo ambalo tayari watalii wanapita?***

*Thadeus Binamungu,*
*Ofisa Mradi Mwandamizi, AWF-TZ*

### HADITHI INAYOKUPA TAHADHARI: TAFITI KWANZA AU JUTA BAADAYE

Katika kijiji kimoja huko kusini mwa Kenya, timu ya wanakijiji na wataalamu walifanya mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi, wakachora ramani ya kijiji na maeneo yote yakatambulika, wakakubaliana kuhusu maeneo ya kilimo, malisho, makazi na mahali pa kunywesha mifugo maji. Mipaka ilionekana kufahamika vyema hivyo hawakumtumia mpima aliyesajiliwa.

Baada ya wahusika wote kufanya kazi kubwa, mwekezaji alitia saini kwenye mkataba na kijiji. Akijua kuwa atapata haki za ardhi na utalii wa kupiga picha, mwekezaji alijenga hoteli nzuri ya kitalii na akakubali kulipa mchango wa kila mwaka, ikiwa ni kwa kila mgeni atakayelala kwenye hoteli na gharama nyinginezo.

Mambo yote yalikwenda vizuri hadi siku moja ambapo mtu kutoka jamii jirani alipokuja. "Hoteli yako ipo kwenye ardhi yetu", alidai mtu huyo. Wapima waliosajiliwa waliitwa. Ilionekana kwamba ingawa kila mmoja "aliijua" mipaka, wote walikuwa wamekosea. Ilibidi apatikane mtu mwingine, aliye nje ya mgogoro, wa kusuluhisha, ambaye naye alitaka alipwe.

Shughuli zinazohusu hali asilia ni zaidi ya kambi na mahoteli! Mahali panaweza kuhimili idadi tu fulani ya mahoteli – kwa kuzingatia masuala ya mazingira na ya kiuchumi.

Ihamasishe jamii yako kuwaza – na kuota – kwa mapana zaidi.

Kwenye ngazi hii ya "ndoto", wanajamii wanaunda timu na wataalamu kutoka nyanja mbalimbali pamoja na: utalii, misitu, miradi ya misitu isiyokuwa ya mbao, kilimo, mifugo, biashara, masoko, na serikali. Timu inapita kwenye maeneo husika kuandaa orodha ndefu ya fursa za biashara kulingana na timu inachokiona. Vile vile wanaorodhesha ujuzi walionao wanajamii kwa ajili ya kupata mawazo zaidi.

Hizi ni baadhi ya rasilimali na mawazo ya biashara zinazohusiana na rasilimali hizo, ambazo zaweza kuorodheshwa kwenye hatua iliyofikiwa (Jedwali namba 1):

**FIKIRIA UNA RASILIMALI GANI INAYOKUZUNGUKA? HIYO ITAKUPA MWANGA KWA AJILI YA ZOEZI LA KUKUSANYA TAARIFA ZILIZOPO**

**Maliasili:** Jamii yako ina maliasili za aina gani? Wanyamapori wakubwa? Wanyamapori wanaotishiwa kutoweka au walio nadra? Mitishamba? Miti yenye maua yavutiayo nyuki? Mito au maziwa, nyanda tifutifu? Aina nyingi za ndege? Uwanda unaovutia? Mimea isiyo ya kawaida, kama mibuyu?

**Rasilimali watu:** Je, unao watu wenye ujuzi wa kazi za mikono za kitamaduni – shanga, ufinyanzi, kusuka mikeka na vikapu? Je waswaga mifugo, wawindaji? Watu waliofanya mafunzo ya biashara? wahasibu, wapishi, watu wakarimu katika kijiji? Watu wanaopenda kuimba na kucheza? Au kusimulia hadithi? Au wana mapenzi makubwa kwa miti?

## Rasilimali watu

Unaweza pia kuorodhesha watu wenye utaalam, waliopo kijijini. Yawezekana kuwa baadhi ya wakazi wana ujuzi au mapenzi juu ya aina fulani ya kazi kati ya zifuatazo (Jedwali namba 2).

Timu yaweza kuandaa orodha ya kuanzia, aina kama tano za miradi kwa utalii, kuongezea na kufuga nyuki na kulima uyoga. Juhudi za utalii zinaweza kuhusiana na hoteli ya kitalii inayoweza kuuza bidhaa za kazi za mikono kwenye duka lake; nafasi ya kwenda machungani pamoja na wazee; matembezi kwenye eneo la wazi mpakani mwa makazi na hifadhi, na banda la kufanyia maonesho ya ngoma za utamaduni na kusimulia hadithi.

## HATUA YA 5: FANYIA TATHMINI FURSA ULIZONAZO

Hii ni hatua inayojulikana kuwa ni hatua ya uangalifu, ikimaanisha kuwa katika hatua hii unapaswa kuchambua kwa karibu fursa zote zilizopo ili kuona jinsi zinavyoweza kutekelezeka, na matokeo yake kwenye jamii na mazingira. Manufaa yanayowezekana na pia shida zinazoweza kutokea zinapaswa kufikiriwa.

Tathmini inaangalia taarifa kama:

- Mradi unaotarajiwa unaweza kuboresha njia/ namna ngapi zinazotegemewa na jamii kwa kuingiza kipato na kupata chakula?
- Mradi huu unaweza kuwaathiri vipi wanawake, wanaume na pia watoto?
- Unaweza vipi kuathiri wanyamapori na makazi?

**HADITHI YENYE ANGALIZO: "KUWA MWANGALIFU" KWA MBIA MTARAJIWA**

Huko kaskazini mwa Tanzania, mwekezaji alitaka eka 100 ili ajenge kambi. Mwanzoni aliheshimu ahadi yake na kuilipa jamii dola za kimarekani zipatazo 10 kwa siku kwa kila kitanda kitakachotumika. Muda mfupi baadaye malipo yalisimama.

Inaonekana kuwa mwekezaji huyu alikuwa amepata mkopo mkubwa – na alitumia kambi kama dhamana. Aliweka pesa zake na benki ikachukua kambi. Baadaye benki iliuza kambi kwa mwekezaji mwingine, bila kuwasiliana na jamii.

Hali hii ingeweza kuepukwa kama pangelikuwepo uchambuzi na uangalifu kumchunguza mwekezaji: mali yake, historia ya kifedha, na uzoefu kutoka kwenye jamii nyinginezo.

Kwa bahati nzuri, mwisho wa hadithi hii ni mzuri. Ingawa alielezea kuwa ilitokea bila kutarajiwa, mwekezaji mpya alikubali kuilipa jamii sehemu ya mapato kwa kila kitanda kitakachotumika. Licha ya hivyo, aliweza kuitangaza kambi, ambayo inaingiza kipato kikubwa kwa kampuni na jamii kuliko awali. Malipo yaendayo kwa jamii yamegharimia shule, kituo cha afya, gari na karo shuleni.

- Maji na udongo?
- Ni aina gani ya rasilimali za kitaalam zitahitajika?
- Ni aina gani ya miundombinu itahitajika kujengwa, na ni nani atakayeijenga?
- Je, kuna uwezekano wa kuhitaji, na kuvutia, watu wengine wa nje kuja kuwekeza – sekta binafsi, mfadhili, au wote?
- Jamii nyingine zilikuwa na uzoefu gani juu ya biashara kama hii? Tazama kisanduku namba 5.

Mwisho wa zoezi hili, unaweza kuwa na biashara 5 hadi 7 ambazo zitakuwa nzuri kwa jamii na kwa kuzingatia sehemu mlipo, mahitaji, ushindani na kadhalika, ambavyo vyote vinaonekana kuwa vinawezekana.

## JEDWALI NAMBA 1: RASILIMALI ZA JAMII NA BIASHARA AMBAZO ZINAWEZA KUKUZWA

| Rasilimali | Fursa ya biashara |
|---|---|
| **JIOGRAFIA** | |
| Kilima au mlima; mto au ziwa | Kuanzisha hoteli ya kitalii |
| Bahari, maziwa, au mito | Michezo mbali mbali ya kwenye maji |
| Chemchemi au kijito chenye maji safi | Kiwanda cha kusafisha maji na kuyajaza kwenye chupa |
| Chemchemi yenye maji ya joto | Biashara ya kupumzisha viungo, mishipa na ubongo kwa kukaa katika chumba cha joto |
| Miinuko, milima | Kupanda milima |
| Maeneo yenye vivuli na udongo mzuri | Biashara ya kilimo cha uyoga |
| Ardhi yenye maji mengi | Kilimo-misitu kwa ajili ya matumizi kijijini na kuuza matunda na mbogamboga kwenye hoteli zilizopo karibu (tazama kisanduku namba 4 juu ya kilimo-misitu). |
| **MIMEA** | |
| Mitishamba | Kuwatembeza wageni kuona mimea mbali mbali katika "Kutafuta aina za mimea fulani Fulani": kuuza mitishamba kwa watengeneza dawa kwa malipo kama itakavyokubalika |
| **MISITU** | Mazao ya misitu yasiyokuwa mbao |
| **MIFUGO** | |
| Kuboresha uzalishaji | Aina bora ya mifugo, pia vijishamba vya malisho na machinjio |
| Kwa ajili ya utalii | Kwenda na wageni machungani |
| **RASILIMALI ZENYE HISTORIA NA ZA KITAMAUDUNI** | |
| Sanaa ya miamba | Utalii; kuswaga mifugo |
| Maeneo ya kihistoria au vivutio maalum | Utalii |
| Makazi au Boma za kuishi | Kufanya sanaa za maonesho; shirikisha wageni kwenye ngoma na muziki |
| Kazi za mikono na sanaa za kuvutia | Kubuni mitindo na kuuza shanga na kazi nyingine za mikono; Kuanzisha darasa la kuwafundisha wageni kutengeneza shanga |

## JEDWALI NAMBA 2: ORODHA YA STADI

| Ujuzi au mapenzi ya mtu katika kufanya kitu | Kazi zinazoweza kufanyika chini ya CBV |
|---|---|
| Biashara | - Uhasibu<br>- Huduma<br>- Mapishi |
| Ujuzi kuhusu wanyama na mimea | - Kuchunga mifugo<br>- Kuswaga mifugo au kuwinda<br>- Kutayarisha na kutumia mitishamba<br>- Bustani, kuzalisha bidhaa maalum kama mimea ya dawa |
| Kazi za mikono, sanaa za maonesho | - Kutengeneza shanga<br>- Kazi za kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi<br>- Ufinyanzi, kutengeneza vikapu, au bidhaa nyinginezo<br>- Kupaka rangi<br>- Useremala, kutengeneza samani |
| Sanaa za maigizo | - Kucheza ngoma, kuimba<br>- Kusimulia hadithi<br>- Michezo ya kuigiza kwa watalii au kwa shughuli za kielimu |

## HATUA YA 6: ANDAA MCHANGANUO WA AWALI WA BIASHARA

Mchanganuo wa biashara unachambua kwa kina juu ya kitu gani kitahitajika kwa ajili ya aina fulani ya biashara, umahiri (nguvu/sifa) na mapungufu yake ikilinganishwa na washindani wake, na pia matarajio ya mapato. Vile vile mchanganuo utaeleza udhaifu, nguvu au sifa, fursa na mambo yatakayotishia uhai wa biashara. Hiyo itaifanya biashara hiyo kueleweka vizuri.

### KISANDUKU NAMBA 5: VIPI KUHUSU UWINDAJI?

Katika baadhi ya nchi, jamii zinafaidika sana kutokana na utalii wa uwindaji ulio halali, na kwa hivyo kuzuia ujangili na kuwezesha idadi ya wanyamapori kuongezeka kwa haraka. Namibia, kwa mfano, jamii inapokea asilimia 100 ya mapato yatokanayo na wanyamapori, ikiwa ni pamoja na uwindaji. Katika muongo uliopita, jamii 50 zilikuwa zimeunda hifadhi, ambazo kwa sasa kwa pamoja zinaingiza kiasi cha dola za kimarekani zipatazo milioni 2.5 (kama shilingi za kitanzania bilioni 3) kwa mwaka. Hifadhi nyingine zinaingiza zaidi ya dola za kimarekani 100,000 (ambazo ni kama Shilingi za kitanzania milioni 120) kwa mwaka. Hata idadi ya wanyama ambao hapo awali walikuwa wanatishiwa kuisha kama kifaru, sasa inaongezeka hata kwenye hifadhi za jamii.

Nchini Tanzania, malipo ya uwindaji yanaendelea kukusanywa na serikali kuu, wakati jamii wanapata sehemu tu ya malipo hayo. Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori zilianzishwa katika miaka michache iliyopita kwa matarajio kuwa jamii itasimamia uwindaji kwenye maeneo yao, lakini sera bado zinaboreshwa (tazama sura ya 4). Na idadi ya wanyamapori bado inapungua kwenye maeneo mengi.

Kenya, ambayo imepiga marufuku uwindaji, nayo inakabiliwa na kupungua kwa idadi ya wanyamapori – isipokuwa kwenye maeneo ambayo jamii imefanikiwa kuunda CBVs zenye mafanikio.

Wawindaji wanatumia fedha nyingi zaidi kwa wastani kwa mtu kuliko ilivyo kwa utalii wa kupiga picha, kwa sababu ya leseni, ada za "kombe" (trophy), n.k. Lakini watu wengi wanaweza kwenda kwenye utalii wa kupiga picha kwenye eneo fulani. Licha ya hivyo, utalii wa kupiga picha unatumia miundombinu zaidi – kambi, hoteli, barabara, kwa hiyo utalii huu unaweza kuzalisha nafasi nyingi za kazi na mapato kutokana na huduma nyinginezo (TNRF 2008).


- **Umahiri:** hazina ulizonazo na mazingira yanavyokusaidia kufanya vizuri ikilinganishwa na washindani wako. Kwa mfano, unaweza kuwa na wanyamapori zaidi kuliko eneo jingine lolote karibu na barabara fulani.
- **Udhaifu:** kwa mfano, kunaweza kuwa na tatizo la kukosekana kwa chanzo cha maji kinachoaminika.
- **Fursa:** kwa mfano, kuwa karibu na mapito ya watalii ambayo yamejengeka; mwenyeji ambaye tayari anafuga ngamia.
- **Vitisho:** Nchini Tanzania, kwa mfano, inaweza kuwa kwenye kitalu cha uwindaji, ambacho kitakinzana na utalii wa kupiga picha.

Mchanganuo wa biashara pia unaangalia masuala kama ushindani, mazingira ya kisheria na kodi, mahitaji ya uwekezaji, miundombinu inayohitajika, changamoto za usimamizi na ufuatiliaji, fursa za masoko zilizopo, mahitaji ya wafanyakazi kutoka ndani na nje ya jamii, muda unaotakiwa kuizindua, malengo ya mapato kwa mwaka mmoja na miaka mitano ...

## HATUA YA 7: VUTIA WADAU WENGINE KATIKA BIASHARA

Kama biashara itahitaji uwekezaji mkubwa na/au utaalam maalum, ubia waweza kuwa njia nzuri zaidi. Tena, mwezeshaji wenu atawasaidia kupata mbia, au "mwekezaji" anayestahili.

Wanapaswa kuhakikisha kuwa mwekezaji ana kila kitu kinachotakiwa kufanikisha biashara: uzoefu, fedha, mawazo, na kujitoa kwake kwa jamii, na mtazamo chanya juu ya mazingira.



*Mradi wa jamii wa kilimo cha uyoga*

## Njia za kupata mbia wa biashara

a) "Machapisho yanayoelezea wafanyabiashara na biashara zao" yanaweza kusaidia kuanza mchakato. Likiwa tangazo au chapisho linalovutia na linalohabarisha – ambalo linaweza kuandaliwa kwa msaada wa mbia – machapisho kama hayo ya biashara yanajibu maswali mengi ya msingi ambayo mwekezaji angependa kuuliza:

- Kwa nini mwekezaji awazie biashara hii badala ya fursa nyingine anayoweza kuipata?
- Ni vitu gani mahsusi na rasilimali ulizonazo – kuanzia miundombinu hadi wanyamapori na sifa za mambo ya kimila – zitakazochangia biashara kuwa yenye faida?

Chapisho linaweza kupelekwa kwa wawekezaji ambao tayari unaona wana nia ya kuja kuwekeza. Unaweza pia kulisambaza chapisho kwa kutumia mtandao wa kompyuta au namna nyingine ili iwafikie wafanyabiashara mbalimbali.

b) Wasiliana na wawekezaji wanaofahamika. Kujitambulisha kwa wafanyabiashara ambao tayari wamekwisha wekeza kwenye biashara kama unayoifikiria ni njia sahihi ya kumpata mbia mtakayeweza kuelewana.

***"Jihadhari na matarajio makubwa kutoka kwa mwekezaji: "Kama mbia amekuwa pia mfadhili kwenye jamii – labda alijenga kliniki – jamii yaweza kuwa na matarajio kwamba ataendelea kufadhili mambo mengine. Matarajio ya namna hii yanaweza kuwa hatari ... yanaweza kuwafanya watu wafikirie kuwa wapo kwa ajili ya kupewa misaada. Lakini ili iweze kuwa endelevu, biashara lazima ijengwe kwenye misingi ya biashara, siyo misaada***

*Ben Mwongela*
*Meneja, Huduma za Miradi*
*AWF, Kenya*

c) Andaa "mkutano wa wawekezaji" na kutembelea sehemu inayolengwa. Kwenye mkutano wa wawekezaji, wawakilishi wa makampuni ya biashara yenye uzoefu hukutana na NGOs na wajumbe kutoka kwenye jamii. Hapa unawasilisha fursa ya biashara na kujibu maswali yote watakayouliza. Bila shaka mkutano wa wawekezaji utafuatiwa na safari ya kutembelea sehemu inayolengwa kuwekeza. Matembezi hayo yanaweza kuwa ya pamoja, mtu mmoja mmoja au kwa makundi.

d) Tangaza "tenda." Kwa kupitia mialiko binafsi au hata tangazo kwenye gazeti, makampuni yanakaribishwa kushindana – au kutuma andiko la mradi juu ya fursa ya biashara hiyo. Kila kampuni yenye nia itaandika andiko lake la mradi, likionesha jinsi watakavyofanya biashara inayokubalika kwa jamii na isiyoathiri mazingira.

Waweza kuwataka waombaji walete habari zifuatazo:

- Ni kwa kiasi gani kampuni itakuwa tayari kulipa kwa kukodisha, kila kitanda kinapolaliwa na mgeni, mfuko wa maendeleo wa jamii, hifadhi na ushuru mwingineo
- Kuahidi kuwaajiri wanakijiji na kuwapa mafunzo
- Miundombinu waliyo tayari kuijenga, na nani atakaimiliki
- Aina na kiwango cha juhudi za masoko zilizokwisha ahidiwa ili kuhakikisha mapato mazuri
- Muda wa ukodishaji anaoutaka mwekezaji
- Hatua zitakazochukuliwa kuhakikisha mazingira hayachafuliwi, kama kutumia nguvu za mionzi ya jua, kudurufu vitu, hifadhi ya maji...
- Shughuli nyingine na jamii: kwa mfano: watakubali kuuza asali iliyozalishwa kijijini au bidhaa za kazi za mikono zilizozalishwa kijijini? Watakubali kununua vitu kama hivi kwa ajili ya biashara yao, kwa mfano kununua mikeka au majani ya kuezekea kwa ajili ya hoteli?

## HATUA YA 8: CHAGUA MBIA

Kwa vyovyote, juhudi zako zitakuwa zimeishaibua fursa nzuri za uwezekano wa kumpata mwekezaji. Sasa timu kutoka kwenye jamii, mwezeshaji, serikali, na wadau wengine wanayapitia maombi ili kuyalinganisha na kukubaliana nani mshindi.

## HATUA YA 9: JADILIANA KUHUSU BIASHARA

Ingawa unalo andiko la mradi tayari, lakini kujadiliana kutagusia undani wa, kwa mfano, Nani anatoa nini? Nani anapata nini? Nani anafanya nini? (tazama kisanduku namba 6).

Yafuatayo ni baadhi ya masuala ambayo mara nyingi hujadiliwa. Ada nyingine zinaweza kuwa zinapangwa kufuatana na taratibu zilizowekwa na serikali, lakini hata hizo zinaweza kujadiliwa kwa kiwango fulani.

- Umiliki wa biashara: Jamii itamiliki biashara kwa pamoja na mwekezaji? Au patakuwa na uwezekano wa hali hiyo kutokea muda ujao katika tarehe iliyopangwa?

### KISANDUKU NAMBA 6: MAKUBALIANO "MAZURI" NI YAPI?

Unaweza kusikia: "Kampuni X inaipatia jamii dola za kimarekani 50 kwa malazi ya siku moja kwa kila kitanda wakati sisi tunapewa dola 10 tu!" Au. Kampuni Y inachangia kwenye mfuko wa jamii wakati mbia wetu anatoa ushuru wa mfuko wa maendeleo ya jamii tu!"

Kama ambavyo kila sehemu na kila jamii inatofautiana, kila makubaliano nayo hutofautiana. Mkataba wowote utategemea mazingira ya kisheria yanayouzunguka, aina za rasilimali zinazohusika, utaalam, mitazamo na mahitaji ya wanaohusika kwenye majadiliano – na fursa walizo tayari kuzipoteza ili kuzipata nyingine.

Unaweza kukuta katika sehemu moja, hoteli inaweza kuwa imekwishajengwa tayari, kwa hiyo kiwango cha kukodisha kikawa cha juu; mahala pengine, mwekezaji analazimika kuongeza majengo, kwa hiyo kiwango cha kukodisha na ada nyingine kwa wakati huo vinaweza kuwa vya chini. Katika jamii moja, nafasi za kazi na vyanzo vya maji vinaweza kuwa vinapewa kipaumbele kuliko ada ya kuangalia wanyama; mahali pengine, mwekezaji anachangia katika mfuko wa maendeleo, na hivyo kuchangia kidogo kwa malazi ya siku moja kwa kila kitanda, na kadhalika.

Kitu kimoja tu ambacho ni cha uhakika ni kuwa: Jamii na mwekezaji lazima wakubaliane kuwa wote watafaidika. Kila upande unahitaji kuona kuwa huenda haukuingia kwenye makubaliano yaliyo "bora sana" lakini "mazuri". Wataalamu wa majadiliano wanasisitiza kuwa kama upande mmoja unahisi umepunjwa, makubaliano hayo yamo kwenye hatari ya kuvunjika.

Ni rahisi matarajio kutotokea. Na inawezekana pia usipate kila kitu unachokitaka. Lakini hapa ni baadhi ya maswali ya kujiuliza kabla ya kutia saini:

- Je, makubaliano yatakuwa na faida kuliko kama tusipoingia katika makubaliano hayo?
- Je, utaratibu ni mzuri kiasi cha kuiletea jamii mabadiliko ya kweli na ya kimaendeleo?
- Makubaliano yanairidhisha jamii kuheshimu mipaka itakayowekwa kwa matumizi mbalimbali ya ardhi, kwa mfano, kutokiuka maeneo yaliyotengwa kwa kilimo au kufuga?
- Makubaliano ni ya muda mrefu kiasi cha kutosha kugharimia mahitaji yaliyokuwapo kwa muda mrefu ya miundombinu au huduma za jamii?
- Upande mwingine unaonekana kuridhika? Hili ni muhimu kuwafanya wabakie kwenye makubaliano.

Yawezekana makubaliano si mazuri sana kama ambavyo ungependa – lakini yanaweza kuwa yanafaa kwa kiasi chake na yanaridhisha. Ukiona hivyo basi ni vema kuyakubali na kuendelea na hatua zinazofuata.

---

- **Umiliki wa majengo:** Ni vema kama jamii ingelimiki mali zote zisizohamishika makubaliano yakifikia mwisho. Kwa mfano, jamii itamiliki hoteli au maegesho ya mitumbwi, wakati kampuni inaweza kutaka kumiliki mali inayohamishika – samani, vyombo vya jikoni, mapambo, n.k., ambavyo wanaweza kuhamisha mkataba wao ukifikia mwisho.
- **Usimamizi wa hifadhi:** Jamii inakubali kuheshimu usimamizi wa maeneo yake, na hasa yaliyo kwenye makazi, malisho, malisho wakati wa ukame; wanyamapori tu? Utakubali kuhakikisha kuwa mipaka ya maeneo hayo inaheshimiwa, kwa kuwatumia mabwana wanyamapori au mamlaka nyinginezo zisaidie katika usimamizi huo?
- **Matumizi binafsi:** Jamii inatoa mamlaka ya "matumizi binafsi" ya hifadhi yake kwa mwekezaji? Mara nyingi hili ni wazo zuri. Vile vile huishia kwenye kupata malipo mazuri zaidi.
- **Malipo kwa jamii:** Kwa malipo juu ya makubaliano ya kutumia eneo la jamii, kwa kawaida mwekezaji analipa:
  - Ada ya mwaka
  - Sehemu ya gharama ya malazi ya kila siku kitanda kinapolaliwa na mgeni
  - Ada ya uhifadhi
  - Ada ya mfuko wa maendeleo ya jamii
  - Ada ya sanaa za maonesho, iwapo jamii inataka kuanzisha sanaa za maonesho au mambo mengine ya ki-utamaduni.

Pia, kunaweza kuwa na mengi au pengine pungufu zaidi ya hayo yaliyoorodheshwa. Mchanganyiko wa mambo hayo na viwango vyake vya ada vinaweza kupangwa kwa majadiliano.

- **Ajira**
  - **Idadi:** Iwapo suala la ajira ni muhimu kwa jamii yako, katika majadiliano onesha kuwa asilimia (kwa mfano kama 60%) ya wafanyakazi watoke kwenye jamii yako. Wanaweza kufanyakazi za uashi, kuongoza wageni, ulinzi, uhudumu/mapokezi, masuala ya kuburudisha .... Inawezekana kuhitaji mpango wa mafunzo na kuwaongezea wafanyakazi ujuzi.

- Taratibu za kuajiri: Wanajamii wataajiriwa kwa utaratibu upi? Ushiriki wa jamii unaweza kusaidia kuhakikisha kuwa wanajamii wanafikiriwa kwa ajira hizi na wanalipwa viwango vinavyoridhisha.
- Posho: Kampuni itatoa viwango gani vya posho? Je viwango hivyo vinalingana na malipo yatolewayo kwa ajira kama hiyo katika eneo lako? Ni viwango vya juu kuliko jamii inavyotarajia kupata kutokana na mifugo au kazi nyingine za kawaida kijijini?

- Usimamizi wa mazingira: "Utalii wa mazingira" unamaanisha kufanya biashara katika namna inayowezesha viumbe hai vyote kubaki vikiwa endelevu – "ekolojia" ya ardhi na watu. Kwa faida ya jamii yako, na ulimwengu kwa ujumla, unaweza kuitaka kampuni kutekeleza taratibu nzuri zilizokubalika kwenye utalii wa mazingira na kuweka wazi mipango yao kwa ajili ya mfumo wa kusimamia mazingira. Tazama kisanduku namba 7 kwa mawazo zaidi.
- Muda wa ubia: Kama mbia anawekeza kiasi kikubwa cha pesa, anaweza akataka uwepo ubia wa muda mrefu (upatao miaka 10 hata 20, na kuwepo fursa ya kuandika mkataba upya) kuruhusu gharama za kuwekeza kurudi na kupata faida.
- Kipengele cha kuvunja mkataba: Je, vipi kama biashara haikwenda vizuri? Na hasa kama kampuni haina uzoefu wa kutosha kwenye utalii, fikiria kipengele kitakachowezesha jamii kuvunja mkataba iwapo biashara itakwenda chini ya kiwango fulani kwa muda fulani. Hata hivyo, ieleweke kuwa idadi ya wageni yaweza kushuka ghafla kwa sababu za kitaifa au kimataifa, zilizo nje ya udhibiti wa kampuni.
- Mapitio ya mara kwa mara: Mnaweza kupanga kuurejea mkataba kila baada ya miezi mitatu au kipindi mtakachokubaliana ili kubaini ni kitu gani kinaendelea vizuri na kipi hakiendelei vizuri, jinsi makubaliano yanavyotimizwa, na jinsi jamii na mwekezaji wanavyoweza kushughulikia tatizo lolote.

Mnavyoendelea kujadiliana bashiri:

- Ni yapi kati ya maboresho hayo ambayo mbia wako anapanga au anakubali yatekelezwe?
- Ni yapi wanayoweza kuwa wanawazia kuisadia jamii iyatekeleze?
- Mshawishi mbia wako kufikiria kusajiliwa na kutambulika na jumuiya ya utalii unaojali ekolojia (tazama kisanduku namba 7).

### KISANDUKU NAMBA 7: UTALII WAKO WAZINGATIAJE "EKOLOJIA"?

"Utalii wa ekolojia" si neno tu la kufurahisha. Ni sanaa mahsusi ya utalii wa kuwajibika.

Kwa ujumla serikali huwa zinataka CBV zifanye "Tathmini ya Athari za Mazingira" ili kusaidia kuepuka matokeo yasiyotarajiwa ya kuharibu mazingira. Lakini biashara za Ekolojia zinaangalia kwa undani zaidi ya viwango vya chini na zaweza kulipisha viwango vya juu, kwa sababu uwajibikaji juu ya mazingira unathaminiwa na wateja wengi.

Ili kuweza kuitwa utalii wa mazingira, lazima biashara iwe "rafiki" kwa mazingira kwa namna zote, kwa mambo yanayoonekana wazi na yasiyoonekana wazi. Kwa "hoteli ya kitalii ya ekolojia", kwa mfano, inamaanisha kuwajibika katika:

**Nishati:** Shughuli nyingi za utalii zilizo endelevu zinatumia "nishati inayojizalisha yenyewe: vyanzo vya nishati haviishi vinapotumiwa. Kwa namna inavyoongezeka, waendesha shughuli hizi wanafunga vifaa vitumiavyo nguvu ya jua kuzalisha umeme; matanki yatumiayo nguzu za jua kuchemsha maji, na mitambo ya kutumia upepo kufua umeme. Badala ya kutumia kuni au mkaa kwa kupika, watu wengine wanatumia "mkaa" maalum uliotengenezwa kutokana na mabaki ya vitu. Katika eneo la Maasai Mara, kuna angalau asasi moja isiyo ya kiserikali (iitwayo *"the Millennium Fuel Project"*) inayovisaidia vikundi vya akina mama kutengeneza mkaa huo kwa matumizi ya nyumbani na kuuza kwenye kambi za watalii.

**Usimamizi wa taka:** Hoteli nyingine zinatumia "taka za kijani", hasa mabaki ya chakula, kutengeneza mboji ambayo wanaitumia kwenye bustani zao za mboga. Masalia yasiyoweza kuoza (makopo, chupa, karatasi, betri) yanaweza kusafirishwa kupelekwa kwenye viwanda vya kuyeyushia na kutengeneza bidhaa nyingine. "Ardhi oevu ambazo si za asili bali za kutengenezwa", hutumika kusafisha maji machafu na aina nyinginezo za majimaji kwa kutumia mabwawa. Aina mahsusi za mimea inayotoa sumu na bakteria kwenye maji, hutumiwa kuyasafisha ili yatumiwe tena.

**Uhifadhi wa maji:** Kupungua kwa vyanzo vya maji ni mgogoro unaokua kila siku kati ya binadamu na wanyamapori. Waendesha miradi ya hoteli za kitalii wanaweza kupunguza matumizi ya maji kwa kuwataka wageni kutumia taulo zaidi ya mara moja kuwezesha kutumia maji kidogo kwa kufua. Wanaweza kufunga mabomba yanayotoa maji kidogo na vyoo vinavyotumia maji kidogo. Wanaweza kuvuna maji ya mvua. Wanaweza kuisaidia jamii kuotesha miti kwa ajili ya kuni na kuhifadhi vyanzo vya maji.

Kwa mawazo zaidi tembelea: www.ecotourismkenya.org.

### MFANO WA BIASHARA INAYOHUSIANA NA JAMII: KOIJA STARBEDS, LAIKIPIA, KENYA

Katika kipindi cha ukame wa mwaka 1997-2000, Ranchi ya Koija iliyopo Laikipia, kaskazini mwa Kenya, ilipoteza asilimia 70 ya mifugo yake. Kwa sababu inaonekana kuwa matukio ya ukame yanaongezeka, ilionekana wazi kuwa jamii ya wafugaji ingefaidika kutokana na kuwepo mikakati ya ziada kwenye njia wanazozitegemea ili kumudu maisha. Licha ya hivyo, sehemu ipo kwenye mfumo wa ekolojia moja kati ya zile zenye rasilimali kubwa ya wanyamapori nje ya maeneo ya hifadhi na karibu na ranchi ya Loisaba, ambayo imefanikiwa sana katika shughuli za utalii.

Mwaka 2001, wamiliki wa Loisaba, ambao ni AWF na jamii, waliunda ushirikiano ujulikanao kama Koija Conservation Trust (KCT) ili kuanzisha hoteli ya kifahari lakini ndogo, kwenye ardhi ya jamii. Koija Starbeds, kwa ufupi, ni majengo mahsusi ya miti, yaliyopo nyikani, yaliyoanzishwa baada ya kuona biashara kama hivyo inafanikiwa huko Loisaba.

Kinachotofautisha biashara ya Koija ni muundo wake na ukweli kwamba mahali ilipo huduma hiyo na huduma wanazotoa ni za moja kwa moja kiasi kwamba wafanyakazi wote wanatoka kwenye jamii ya hapo.

Biashara inamilikwa na kusimamiwa na Koija Conservation Trust (KTC) - ubia wa AWF na Loisaba, kupitia kampuni ya Oryx na jamii. KTC inasimamiwa na bodi ya wadhamini, wawili kutoka Koija Group Ranch, wawili kutoka Loisaba na mmoja kutoka AWF.

Ni jambo la kushukuru kwamba tangu kuanzishwa, biashara imekuwa ikienda vizuri na faida imekuwa ikipatikana kuanzia mwaka wa kwanza wa baishara. Mwaka 2007, jamii ilikuwa imekwishapokea zaidi ya dola za kimarekani 77,000 ambazo kiasi kikubwa kati ya mapato hayo kilikwenda kwenye miradi ya maendeleo ya jamii ikiwa ni pamoja na michango ya shule kwenye mradi wa "Uhifadhi kwa Ajili ya Elimu". Mgao wa mapato hupangwa na wajumbe wa ranchi ya pamoja wakati wa mkutano mkuu wa mwaka.

Licha ya hivyo, wanajamii 25 wameajiriwa wakati wavulana wapatao 30 na wasichana 45 wanapata malipo kutokana na sanaa za maonesho na kazi za mikono katika kijiji cha utamaduni, kilichotokana na biashara hiyo.

Ardhi inaonekana kurudia hali yake ya zamani na wanyamapori kuongezeka. Ni jambo la kushukuru kwa faida hizo, mahojiano na jamii yanaonesha kuwa mtazamo wao kuhusu wanyamapori umekuwa mzuri. KTC inatarajia kuwa biashara itaendelea kukua na kuleta manufaa zaidi kwa jamii ambayo inaitegemea biashara hii kwa kipato na chakula.

## HATUA YA 10: YAFANYE MAKUBALIANO YENU YAWE RASMI

- Hakikisha kuwa kila mmoja anaelewa mkataba unamaanisha nini: mtakachopata, lakini pia kile unachoahidi kufanya au kutofanya.
- Hakikisha kuwa kila kitu mlichokubaliana kimeandikwa.
- Hata siku moja usije ukaanza kujenga mpaka kila kitu kimeeleweka, kimekubalika, na kutiwa saini.
- Hakikisha kuwa makubaliano yanatoa nafasi ya kuyarejea mara kwa mara, hasa kuangalia jinsi biashara inavyoendelea kwa mtazamo wa kila upande, na uwezekano wa kufanya mabadiliko, ikibidi.

## HATUA YA 11: KUFUATILIA, KUUREJEA MKATABA NA KUUFANYIA MABADILIKO

Kuurejea mkataba kulikoandikwa hapo juu kunaweza kupangwa kufanyika kila baada ya miezi mitatu, au hata mara nyingi zaidi hasa mwanzoni. Kwenye mikutano mikuu, marejeo haya yatazifahamisha pande zote masuala kama haya yafuatayo:

- Makubaliano:
  Makubaliano yote yanaheshimiwa?
  Kama kuna vipengele ambavyo vinaweza kusababisha kutoelewana, washiriki wa pande zinazohusika wataviwekaje sawa?
  Kuna mafanikio yoyote yaliyopatikana katika kushughulikia migogoro iliyoonekana kwenye marejeo yaliyopita?
- Malengo ya biashara
  Je, ujenzi na makadirio mengine, kama idadi ya wageni, ni kama malengo?
  Kama sivyo, kwa nini? Na ni kitu gani kinaweza kufanyika ili mambo yaende kama yalivyopangwa?

- Mapato ya jamii:
  Jamii imekwishapokea fedha kiasi gani, kulinganishwa na matarajio yaliyokuwepo?
  Jamii inatumiaje mapato hayo?
  Matumizi hayo ni kama yalivyo kwenye makubaliano na mipango?
  Iwapo miundombinu inajengwa, inaendelea kama ilivyopangwa?
- Matokeo kwenye jamii:
  Ni mabadiliko gani yaliyokwishaonekana kwenye shughuli ambazo jamii inazitegemea kupata kipato na chakula, iwe chanya au hasi?
  Ni mabadiliko gani, kama yapo, yaliyokwishaonekana kwenye mahusiano ya kijinsia kutokana na mabadiliko kwenye uchumi wa jamii?
- Madhara kwenye mazingira au wanyamapori:
  Ni madhara au mabadiliko yapi yameonekana kwenye malisho, udongo, vyanzo vya maji, au wanyamapori, ambayo yanaweza kuhusishwa na CBV au wageni?
  Kama ni chanya, ni vipi yanaweza kuibadilisha jamii na CBV?
  Kama ni hasi, zinaweza kukabiliwa je?

Sura ya
3

# Hatua kuelekea mafanikio

# Mambo muhimu ya kukumbuka

1 Jamii za vijijini mara nyingi zina fursa za biashara kuliko jamii inavyofikiri, na rasilimali zaidi, za watu na za asili. Kwa mfano, mabadiliko ya ghafla ya muinuko wa nchi, au hata sura ya mwamba, yanaweza kuwa ya thamani kwenye soko la utalii. Ufugaji nyuki unawaletea maelfu kipato katika Afrika Mashariki tu. Inaweza kusaidia kuingia ubia na asasi isiyo ya kiserikali au shirika jingine kusaidia kuendeleza biashara inayohusiana na mambo ya asili.

2 Jamii inapoingia ubia na mwekezaji, mapato ya jamii yanatofautiana sana, kutegemea kwa kiasi fulani aina ya biashara na kwa kiasi kingine kwenye uwezo wa jamii kujadiliana, na wawezeshaji wa jamii hiyo. Ni muhimu kwamba mienendo yote ya fedha iwe wazi na jamii yote ielewe na kujituma kwa dhati katika biashara na masuala yaliyomo kwenye mkataba.

3 Ni muhimu kuangalia jinsi ya kugawana manufaa na kuweka mahesabu wazi kabla mapato hayajaanza kupatikana. Ila tu kama mapato ni makubwa, yaweza kuwa vizuri zaidi kuwekeza mapato hayo kwenye huduma za elimu na afya, na miradi mingine ya jamii, kuliko kuyagawanya kwa kila kaya. Lakini watu binafsi wanaweza kupata soko kwa bidhaa zao za kazi za mikono au asali au bidhaa nyinginezo kupitia kwenye CBV kubwa.

4 Aina mpya za manufaa zinaibuka kwa wale waishio kwenye mazingira ambayo pia yana wanyamapori. Aina hizi ni pamoja na malipo kwa kijiji kusaidia usimamiaji wa kimila wa ardhi yao; na pale ambapo ardhi tayari imegawanywa, malipo kwenda kwenye kaya husika. Ni muhimu kwamba mapato yasaidie vitu ambavyo tayari jamii inataka kufanya, kama kuendeleza ufugaji wa kienyeji na matumizi mengine endelevu ya ardhi.

# Mambo muhimu ya kukumbuka

## FAHARASA

**Baldus, R.D., Kaggi D.T. and Ngoti P.M.** 2004. Community based conservation (CBC): Where are we now? Where are we going? Miombo 27: 3,7,10.

**Baldus, R.D. and L. Siege.** 2001. Experiences with Community Based Wildlife Conservation in Tanzania. Tanzania Wildlife Discussion Paper No. 29. Dar es Salaam: Wildlife Division and Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ).

**Ministry of Natural Resources and Tourism.** 2007. The Wildlife Policy of Tanzania, Revised March 2007. Dar es Salaam: Government Printer.

**Ministry of Natural Resources and Tourism.** 2002. The Wildlife Conservation (Wildlife Management Areas) Regulations. Dar es Salaam: Government Printer.

**Ministry of Natural Resources and Tourism.** 1998. The Wildlife Policy of Tanzania. Dar es Salaam: Government Printer.

**Ministry of Natural Resources and Tourism.** 1998. The National Forest Policy. Dar es Salaam: Government Printer.

**Ministry of Natural Resources and Tourism.** 1995. Policy and Management Plan for Tourist Hunting. Dar es Salaam: Government Printer.

**Namibian Association of CBNRM Support Organisations (NACSO).** 2007. Namibia's Communal Conservancies: A Review of Progress in 2006. Windhoek: NACSO.

**Nelson, F. 2008.** Translinks Case Study: Developing Alternative Frameworks for Community-based Conservation: Piloting Payments for Environmental Services (PES) in Tanzania's Simanjiro Plains. Report prepared for Wildlife Conservation Society.

**Nelson, F. 2007.** Emergent or Illusory? Community Wildlife Management in Tanzania. Drylands Issue Paper No. 146. London: International Institute for Environment and Development (IIED).

**Nelson, F.** 2004. The Evolution and Impacts of Community-based Ecotourism in Northern Tanzania. Drylands Issue Paper No. 131. London: International Institute for Environment and Development (IIED).

**Sachedina, H.** 2006. Conservation, land rights and livelihoods in the Tarangire Ecosystem of Tanzania: Increasing incentives for non-conservation compatible land use change through conservation policy. Paper presented to: Pastoralism and Poverty Reduction in East Africa: A Policy Research Conference, Nairobi.

**Sumba, D., Warinywa, F., Lenaiyasa, P., and Muruthi, P.,** 2007. Koija starbeds ecolodge: A case study of a conservation entreprise in Kenya. African Wildlife Foundation: AWF Working Papers.

**Tanzania Natural Resource Forum (TNRF).** 2008. (Jumuiko la Maliasili), Wildlife for all Tanzanians: Stopping the loss, nurturing the resource and widening the benefits. An information pack and policy recommendations. Also at www.tnrf.org

**United Republic of Tanzania.** The Wildlife Conservation Act, 1974. Dar es Salaam: Government Printer.

**Wildlife Sector Review Task Force.** 1995. A Review of the Wildlife Sector in Tanzania. Volume 2: Possible Future Options. Dar es Salaam: Ministry of Tourism, Natural Resources and Environment.

# Viambatanisho

# Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs): manufaa, changamoto na hatua za kuanzisha



Wanyamapori wanaweza kuhatarisha maisha ya jamii na binadamu – au wakawa hazina kubwa ya asili. Kama unajaribu kulima au kufuga, tembo na simba wanaweza kusababisha uharibifu. Lakini kama uko radhi kukubali mabadiliko na kufanya juhudi za makusudi, wanyama hao hao wanaweza kuwa kivutio cha kipato, ajira na kukuunganisha na ulimwengu.

Mahali ambapo wanyamapori bado wanarandaranda kwa idadi kubwa, serikali zinaruhusu jamii kuanzisha hifadhi za wanyamapori – hususan kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi za taifa au hifadhi nyingine, na kwenye ushoroba (njia maalum za wanyama) ambapo wanyama wanasafiri kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta chakula, maji na wenza.

## KWA NINI KUWE NA JUMUIYA ZA HIFADHI ZA WANYAMAPORI (WMAS)?

WMAs zipo kwa ajili ya kazi mbili. Zinaendeleza urithi wa kipekee wa Afrika wa wanyama wa porini – urithi unaowavuta mamilioni ya watu kutoka maeneo mbalimbali ya ulimwengu kila mwaka.

Pili, zinaruhusu jamii kutoza pesa kutoka kwa wageni hao kwa kuja kuangalia wanyama na /au kukaa kwenye ardhi yao. Mwanzoni, karibu mapato yote kutoka kwa wageni yalikuwa yanaenda moja kwa moja kwa waendeshaji wa shughuli za kitalii – mara nyingi ni wa nje ya nchi – na serikali.

Kila nchi ina majina tofauti, sheria na sera, majina ya maeneo ya hifadhi yanayomilikiwa na jamii. Wengine kama Namibia, wanakubali asilimia 100 ya faida kubaki katika jamii. Kenya inaruhusu jamii kubaki na mapato yote, kasoro kodi inayotokana na matumizi yasiyoathiri wingi wa wanyamapori kwenye ardhi yao.

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 ya Tanzania inasema kuwa WMAs zitahakikisha kuwa "jamii itakuwa na mamlaka yote ya kusimamia na kupata manufaa kutokana na juhudi zao za uhifadhi," ingawa umiliki wa rasilimali-wanyamapori unabaki kwa serikali. Hata hivyo kanuni za WMA za mwaka 2002 zinaeleza kuwa mgawanyo wa manufaa utaelezwa 'na



*Nyumbu wakihama*

# Utangulizi





*Wanyamapori wanavutia utalii*

waraka utakaokuwa ukitolewa mara kwa mara'. Waraka wa hivi karibuni unaeleza kuwa mapato yatokanayo na shughuli za uhifadhi yaende moja kwa moja kwa Serikali, ambayo itarudisha asilimia fulani vijijini.

## UMUHIMU WA SURA HII*

Kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) kunatakiwa kuwa ni juhudi zinazoongozwa na jamii yenyewe. Mchakato wake unapaswa kuwa wazi na kushirikisha jamii yote ili maoni ya wadau wote yazingatiwe.

Mchakato, vile vile, huchukua muda mrefu, una ukiritimba na ni wenye gharama kubwa. Inaelekea jamii peke yake haiwezi kuufanikisha mchakato bila kupata kutoka nje ya jamii hiyo ushauri wa kitaalam, pia uwezeshwaji wa kitaalam na kifedha.

Sura hii imeundwa hasa kusaidia wanajamii na viongozi kujua nini cha kutarajia kutokana na mchakato na matokeo yake. Haitumiki badala ya mwongozo wa serikali lakini inaruhusu jamii kufuatilia mwongozo kwa urahisi zaidi na kuuelewa vyema.

Mahitaji ya kila nchi yanatofautiana na mwongozo ulioambatanishwa kwenye sura hii ni wa Tanzania. Hata hivyo, ushauri kwa ajili ya mipango shirikishi na shughuli nyingine bado vinaweza kuwa na maana kwa jamii nyingi zenye wanyamapori wengi katika Afrika Mashariki na Kusini.

## NJIA YA KUFUATA UKITAKA KUUNDA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI (WMA)

Mchakato unaipitisha jamii kwenye hatua kuu 7 zifuatazo:

1. Kuhamasisha jamii kuhusiana na wanyamapori, matumizi ya ardhi na haki za msingi.
2. Kukubaliana kupitia mkutano mkuu wa kijiji ili kuweza kuendelea na zoezi.
3. Kundaa mpango wa matumizi ya ardhi na kutenga maeneo kwa ajili ya WMA.
4. Kusajili kisheria asasi ya kijamii (CBO) ili iweze kutambulika kisheria kama asasi yenye mamlaka ya kusimamia WMA hiyo.
5. Kutangazwa kisheria kwa WMA hiyo na kupata haki za kisheria juu ya wanyamapori.
6. Kushirikiana na mwekezaji ili kuanzisha mradi wa biashara wa kijamii.
7. Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa WMA hiyo.

*NGUMU LAKINI YENYE THAMANI*

***Mchakato ni mrefu na wa kuchosha. Lakini WMA ndio mfumo pekee ulioko Tanzania kwa sasa, unaowezesha jamii kupata mamlaka ya kisheria juu ya rasilimali za wanyamapori. Siyo umiliki wa asilimia 100, lakini uwezo wa kuamua na kutumia rasilimali ya wanyamapori kwa manufaa yao ..... Mwanzoni watu walifikiri WMA ni kama mtego wa kuchukua ardhi yao. Lakini ukweli ni kinyume cha walivyofikiri.***

*Steven Kiruswa,*
*Mkurugenzi wa Maasai Steppe Heartland*
*African Wildlife Foundation, Arusha*

* Idara ya Wanyamapori ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania imeandaa *kitini cha kufuata wakati wa Kutekeleza Mwongozo wa Kuunda na Kusimamia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) nchini Tanzania.* Sura hii inalenga hatua muhimu kwa ajili ya jamii, lakini hairudii kitini. Kwa masuala kama ya maofisa gani wa kushirikisha, na jinsi gani ya kuweka kumbukumbu ya mipango, jinsi ya kuomba vibali, hakikisha kutazama kitini na kuwasiliana na mamlaka zinazohusika na wanyamapori.

## KUUNDA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI (WMA): HATUA ZA MSINGI

### Hatua ya kwanza: Uhamasishaji na kujitayarisha

Kwa kuwa WMAs zitakuwa kwenye ardhi ya kijiji kumilikiwa kwa pamoja kupitia kijiji, wajumbe wote wa kijiji lazima wakubali au "kufikia muafaka" kwamba wangependa kuendelea na hatua zinazofuata. Ili kuweza kufanya maamuzi ya busara, watu wanahitaji wajue kwa undani taarifa zote kuhusiana na nini maana ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA), gharama na manufaa kuhusiana na kuiunda, na hatua za kisheria za kufuata wakati wa kuunda WMA.

Katika hatua ya kwanza, timu ya uhamasishaji inafanya kazi na jamii ili kutoa taarifa hizi na kujibu maswali na dukuduku kutoka kwa jamii. Timu hii inaweza kujumuisha wafanyakazi kutoka Idara ya Wanyamapori, Halmashauri ya Wilaya na taasisi nyingine za serikali. Zaidi ya hao, asasi isiyo ya kiserikali (NGO) inaweza kuongezeka pamoja na asasi ya kijamii (CBO), au mshauri wa kitaalam anaweza kusaidia uhamasishaji na hatua zinazofuata za mchakato.

*KITUNZE KIDUMU.....*

*Nataka watu wajue kuwa kama mtu asipowahifadhi vizuri wanyamapori, na maliasili nyinginezo, zitapotea. Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) zinatoa nafasi kwa watu kulinda vitu hivi – miti, inayohifadhi maji chini ya ardhi na kuruhusu mito kuendelea kutiririka; malisho yanayowezesha mifugo yetu kuishi; udongo unaowezesha nyasi kuwepo. Na wanyama wa porini – ambao kama rasilimali hizi zikitumika kwa busara, zinaweza kukuletea manufaa dhahiri.*

*Seraphino Bichabicha Mawanja*
*Ofisa Wanyamapori wa Wilaya*
*Wilaya Monduli, Tanzania*

### Hatua ya pili: Kukubaliana kuendelea hatua inayofuata

Elimu ya msingi juu ya faida, hasara, na utaratibu wa kuunda WMA utasaidia wanajamii kuamua kama wanakubali kuendelea au la.

Halmashauri ya kijiji inapendekeza kuwa WMA zianzishwe katika maeneo maalum, lakini jamii ni lazima ikubaliane na kufikia muafaka (kupitia mkutano mkuu) ili kusonga mbele. Ni muhimu kuwa watu wote wenye uwezo wa kupiga kura – watu wazima kutoka vijiji vyote vinavyohusika – wawe wanaelewa vizuri juu ya WMA itakachomaanisha na wakubali kutoa ushirikiano wakati wa kutenga maeneo na mahitaji mengine.

*SIKU ZOTE TUMEKUWA TUKISIMAMIA ARDHI*

*"Usimamizi wa ardhi siyo wazo jipya. Wamasai kwa kijadi, kwa mfano, siku zote wamekuwa wakitumia mfumo wa usimamizi wa ardhi. Walikuwa wanalisha mifugo yao kwa mzunguko: mabondeni wakati wa masika, na milimani wakati wa kiangazi. Kwa njia hiyo maeneo yote yanarudi katika hali yake.*

*Kwa nyongeza, kila mpiganaji – morani – angeweza kukwambia miti ya asili na wangeilinda kama inatumika kwa ajili ya dawa. Kwa jadi yao Wamasai wanakata miti pale tu wanapotaka kujenga boma hivyo miti ingeoteana upya. Sasa, kwa sababu idadi ya watu inaongezeka, hakuna tena fursa kubwa ya kuhama na watu wanakata miti kiholela. Zoezi la kupanga na kuanzisha WMA linasaidia kila mtu kufikia muafaka kuwa manufaa yatakuwa kwa watu, ardhi, mifugo na wanyamapori pia".*

*Enock Chengullah,*
*Ofisa Wanyamapori*
*Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF)*

### Hatua ya tatu: Kuunda asasi ya kijamii (CBO) na Chama kinachotambuliwa kisheria

Kwa kuwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) nyingi zitaundwa kwenye ardhi ya vijiji viwili au zaidi, kila kijiji kinachagua wawakilishi kwenye asasi ya kijamii (CBO) inayojumuisha vijiji hivyo. CBO hii sasa inaandaa rasimu ya katiba na kutayarisha mpango mkakati kwa ajili ya WMA.

Katiba ya asasi hiyo itaongelea wajibu na majukumu, usimamizi wa fedha, na njia za kutatua migogoro.

Mpango mkakati utajumuisha:

- dira ya wanajamii kwenye WMA
- jinsi dira itakavyofikiwa – malengo na shughuli; na
- jinsi WMA itakavyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini.

Itakapokuwa imesajiliwa na serikali, asasi hii itakuwa chama kinachotambulika kisheria, chenye mamlaka ya kuisimamia WMA na wanyamapori wake.

### Hatua ya nne: Mpango wa Matumizi ya Ardhi na kutenga maeneo kwa ajili ya WMA

Kupanga ni muhimu sana ili kufanikisha WMA. Angalia Sura ya 2 kwa kanuni za kijamii za mpango wa matumizi ya ardhi.

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Ili kupunguza mkanganyiko, haya ndiyo maswali yanayoulizwa mara kwa mara juu ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA)

**Nini hasa maana ya WMA?**

Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) ni eneo kwenye ardhi ya kijiji/vijiji yaliyokubalika na kutengwa na kijiji kimoja au zaidi kwa misingi ya kuhifadhi wanyamapori na kwa ajili ya biashara inayotokana na uhifadhi huo. Kama vijiji jirani vimeunda WMA

- vinakubaliana kusaidiana kulinda rasilimali ya wanyamapori;
- vina haki ya kuanzisha biashara au kuingia mkataba na watu wengine ili kuanzisha biashara inayohusiana na wanyamapori (mfano miundombinu ya utalii); na
- vinapata mapato kutokana na biashara hiyo na kuamua kwa pamoja jinsi gani ya kuyagawana na kuyatumia.

Jamii inakubaliana juu ya maeneo yaliyotengwa ndani ya WMA ambayo yataruhusu

- kutumika kwa malisho ya mifugo wakati wa kiangazi na wanyamapori;
- biashara zinazohusiana na wanyama wa porini (kama hoteli ya kitalii); na
- matumizi mengine ikiwemo makazi yaliyopo na shughuli za kilimo.

**Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) SIYO ..............**

WMA **SIYO** eneo la kijiji la malisho ya mifugo au kilimo kwa mwaka mzima, ingawa kunaweza kuwa na maeneo ndani ya WMA kwa matumizi hayo.

Muhimu, pia, WMA **SIYO** Hifadhi ya Taifa. Wala SIYO muendelezo wa Hifadhi ya Taifa, Hifadhi ya Taifa kwa siku za usoni, hifadhi ya Wilaya, au hifadhi inayomilikiwa na mtu binafsi. Vijiji vinaweza kutoa leseni kwa wawekezaji binafsi ili kujenga miundombinu ama kuendesha shughuli zao ndani ya maeneo ya WMA (mfano kujenga kambi, kuendesha uwindaji wa usiku). Lakini jamii lazima ikubali juu ya maeneo hayo na shughuli hizo, na ipate sehemu ya mapato kutokana na shughuli hizo na ikiwezekana ipate manufaa mengine kama ajira.

**Kwa nini tuhamasishe wanyamapori kuongezeka wakati wanatuingilia?**

- Jamii inaweza kupata fedha nyingi kutokana na biashara katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) na WMA inaweza kufanya jamii kuwa na mvuto mkubwa kwenye biashara hizo.
- Jumuiya za Hifadhi za wanyamapori (WMA) ni njia pekee ambayo sheria inaruhusu jamii kupata mapato kutokana na wanyamapori nchini Tanzania.
- Mfumo wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) unawapa wana jamii fursa ya kupanga, kusimamia na kunufaika kutokana na ardhi yao.
- Mchakato wa kupanga na kusimamia Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) unawaongezea wanajamii namna nyingine ya kutatua migogoro, kama vile juu ya matumizi ya ardhi na maji, moto kichaa, uvunaji wa maliasili, na wanyamapori.
- Vijiji vinajivunia kuhifadhi urithi ambao haupatikani mahali pengine duniani.

**Je kukubali kuunda Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) kunamaanisha vijiji vinapoteza ardhi yao?**

Hapana. Ukweli ni kwamba unaweza kuunda Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) pale tu kama kijiji kimesajiliwa kisheria na WMA kama imesajiliwa pia.

Hata hivyo, kama mmeamua kuendelea na hatua inayofuata, ni vyema mkubaliane juu ya shughuli mtakazokuwanazo, au ambazo hamtazifanya, katika maeneo fulani fulani ya WMA. Kwa mfano, wanajamii wanakubaliana kuwa wakazi hawatakuwa wanalisha mifugo katika baadhi ya maeneo ndani ya WMA, angalau kwa kipindi fulani cha mwaka.

Kukubaliana juu ya maeneo yaliyotengwa kutokuwa malisho ya mifugo kunapunguza uwezekano wa kuwepo migogoro baina ya binadamu na wanyamapori, pia inaruhusu wanyamapori kuzaliana, na inaongeza maeneo yanayoweza kuwa ya kuvutia kwa wageni.

**Je manufaa yote yatakwenda serikalini?**

Hapana. Kwa sasa wawekezaji wanatakiwa kuilipa serikali ambayo itarudisha sehemu ya malipo hayo kijijini. Utaratibu huu unaendelea kujadiliwa na wengi wanatumaini kuwa sera hii itabadilika ili wawekezaji wavilipe vijiji moja kwa moja.

**Kwa nini hadi hivi sasa WMA ni chache sana?**

Dhana ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA)

*(inaendelea)*

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA (inaendelea)

bado ni ngeni hapa Tanzania. Sera ya wanyamapori ya Tanzania ya mwaka 1998 inaziruhusu lakini kanuni na miongozo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) haikuwa imetolewa hadi mwaka 2002.

Zaidi ya hivyo, mchakatao wa kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) si kitu ambacho wanajamii wanaweza kufanya kwa urahisi, haraka au wenyewe.

Mwaka 2002, serikali ya Tanzania ilipitisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) za majaribio 16. Hadi Septemba 2008, 10 zilikuwa zimepitishwa kisheria (kulingana na TNRF).

Lakini jamii ambazo zilivutiwa na kuanzisha WMA na biashara zinazohusiana na uhifadhi zinaeleza manufaa makubwa na kuridhika.

**Je wanachama wa WMA wanaweza kusimamia uwindaji?**

Kwa wakati huu, serikali kuu, na siyo jamii, ndiyo inayotoa leseni za uwindaji kwa wakazi na watalii. Licha ya hivyo, kwa kuwa WMA nyingi ziko ndani ya vitalu vya uwindaji, kumekuwa na migogoro kati ya makampuni ya uwindaji na wawekezaji ndani ya WMA ambao wanafanya safari zisizo na uwindaji. Hadi sasa vibali vya vitalu vya uwindaji vinaishia mwishoni mwa mwaka 2009. Wengi wanaona kama kufutwa kwa vitalu vya uwindaji kutatoa fursa kwa jamii kusimamia kikamilifu na kunufaika na uwindaji wa vijijini. Mjadala juu ya suala hili hakika utaendelea.

Mwishoni mwa miaka ya 1990, vijiji 19 vilivyo kwenye mradi wa Matumizi Bora ya Maliasili Idodi na Pawaga (MBOMIPA), ulioko karibu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, vilikubaliwa na Idara ya Wanyamapori kuuza leseni kwa wawindaji wakazi. Mradi wa MBOMIPA uliuza kota za kuwinda. Mwaka 1997, walianza kuuza kwenye minada kwa bei ya juu zaidi, kipato kiliongezeka kutoka karibu milioni 5 mwaka 1996 hadi zaidi ya milioni 20 mwaka 2003 (karibu dola za kimarekani 1,000 kwa kila kijiji).

**WMA inaundwaje?**

Kusaidia jamii kuelewa vipengele muhimu vinavyoongelewa hapo juu na wao kuamua kama waendelee mbele ndiyo mwanzo.

Hatua zinazofuata zinajumuisha kuunda timu ya mipango ambayo ina wakazi na wawezeshaji; kuunda asasi ya kijamii; kuisajili kisheria kwa kufuata taratibu za nchi. Timu ya mipango itaandaa taarifa mbalimbali juu ya matumizi ya sasa na manufaa yanayoweza kupatikana kwa kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA), kutafuta maoni mbalimbali kutoka kwa wanajamii juu ya hofu zao na malengo ya WMA, kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wa serikali na wasio wa serikali, kuandaa taarifa ya athari za kimazingira, na kuandaa Mpango wa Jumla wa Usimamizi, au Mpango wa Usimamizi wa rasilimali katika eneo lililotengwa kwa ajili ya WMA.

Kwa kufanya hivyo, timu hiyo na wataalam wa nje watahitajika kufuata kanuni za hifadhi za wanyamapori (Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA)) ya mwaka 2002 na mwongozo wa Kuunda na Kusimamia Maeneo ya Usimamizi wa Wanyamapori ya mwaka 2002.

**Ni lazima jamii kuunda WMA ili kuwa na mradi wa kijamii (CBV)?**

Hapana. Mnaweza kuingia mkataba mzuri na mwekezaji bila kuwa na WMA, ingawa kutakuwa na faida nyingi kisheria kama kungekuwa na WMA. Moja kati ya faida kuu ni kuwa na uwezekano wa ama kuzuia au kuteka mapato yanayotokana na uwindaji, ingawa pia faida hii inaweza kuwa na walakini kwa wakati huu. Faida nyingine ni kuwa kampuni za kitalii zitakazokuwa zinavutiwa zaidi kwenye maeneo yenye hali nzuri, yenye wanyamapori wengi – na WMA zitasaidia kuhakikisha kuwepo kwa ubora wa mandhari na hali ya wanyamapori.

Hata hivyo, watafiti wanataja kijiji cha Ololosokwan kilicho katika Wilaya ya Loliondo kuwa kijiji kilichofanikiwa sana kwenye kuzalisha kipato kwa jamii kinachotokana na wanyamapori nchini Tanzania, na hakiko kwenye WMA. Nyumba za wageni na kambi zinazoendeshwa vizuri na kijiji zinaiingizia jamii kijijini Ololosokwan zaidi ya dola za kimarekani 55,000 kwa mwaka kwa kukodi na gharama za kulala, pamoja na kutoa ajira kwa ma-skauti wa wanyamapori. Kwa ujumla wao vijiji 7 katika wilaya ya Loliondo vinavuna dola za kimarenai 300,000 kwa mwaka bila kuwa na WMA (Nelson 2007).

Kupanga kwa ajili ya WMA ya wanajamii kunafanana, ingawa kunaweza kushirikisha watu wengi zaidi kuliko inavyokuwa wakati wa kupanga kwenye ngazi ya kijiji kwa sababu WMA zinahusisha vijiji vingi zaidi kwa wakati mmoja. Pia vijiji vinavyohusika vitatayarisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Pamoja.

Kwa kushauriana na jamii, CBO iliyoundwa itaandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi pamoja na

- Mpango wa Jumla wa Usimamizi au Mpango wa Usimamizi wa rasilimali katika eneo lililotengwa kwa ajili ya WMA, na
- Taarifa ya athari za kimazingira juu ya jinsi gani shughuli zilizopendekezwa zitaathiri ardhi, maji, wanyamapori na rasilimali nyingine.

Nyaraka hizi zinaelezea shughuli zipi au maendeleo aina gani watu wanaweza kufanya katika maeneo mbalimbali ya WMA na kwa nini. Mipango yote ya matumizi ya ardhi ni lazima ipimwe kitaalamu na kusajiriwa kisheria.

*UHIFADHI DHIDI YA KILIMO*

***"Kama tukihifadhi ardhi yetu kwa ajili ya miti na mimea mingine, na wanyamapori: tutapata kuni, mvua na kuhifadhi maji kwenye udongo ambavyo pia vinatakiwa kwa ajili ya malisho ya mifugo wakati wa kiangazi. Kama ukiwapa ardhi hiyo watu binafsi kuifanya mashamba ya kilimo unafikiri utapata nyasi tena?"***

*Noah Teveli*
*Msemaji wa WMA ya Burunge*

## Hatua ya tano: Kutangazwa rasmi na kupata haki za kisheria juu ya wanyamapori

Kwa kulingana na mipango mbalimbali asasi hii itakayokuwa na mamlaka kisheria itaandika barua ya maombi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kuitangaza kisheria WMA.

Halafu asasi hii ni lazima pia iombe kupewa haki ya kutumia rasilimali za wanyamapori.

Utambuzi huu wa kisheria ni muhimu kwa sababu ni hatua muhimu itakayohakikisha kuwa kuna manufaa yanayotokana na hifadhi ya wanyamapori. Manufaa yana wigo mpana kuanzia kuni za kupikia hadi kumiliki biashara zinazohusiana na uhifadhi (Jedwali namba 1).

*MANUFAA KATIKA WMA YA BURUNGE*

***WMA ya Burunge inaweka mazingira mazuri, hii inavutia wanyama wa porini pamoja na wawekezaji. Uundaji wa aina hii wa WMA utaleta uhifadhi wa muda mrefu wa mazingira na wa kupata kipato. WMA inapata mwekezaji kwa ajili ya kila mtu. Katika mwaka wa kwanza wa Burunge, vijiji vilivyoko kwenye WMA vilipata milioni 34 (fedha za kitanzania). Mwaka wa pili zilipatikana milioni 76.***

*Noah Teveli,*
*Msemaji wa WMA ya Burunge*

## Hatua ya sita: Kuanzisha biashara inayohusiana na uhifadhi (CBV)

Sasa wanajamii wanaweza kuanzisha mradi unaohusiana na uhifadhi (pia unajulikana kama "biashara inayohusiana na wanyamapori" au "mradi wa uhifadhi"), ambao umo ndani ya WMA au inatumia rasilimali iliyomo kwenye WMA. Mfano ni njia asilia, kambi za uvuvi, mizinga ya nyuki, haki ya kutalii kwa ajili ya safari za kupiga picha au utalii wa utamaduni.

Biashara au miradi ya jamii inayohusiana na uhifadhi mara nyingi ni ya ubia au kuungana baina ya jamii na mwekezaji binafsi. Mwekezaji anatoa mtaji, utaalam wa biashara, mafunzo kazini na ajira kwa ruhusa ya kumkubalia kutumia ardhi ya WMA.

Sura ya 3 inatoa maelezo kiundani juu ya kuchagua, kujadiliana na kugawana manufaa kutokana na biashara au miradi inayouhusiana na uhifadhi.

## Hatua ya saba: Ufuatiliaji wa mara kwa mara

Wakati wa mchakato wa kuundwa, Bodi ya Wadhamini pamoja na kamati kadhaa na maafisa wa Asasi ya Kisheria watakuwa wamekwishachaguliwa. Maofisa hao wataendelea kufanya kazi ya ufuatiliaji wa WMA, kuhakikisha kuwa mipango inatekelezwa na kanda zilizotengwa zinaheshimiwa, na kuweka wanajamii na wanyamapori katika usalama. Mfano wa hizo kamati ni kama kamati ya utendaji, ya fedha, ya mipango, ya mazingira, na ya usalama. Kila kitu kinawekwa sawa kwa wanajamii na mamlaka ya vijiji ili usimamizi ubaki kuwa wa uwazi.

Askari/skauti wa wanyamapori kutoka katika jamii, ambao kwa kawaida wanapewa mafunzo na kulipwa na wawekezaji, ndio wanaosimamia usalama na kutoa taarifa za wawindaji haramu na wahalifu wengine (kisanduku namba 1).

*TUNAONA THAMANI IMEONGEZEKA*

***"Ujangili ulikuwa tatizo kubwa katika Enduimet. Lakini tangu tuwe na WMA kiwango cha ujangili kimeshuka kwa asilimia 20-30. Hapo zamani, kama majangili wangeonekana, hakuna mtu ambaye angejishughulisha na kufanya lolote. Kwa sasa, wanakijiji wengi, wakisikia tu kuhusu majangili, wanawafuatilia wenyewe.
Kuna matukio ambapo nyara zinakusanywa na wanavijiji na kuletwa kwenye ofisi ili zichukuliwe na Idara ya Wanyamapori. Hii inanifanya kufikiria kuwa sasa watu wanapenda uhifadhi kuliko ilivyokuwa zamani***

*Joseph Lendiy*
*Katibu wa kuteuliwa, WMA ya Enduimet"*

JEDWALI NAMBA 1: FURSA NA UDHAIFU, KAMA ILIVYOONEKANA NA WANAJAMII NA MAOFISA, KWENYE MPANGO WA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA KANDA ILIYOTENGWA KATIKA WMA YA LOLKISALE

| UMAHIRI/FURSA | OLKONONOI (Njia ya wanyamapori) | EMBARNETI (Makazi ya kudumu) | RONJOO (Kiangazi cha muda mrefu) |
|---|---|---|---|
| Uokotaji wa kuni za kupikia kutoka kwenye miti iliyokauka | ✓ | | ✓ |
| Utalii au safari za kuangalia wanyama na kuwapiga picha | ✓ | ✓ | ✓ |
| Utafiti | ✓ | ✓ | ✓ |
| Ufugaji wa nyuki | ✓ | ✓ | ✓ |
| Kuchunga ng'ombe na uhifadhi wa wanyamapori | ✓ | ✓ | ✓ |
| Mabwawa ya maji (kwa ajili ya mifugo na wanyamapori) | ✓ | | |
| Elimu na mafunzo | ✓ | | |
| Njia asilia (kuzifuatilia) | ✓ | | ✓ |
| Ufugaji wa minyoo ya silica | ✓ | | |
| Mabango ya wawindaji | ✓ | | ✓ |
| Ukusanyaji wa mbegu | ✓ | | ✓ |
| Matumizi ya jumla | | | |
| Kambi za muda mfupi | | | ✓ |
| Hoteli/nyumba za wageni | | | ✓ |
| Kambi za kudumu za maturubai | | | ✓ |
| Uchimbaji wa mchanga mitoni | | | ✓ |
| Uvuvi | | ✓ | ✓ |
| Sehemu za kufanyia sherehe/starehe | | ✓ | ✓ |
| Kambi za michezo ya kuruka au kupaa angani | | | ✓ |
| Kilimo | | ✓ | |
| Uendeshaji magari ndani ya hifadhi | | ✓ | |

| UDHAIFU | Sababu zilizofanya WMA ya Lolkisale na RZMP kufanikiwa |
|---|---|
| 1. Kupita kwa magari yanayosomba changarawe kwenye WMA | 1. Ujuzi wa ujasiliamali |
| 2. Ujuzi mdogo kwa jamii kuhusiana na usimamizi wa maliasili | 2. Miradi ya kuongeza kipato |
| 3. Kutokuwa makini katika kutekeleza sheria | 3. Uwekezaji katika makambi, hoteli na nyumba za kulala wageni |
| 4. Ujangili kwa ajili ya chakula | 4. Kuendeleza na upatikanaji wa masoko |
| 5. Uhifadhi mdogo wa mazingira | 5. Uendelezaji wa ranchi ndogo kwa ajili ya mifugo iliyoboreshwa |
| | 6. Utengenezaji wa kiwanja kidogo cha ndege |
| | 7. Kuwepo kwa kituo cha mafunzo ya utamaduni |
| | 8. Mafunzo kwa viongozi wapya na waliopo |
| | 9. Kufanyika kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara na kufanyika kwa tathmini zinapohitajika |
| | 10. Miundo mbinu na rasilimali |
| | 11. Maji |
| | 12. Njia za usafiri |
| | 13. Ofisi na vitendea kazi |

# Hatua kuelekea mafanikio



### KISANDUKU NAMBA 1: WAJIBU MKUU WA ASKARI WA WANYAMAPORII

Askari wa wanyamapori wanawajibu mkubwa katika WMA na biashara zinazohusiana na asili:

- Wanalinda ardhi ya jamii na wanyamapori dhidi ya wawindaji haramu, ukataji miti kiholela, uchungaji au ujenzi katika maeneo yasiyoruhusiwa, na uvamizi kutoka vijiji vingine.
- Wanasaidia vijiji kutekeleza shughuli za kanda kama wanachama wake wanavyokubaliana. Wanalinda dhidi ya/kutoa taarifa za migogoro kati ya binadamu na wanyamapori.
- Wanatoa ulinzi kwa wanavijiji.
- Wanasaidia kutunza rasilimali na biashara ambazo jamii inategemea zibaki katika hali nzuri.
- Wataalam wanashauri kwamba timu za askari wanyamapori hufanya vizuri kama:
  - Wanajiona kama ni sehemu ya biashara - wao wakiwa katika Idara ya Usalama.
  - Kama wamepewa mafunzo madhubuti ya kutatua migogoro; uokoaji katika matukio ya hatari; ukusanyaji wa taarifa, na ujuzi wa kutumia vifaa vya kisasa vya kupata taarifa za kijiografia (kujua mahali na usawa wake - GPS) na mafunzo ya mara kwa mara.
  - Wana vifaa vya mawasiliano kama redio za upepo, simu za mkononi, na GPS.
  - Wanasimamiwa na wana kambi.
  - Wanawajibika kwa askari wa wanyamapori wa kijiji au maofisa wengine.
  - Kama ni sehemu ya biashara inayohusiana na uhifadhi, wameajiriwa na kulipwa na mwekezaji, kutokana na mapato ya biashara hiyo.

Mambo ya kuzingatia zaidi ni uwezekano wa kutokuwa na migogoro na wanajamii, kwa sababu maaskari wanyamapori wanatoka miongoni mwa jamii hiyo na wangehitaji kuchukua hatua dhidi ya marafiki au ndugu zao.

*"Linaloweza kutokea ni kuwa, tuseme jamii inapata hundi yake ya kwanza ya malipo mwezi Januari - na fedha zote ziwe zimetumika kufikia mwezi Mei. Binadamu wanasahau haraka. Mwezi Juni ni rahisi kufikiria, 'hatupati faida yoyote kutokana na hii WMA. Tunaweza hata kuiachia mifugo yetu ikachungiwa popote.' Hapa ni kazi ya askari wa wanyamapori kutoa mifugo ndani ya ukanda usioruhusiwa kuchungiwa, na kuwakumbusha watu kuhusu makubaliano."*

*Ben Mwongela*
*Msimamizi, Huduma za Ujasiliamali*
*AWF-Kenya*

## JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI YA BURUNGE

WMA ya Burunge ni moja kati ya WMA za majaribio za kwanza.

Eneo lina vijiji 9, na karibu wakazi 45,000 na njia kuu ya maelfu ya wanyamapori wanaosafiri kati ya ziwa Manyara na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Sio kila mtu alifurahia wazo la kuanzishwa kwa WMA (angalia Sura ya 5 juu ya Migogoro). Mfuko wa Taasisi ya Wanyamapori Afrika (AWF), asasi isiyo ya kiserikali (NGO) iliyofanya uwezeshaji, ilianza kwa kuelimisha, ikihusisha wajumbe muhimu wa vijiji vyote 9 na kuendesha semina vijijini juu ya faida zilizopo wakihifadhi wanyamapori na kuendeleza eneo lao kama eneo muhimu la utalii.

Baada ya mikutano mingi na miaka kadhaa ya kufuatilia matakwa ya ukiritimba, WMA ya Burunge ilitangazwa rasmi na kupewa haki ya kutumia wanyamapori.

Vijiji vilikubaliana kuhamisha eneo la makazi, na mifugo mbali na njia za kusafiria wanyamapori ili kupunguza migogoro kati ya wanyama na binadamu. Walianzisha maeneo mengine ya kuchungia kipindi cha mwaka mzima na wakati wa kiangazi.

Hivi leo WMA ya Burunge inapata karibu dola za kimarekani 230,000 kwa mwaka kutoka hoteli za kitalii mbili, Maramboi Tented Lodge na Ziwa Burunge Tented Lodge. Eneo lilikuwa tayari linanufaika lakini mapato yameongezeka. Pia nyumba nyingi za wageni zinajengwa. Fedha hizo zinasaidia miradi ya maendeleo mingi ya kijamii zikiwemo huduma za afya na ujenzi wa shule tatu.

Zaidi ya hivyo, wakazi wamepata ajira katika biashara hizi zinazohusiana na uhifadhi. WMA nayo imeajiri hapo kijijini askari wa wanyamapori zaidi ya 40 na wamepata mafunzo ya kiufundi. Askari hao wanaratibu uzuiaji wa ujangili na ufuatiliaji wa doria, na pia kuchangia katika usalama wa kanda nzima.

Hata hivyo, migogoro inaendelea, na hadi sasa vijiji viwili vimekwishajitoa kwenye WMA, vikidai kuwa havikuafiki kuanzishwa kwa WMA. Majadiliano juu ya hili yanaendelea.

## KIKUNDI CHA WANAWAKE CHA MWADA, BURUNGE

Kikundi cha wanawake cha Mwada kinashughulika na utengenezaji wa vikapu na bidhaa nyingine, wana kibanda kwenye soko ndani ya WMA. Wageni ndani ya WMA ndio wateja wa kikundi, wanapata oda kutoka kwenye mahoteli na biashara nyingine pamoja na maonesho ya kibiashara.

Kabla ya kuundwa kwa kikundi hiki cha kinamama, baadhi ya akinamama walikuwa wanatumia muda wao mwingi kufanya vibarua vigumu mashambani ambavyo vilikuwa na ujira duni.

Wakati baadhi yao walikuwa wanatengeneza vikapu tangu siku za nyuma, mafunzo waliyopewa na AWF yaliwasaidia kuongeza ujuzi na kuwa wabunifu zaidi. Kikapu kingeweza kuuzwa kwa shilingi 1,000 hapo zamani; kwa sasa kikapu hicho kinauzwa kwa shilingi 10,000 za kitanzania au zaidi.

"Vikapu ni vizuri sana, wateja wengine wanapandisha juu bei" anasema Josephine Simons, mwezeshaji wa kikundi kutoka AWF. "Siku moja nilimsikia mwanamke mmoja anasema kwa mshangao: 10,000? Hiyo haitoshi, nitakulipa 15,000!"

Kikundi hicho cha wanachama 30 kinafanya kazi kama Bodi ambayo inawakilisha akinamama wa kijiji cha Mwada. Sehemu ya mapato inakwenda kwenye akiba ya pamoja, sehemu nyingine kwenye kikundi na nyingine kwa wanachama wa kikundi. Akiba ya pamoja inamaanisha kwamba wanakikundi wanaweza wakakopa hapo ili kujisaidia wakipatwa na dharura au karo ya shule kwa watoto.

Fursa ya kupata fedha ina maana sana kwa kaya ngazi ya kijiji. "Wakati mume wa mwanamke mmoja alipofariki, wakwe zake walichukua ardhi yake. Alibaki na nyumba ya manyasi tu na watoto wake watano. Kwa bahati nzuri alikuwa na akiba iliyotokana na mauzo yake ya vikapu. Alikodisha ekari nne kwa ajili ya kupanda mahindi. Baada ya msimu mmoja wa kilimo, na kuendelea kutengeneza vikapu, aliweza kununua ardhi yake - ekari tano katika kijiji cha Mwada".

Kikundi kinaandaa biashara ya ufinyanzi pia.

Sura ya 4

# Hatua kuelekea mafanikio

# Mambo muhimu ya kukumbuka

1 Hatua za kuunda WMA ni ndefu, zenye ukiritimba na ngumu. Makadirio ya gharama za kuianzisha yako kati ya dola za kimarekani 100,000 hadi 250,000 – ni wazi kuwa juhudi za kijiji peke yake hazitoshi bila usaidizi wa kifedha kutoka nje. Hivyo itabidi jamii zianzishe ubia na wawekezaji binafsi na wabia wengine kwa kushirikiana na taasisi zenye wataalam muafaka ili kusaidia utekelezaji wa mchakato huu.

2 Sheria za serikali, sera na kanuni zinapingana hivyo kusababisha mkanganyiko kuhusiana na haki, wajibu na manufaa. Zinabadilika kutokana na jinsi jamii husika itakavyokuwa imepingana au imekubaliana na uhifadhi huo. Lazima jamii zifahamu hali hii na zitapaswa kufuatilia kwa karibu mabadiliko ya kanuni na miongozo.

3 Maeneo ya uwindaji kwa sasa yanapewa kipaumbele kuliko matumizi yasiyoathiri wingi wa wanyamapori, hata kwenye WMA. Uwindaji unasababisha safari za upigaji picha zishindikane na biashara nyingine za uhifadhi pia. Uwindaji unaweza ukafaa zaidi kwenye hifadhi za taifa za ndani zaidi ambako kuna uwezekano mdogo wa matumizi ya utalii usioathiri wanyamapori. Uwindaji ni wa kiwango kikubwa katika maeneo yanayojulikana sana, kama ukanda wa utalii wa kaskazini mwa Tanzania, ambako mapato kutokana na safari za upigaji wa picha yanaweza kuwa makubwa kuliko yale ya uwindaji kwa sababu ya idadi kubwa ya watalii wa kupiga picha.

# Mambo muhimu ya kukumbuka

## FAHARASA

**Baldus, R.D. and Siege L.** 2001. *Experiences with Community Based Wildlife Conservation in Tanzania.* Tanzania Wildlife Discussion Paper No. 29. Dar es Salaam: Wildlife Division and Gesellschaft für Technische Zusammenarbeit (GTZ).

**Bovarnick, A. and Gupta, A.** 2003. *Local Business for Global Biodiversity Conservation: Improving the Design of Small Business Development Strategies in Biodiversity Projects.* New York: United Nations Development Programme.

**Igoe, J. and Croucher, B.** 2007. "Conservation, Commerce, and Communities: the Story of Community-Based Wildlife Management Areas in Tanzania's Northern Tourist Circuit."

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT).** 1998. *The Wildlife Policy of Tanzania.* Dar es Salaam: Government Printer.

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT).** 2001. *Community-based Forest Management Guidelines.* Dar es Salaam, Forestry and Beekeeping Division.

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT).** 2002. *The Wildlife Conservation (Wildlife Management Areas) Regulations.* Dar es Salaam: Government Printer.

**Nelson, F.** 2004. The Evolution and Impacts of Community-based Ecotourism in Northern Tanzania. Drylands Issue Paper No. 131. London: International Institute for Environment and Development (IIED).

**Nelson, F.** 2007. Emergent or Illusory? Community Wildlife Management in Tanzania. Drylands Issue Paper No. 146. London: International Institute for Environment and Development (IIED).

**Sachedina, H.T.,** 2009. *Wildlife is Our Oil: Conservation, Livelihoods and NGOs in the Tarangire Ecosystem, Tanzania.* Doctoral thesis for School of Geography and the Environment, University of Oxford.

**Sosovele, H.** 2005, "Tourism Development and Poverty Reduction Initiatives from Tanzania: Lessons for Practice," presented at the International Institute of Peace for Tourism Conference, 2005.


**Tanzania Natural Resource Forum (TNRF)** 2008. (Jumuiko la Maliasili), Wildlife for all Tanzanians: Stopping the loss, nurturing the resource and widening the benefits. An information pack and policy recommendations. Also at www.tnrf.org

**United Republic of Tanzania.** The Wildlife Conservation Act, 1974. Dar es Salaam: Government Printer.

**United Republic of Tanzania (URT).** 1997. *The National Land Policy, Second Edition,* Ministry of Lands, and Human Settlement Development, Dar es Salaam.

# Viambatanisho

# Migororo katika jamii: kusuluhisha migogoro katika maeneo yenye mifugo, kilimo na wanyamapori



## HADITHI YA VIJIJI VIWILI

*Mwaka 2006, mkulima kutoka Narakauwo Wilayani Simanjiro alianza kupanda mazao na kujenga majumba kwenye eneo lake lenye ekari 60. Punde mkulima kutoka kijiji cha jirani cha Loiborsiret naye aliamua kuliendeleza eneo lake. Lakini aligundua kwamba sehemu ya eneo hilo lilikuwa limeshaendelezwa na mtu kutoka Narakauwo.*

*Wakulima hao wawili wakazungumza. Kila mmoja akatoa cheti cha umiliki alichopewa na Viongozi wa Kijiji. Vijiji vyote viwili vilionekana vimo katika ramani, vimeshapimwa na kusajiliwa mwaka 1978.*

*Mkulima wa Loiborsiret hakuwa radhi kupoteza haki yake hivyo alianza kusafisha eneo la ardhi lililoko ndani ya eneo lenye mgogoro. Punde ndugu, marafiki na viongozi wa vijiji vya pande zote mbili walijihusisha katika hayo majadiliano ambayo yaligeuka kuwa mgogoro wa mipaka ya vijiji. Viongozi wa Loiborsiret waliitisha mkutano na wakaamua kwamba, kulingana na ramani iliyokuwa imesajiliwa, mkulima wao ndiye mmiliki halali wa eneo la ardhi lenye mgogoro. Baada ya hapo wakawafuata viongozi wa Narakauwo na kufanya mkutano wa pamoja uliohusisha wakazi wote.*

### Utafutaji wa taarifa kuhusu ukweli wa suala hilo

Kulifuatia mikutano kadhaa ya majadiliano yaliyohusisha kamati za vijiji kutoka pande zote mbili pamoja na wazee, viongozi wa kimila na wawakilishi kutoka kwenye Asasi isiyo ya Kiserikali inayofanya kazi kwenye hilo eneo.

Majadiliano hayo yalilenga kwenye utafutaji wa taarifa:

- Kulikuwa na hasara au uharibifu gani?
- Nini chanzo cha mgogoro huo?
- Historia yake ikoje?
- Nani mwenye haki juu ya ardhi hiyo, kwa kuwa wote wana hati?
- Eneo hilo ni la kijiji kipi kwa kufuata ramani ipi ya mpaka wa kijiji?

Ramani ziliangaliwa lakini kila upande ulimlaumu mwenzake kwa kushindwa kuzisoma hizo ramani vizuri.

# Utangulizi



### Kualika taasisi au watu walio nje ya mgogoro

Hatimaye wanakijiji walikubali kwamba hizo ramani hazingewasaidia. Wakaamua kuihusisha taasisi nyingine - Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro - ambayo ilipeleka wataalamu ambao waliahidi kutopendelea upande wowote.

Baada ya kuzisoma zile ramani za vijiji kwa kutumia GPS – njia inayotumia kompyuta kupima kwa uhakika maeneo – hiyo timu ya wataalamu ilisema kwamba mamlaka za Narakauwo ndizo zilizopanua mpaka lakini hawakupanua mpaka wa ramani kwenda Loiborsiret kwa makusudi.

Kwa hiyo Kijiji cha Loiborsiret kilishinda mgogoro huo wa ardhi. Vijiji hivyo vilikubaliana:

- kutengua zile hati mbili za wamiliki ardhi za kwanza na kutoa hati mpya za umiliki;
- kumhamisha mkulima wa Narakauwo aliyekuwa wa kwanza kuiendeleza ile ardhi ili awe mwanakijiji wa kijiji cha Loiborsiret;
- kumuomba huyo mkulima kusalimisha nusu ya ardhi yake ya awali kwa mkulima wa pili (ingawa alifidiwa ardhi mahali pengine); na
- kuweka mawe ya mipaka ili kuepuka migogoro siku za usoni.

### Tunachojifunza

- Usuluhishi wa mgogoro ulitegemea utafutaji wa taarifa wa pamoja. Wadau walifanya maamuzi kulingana na taarifa hizo.
- Inaweza kusaidia kuhusisha taasisi au watu walionje ya mgogoro, kutoka ndani au nje ya jamii. Wanaweza kusaidia kufanya utafiti wa kesi pamoja na kuwezesha mazungumzo yenye amani.
- Lengo kuu lilikuwa ni kuendeleza uhusiano uliopo, kwa hiyo vijiji vililenga katika ushirikiano-suluhisho ambalo kila mmoja atanufaika na atakubali, kuliko kujaribu kuthibitisha kwamba mmoja wao ndiye aliyekosea.
- Uaminifu na kusema ukweli ndio ilikuwa muhimu katika kuamua mmiliki halali wa ardhi bila kuharibu uhusiano.



*Wakulima wawili wakibishana juu ya mpaka wa ardhi*



*Wanaogombea ardhi wakisoma ramani, akiwepo mtu mwingine asiyehusika na mgogoro huo*

## UMUHIMU WA SURA HII

Hata tujaribu vipi, hakuna hata mmoja wetu ambaye anaweza kuepuka mgogoro. Iwe mgogoro juu ya mipaka, au baina ya watu na wanyamapori; ndani au baina ya wanafamilia; miongoni mwa vijiji; baina ya biashara au vitengo vya serikali – hata kwa mtu binafsi – mgogoro hauepukiki.

Ingawa inaweza kuwa inaumiza, mwishoni mgogoro unaweza ukasaidia. Mgogoro uliodhibitiwa vizuri kwa kuhusisha kwenye utatuzi wa mgogoro pande zote zinazohusika unaweza:

- kusaidia watu kuelewa maslahi na mahitaji ya wengine;
- kurekebisha au kuimarisha uhusiano kupitia kuelewana na mawasiliano bora na ya mpangilio;
- kusukuma watu kuwaza njia mbalimbali ambazo wasingeweza kuzifikiria; na
- kuleta suluhisho ambapo pande zote mbili zinanufaika – inajulikana kama suluhisho la "wote ni ushindi".

Migogoro mingi inayohusisha watu, mifugo na wanyamapori inatokana na uhaba wa rasilimali – ambayo ni changamoto ya kweli na ngumu. Lakini mvutano mara nyingi hukua kwa sababu watu wana mwelekeo na maadili tofauti, na kushindwa kuelewa mtazamo wa mwenzake. Migogoro mingi inasababishwa

na vyanzo vya undani sana kuliko vile vinavyoonekana dhahiri, na vinafanywa kuwa vigumu zaidi kwa sababu ya hisia za kimaslahi, woga na mahitaji pamoja na maslahi na matakwa ya mtu (kisanduku namba 1).

Kwa kuongezea, majungu au kukosekana kwa mawasiliano kunaweza kuchochea migogoro na kuharibu hata ule uhusiano wa karibu.

Sura hii inaelezea ...

- Mbinu za kawaida za kufanyia kazi migogoro
- Mifumo mikuu ya kitaasisi iliyopo kusaidia jamii kutatua matatizo magumu
- Hatua muhimu za kufikia katika suluhisho la "wote kushinda", ama kwa mazungumzo ya moja kwa moja au kwa kutumia mbinu nyingine. Hatua hizi zinajumuisha jinsi ya kuchanganua mgogoro, kujadiliana, kuongeza uwezekano, kutengeneza makubaliano yenye nguvu na ufuatiliaji.

## MBINU ZA KAWAIDA ZA KUSIMAMIA NA KUDHIBITI MIGOGORO

Kila mtu ana mbinu au namna yake mwenyewe anayopendelea kushughulikia migogoro. Lakini watu na jamii wanaweza kuchagua mbinu ipi watumie, na mbinu nyingine zinaweza kuleta suluhisho za kudumu kuliko zingine.

Hapo chini kuna maelezo mafupi kuhusu mbinu muhimu tano za udhibiti wa migogoro, inayoelezewa kwa mtindo wa hadithi.

### Mbinu kuu tano

**Uepukaji** ni kuepuka matatizo na pengine hata kuwaepuka watu wanaohusika na mgogoro. Kwa kawaida, watu hutumia mbinu ya kuepuka pale ambapo mgogoro unaleta usumbufu au unaonekana kuwa hauna maana. Hii inaweza kufanya kazi ijapokuwa kwa muda, kwenye migogoro midogo. Lakini mbinu ya kuepuka inaweza

### KISANDUKU NAMBA 1: SABABU ZA MIGOGORO KWENYE ENEO LA MRADI

Katika vijiji vya Kaskazini mwa Tanzania karibu na Hifadhi ya Tarangire, ongezeko la idadi ya watu na uhamiaji wa watu kutoka wilaya nyingine imeongeza uhaba wa ardhi na mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka ardhi ya malisho na kuwa ardhi ya kilimo. Migogoro ya ardhi, maji na rasilimali nyingine, baina ya wanyamapori, wafugaji na wakulima inaibuka. Migogoro hii inachochewa na uharibifu wa mazingira na upotevu wa uwezo wa ardhi wa kuzalisha, kuzuiwa kwa njia kuu wanazopita wanyamapori wanapohama na maeneo ya malisho, na ongezeko la ukame na mafuriko kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Sababu za migogoro

1. **Kupanua mashamba na makazi.** Kilimo cha kujikimu na kilimo cha biashara pamoja na maeneo ya biashara yanasogea kwenye maeneo ambayo kwa kawaida yalikuwa ni maeneo ya wafugaji na wanyamapori. Mabadiliko haya yameleta:
   - kiwango kikubwa cha ufyekaji wa msitu na vichaka, yote kwa ajili ya mashamba na mkaa;
   - moto kichaa;
   - uwindaji haramu, kwa ajili ya kujikimu na biashara;
   - kupunguza na kugawa ardhi ya mifugo na makazi ya wanyamapori; na
   - upoteaji wa vyanzo vya kudumu vya maji, mmomonyoko wa udongo, na uharibifu mwingine wa mazingira.
2. **Wanyamapori kuvamia mazao na mifugo.** Asilimia 70 ya wanyamapori wa Tarangire wanakwenda nje ya mipaka ya hifadhi wakati wa masika. Wanyamapori walao majani wanavamia mazao yaliyolimwa na wanyamapori wengine wanaua ng'ombe, mbuzi na kondoo.
3. **Sera na Sheria za rasilimali za ardhi zinazokinzana.** Kwa mfano, sera inayoruhusu Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori inasema jamii ilipwe moja kwa moja na biashara zinazotumia ardhi zao. Lakini mwaka 2007 tangazo la Serikali liliagiza kwamba malipo yafanywe kwa Serikali Kuu, ambayo itarudisha kiasi kwa jamii. Kwa kuongeza, wakati Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori inakusudia kuruhusu jamii kusimamia rasilimali zao wenyewe, mwanzoni mwa mwaka 2009, vibali vya uwindaji vilivyopitishwa na Serikali Kuu viliruhusiwa kwa kiasi kikubwa kuondoa maslahi mengine ambayo jamii ingekuwa nayo kama vile utalii wa kupiga picha.
4. **Kukosekana kwa uwazi na usawa.** Kutokuwa na uwazi kwenye kipato, mapato na ufanyaji maamuzi kuhusiana na faida kutokana na rasilimali inaleta migogoro baina ya wawekezaji, serikali, na jamii, na baina ya viongozi katika jamii na wajumbe. Zaidi ya hayo, wale wanaonufaika kutokana na wanyamapori na rasilimali ... nyingine mara nyingi si kati ya hao wanaodhurika na migogoro kati ya watu na wanyamapori.

# Utangulizi



kudhuru uhusiano pale watu wanapojitenga na wenzao na pengine kuunda makundi kuwazunguka marafiki zao. Hii inaweza kuongeza mgogoro pale ambapo sababu za mgogoro zinabaki bila kutatuliwa (Jedwali namba 1).

*MFANO: Tuseme mtu ananunua ng'ombe kutoka kwa jirani yake. Ndani ya wiki moja huyo ng'ombe anaugua. Mnunuzi ana matumaini ya kwamba ng'ombe atapona. Hata hivyo, mnunuzi anahisi kwamba ngo'mbe alikuwa mgonjwa tangu aliponunuliwa. Hajadiliani kuhusu hili suala na muuzaji, na anakaa mbali na maeneo ambayo wanaweza kukutana.*

Kuchukuliana ambako kunaweza kuwa hali ya "kukubali kushindwa" kwa ajili ya kuleta amani (ya muda mfupi). Hii pia inajulikana kama shindwa/shinda ("mimi ninashindwa, wewe unashinda"). Kutoa mhanga maslahi yetu kwa ajili ya maslahi ya wengine mara nyingi inasifiwa. Lakini, kwa mtazamo wa muda mrefu, kama suala hilo ni muhimu, kutoridhika kunaweza kujengeka, na kuathiri uhusiano.

*Rafiki wa mnunuzi na familia walimwambia kwamba aachane na suala hilo na kwa sasa amtibu ng'ombe tu, kwa kuwa muuzaji anaweza kukasirishwa na shutuma yoyote inayohusu mauzo ya mifugo isiyo na afya. Halafu ng'ombe anakufa........*

Ushindani au ushambulizi unatokea watu wanapojiweka wenyewe mbele na wanalenga matokeo ya "wao kushinda/na wengine kushindwa". Mbinu ya ushindani inaweza kugeuka kuwa kushindania mamlaka, ambayo huenda mbali zaidi ya mgogoro asilia. Watu walio kwenye mgogoro wanaweza kuamua kuanza vitisho au uhasama ili kulazimisha matakwa yao. Mbinu hii ya ushindani haileti uhusiano mzuri.

*Kwa hasira ya kupoteza ng'ombe na kuhisi kudhalilika kwa kutofanya kitu chochote, mnunuzi aliiba ndama kutoka kwa muuzaji wakati wa usiku.*
*Muuzaji naye akatishia kuchoma moto nyumba ya mnunuzi. Walipokutana sokoni, walishutumiana kwa kuwa na mifugo isiyo na afya, na kupigizana kelele kuhusu ugomvi uliotokea hapo zamani. Wakaanza kupigana lakini wakatenganishwa na marafiki ili wasiendelee kupigana.*

Kuafikiana, pale ambapo mtu "anashinda kidogo, anashindwa kidogo" mara nyingi inaonekana kama ndiyo njia nzuri ya kusuluhisha mgogoro. Kila mmoja anapata anachotaka, lakini pia kila mmoja anakosa kidogo. Maafikiano mara nyingi yanaweza kuleta suluhisho la haraka na la muda mfupi. Lakini kwa suluhisho la muda mrefu, watu wanaweza kutofurahia matokeo kwa vile wanafikiria walichokikosa.

*Kwa kushinikizwa na marafiki na familia, hao wawili walikaa chini na kuzungumzia tatizo lao. Mwanzoni kila mmoja alisisitiza kuwe na suluhisho la mmoja 'kushinda/na mwingine kushindwa.'*
*Mnunuzi: "Nitakurudishia ndama wako utakaponilipa kiasi nilicholipia ng'ombe aliyekufa."*
*Muuzaji: "Nipe ndama wangu sasa hivi, na unipe magunia mawili ya mahindi kwa usumbufu ulionisababishia."*
*Baada ya saa kadhaa, marafiki waliwasihi na hatimaye walifikiria kuafikiana: mnunuzi atamrudisha ndama. Muuzaji atamuuzia ng'ombe, ambaye atakaguliwa na daktari wa mifugo, kwa bei ya chini ya bei ya soko.*
*Sio wote waliofurahia kabisa lakini kila mmoja anadhani "ameshinda" kitu.*

Ushirikiano, au utatuzi wa tatizo, unahusisha:

- kuchunguza sababu za ndani za mgogoro – ambazo mara nyingi zinaweza kwenda nje ya wahusika katika mgogoro;
- kuongeza njia zinazoweza kuleta suluhisho kwa kuwa taarifa zaidi zinajulikana; na
- kushirikiana na kila mtu anayehusika kuleta suluhisho la muda mrefu la "wote kushinda" ambalo litaongeza uhusiano wa kikazi.

Ushirikiano, au utatuzi wa mgogoro wa pamoja, mara nyingi ndiyo njia bora ya kutatua mgogoro pamoja na kuendeleza uhusiano katika jamii.

Ushirikiano huchukua muda, na unahitaji watu wote wajitolee katika huu mchakato. Mchakato huu mara nyingi unawezeshwa na mtu kutoka nje au msuluhishi, iwe kutoka serikalini, asasi isiyo ya kiserikali au kutoka katika jamii nyingine.

*Kabla ya kukubaliana na mkataba, mnunuzi na muuzaji walikutana na msuluhishi kutoka asasi isiyo ya kiserikali kutoka ngazi ya chini. Waliamua kupata taarifa nyingine na walianza kwa kushauriana na daktari wa mifugo kama*

JEDWALI NAMBA1: **FAIDA NA HASARA ZA MBINU ZA KUTATUA MIGOGORO**

| Mkakati | Faida | Hasara/vikwazo |
|---|---|---|
| Ushirikiano | Kuangalia mgogoro kama ni tatizo linalohitaji kutatuliwa kwa pamoja kunaleta suluhisho lenye kunufaisha watu wote | • Inachukua muda mrefu na nguvu nyingi<br>• Inahitaji uaminifu wa pande zote mbili<br>• Washirika wengine wanaweza kuchukua fursa ya uaminifu na uwazi wa mwingine kutoa maamuzi yasiyokuwa sahihi |
| Kuafikiana | Kushinda kitu na kupoteza kidogo ndio mkakati wa kawaida. Kwa kuafikiana, kila mtu anaweza kuridhisha maslahi yake japo kidogo | • Washirika wanaweza kukosa kuona maadili muhimu na malengo ya muda mrefu<br>• Inaweza kufanya kazi vizuri zaidi kwa muda mfupi lakini kwa muda mrefu chuki inaweza kujengeka<br>• Inaweza isifanikiwe iwapo mahitaji ya mwanzo ni makuwa sana |
| Ushindani | Mtu mmoja ataweza ijapokuwa kwa muda kufikia mahitaji yake na kuhisi kama "mshindi" kwa kutumia mamlaka au nguvu. Hii inaleta suluhisho la "mmoja kushinda/na mwingine kushindwa" | • Mgogoro unaweza kukua na yeyote atakayeshindwa atajaribu kulipa kisasi<br>• Haki inaweza kuathiriwa |
| Kuchukuliana | Kuridhisha wengine kwa kupuuza mgogoro, kwa kujaribu kulinda uhusiano. Kwa kawaida inakuwa "mmoja kushindwa/na mwingine kushinda" | • Mawazo na wasiwasi wa mmoja wao hayataweza kutiliwa maanani<br>• Mtu mmoja anaweza kupoteza imani na ushawishi kwa siku zijazo |
| Kuepuka | Watu wanaepuka migogoro kwa kujitoa, kukwepa au kuahirisha matokeo - yaani "shindwa/shindwa" au "hakuna mshindi/hakuna aliyeshindwa" | • Maamuzi muhimu yanaweza kushindikana<br>• Kuahirisha mgogoro kunaweza kusababisha madhara zaidi |

*yule ng'ombe alikuwa mgonjwa wakati akiuzwa. Inaoekana kwamba inawezekana kuwa ng'ombe hakuwa mgonjwa wakati wa mauzo. Hatimaye muuzaji alikubali kwamba huyu ng'ombe mdogo, kama wengine hivi karibuni, hawakunyonya maziwa ya mama zao vizuri na walikuwa wana uzito mdogo; daktari wa mifugo anakamilisha kwa kusema kwamba hii inaweza kuwa sababu ya kushambuliwa na maradhi kwa urahisi.*

*Wengine katika jamii walisema kwamba ng'ombe wengi wamekuwa wakiugua maradhi mbalimbali. Kwa maneno mengine, hii inaweza kuwa tatizo la jamii nzima.*

*Wasuluhishi walimshauri daktari wa mifugo wa wilaya kuhusu kinga kwa ajili ya ng'ombe wote waliopo kijijini. Wilaya imekubali kutoa dawa ya kuoshea na huduma ya chanjo kwa muda muafaka, pamoja na kutoa taarifa ya jinsi jamii inavyoweza kuboresha eneo la malisho lililoharibika.*

Katika mchakato wa kutafuta taarifa, ugunduzi wa sababu za ndani za migogoro, na kuja na suluhisho mbadala ambalo litaisaidia jamii nzima, mnunuzi na muuzaji wameweza kurudisha uhusiano wao.

Sasa wamekubaliana kwamba

- wote watafaidika na fursa ya huduma bora ya matibabu ya mifugo
- mnunuzi atarudisha ndama
- muuzaji atampa mnunuzi ndama aliye na afya atakayezaliwa karibuni, kwa kubadilisha na gunia la mahindi.

Wote wakasema kwamba makubaliano hayo ni ya haki na inaonekana wameridhika. Wamealika marafiki wengine na majirani ili kusherekea.

Makubaliano yanaandikwa na kushuhudiwa na wasuluhishi, Ofisi ya Wilaya, na jamii.

## MSAADA UNAPATIKANA: MIFUMO YA KIMILA, KITAIFA NA YA KUSHIRIKIANA YA UDHIBITI WA MIGOGORO

Kuna mifumo mitatu mikuu ya kusaidia mtu mmoja mmoja na jamii kudhibiti migogoro. Kila mfumo una nguvu zake na mapungufu yake (Jedwali namba 2).

### Mifumo ya kimila ya kudhibiti migogoro

Vijiji vya Tanzania vimeendeleza mfumo wa kisheria wa kimila ambapo viongozi wa vijiji na wazee

JEDWALI NAMBA 2: **FAIDA NA HASARA ZA MFUMO WA KUSULUHISHA MGOGORO**

| Mfumo | Faida | Hasara |
|---|---|---|
| Mifumo ya kimila | • Inahimiza ushiriki wa jamii na kuheshimu maadili na tamaduni katika jamii.<br>• Ufanyaji maamuzi ni kwa ushirikiano na unaendeleza mapatano.<br>• Inasaidia jamii kujengewa uwezo.<br>• Inahusisha viongozi wa kijiji kama wasuluhishi au wazungumzaji.<br>• Inaleta hali ya umiliki wa mchakato na matokeo yake. | • Nafasi ya mfumo huu imechukuliwa na mfumo wa mahakama na sheria za kiutawala.<br>• Inaweza isihusishe watu kwa misingi ya jinsia, kundi, kabila na sababu zingine.<br>• Inaweza kuruhusu viongozi wa kijiji kutumia mamlaka yao kwa manufaa yao wenyewe au kwa manufaa ya kundi lao la kijamii au mteja wao.<br>• Inaweza isiandike maamuzi na mchakato yaliyofanywa kwa njia ya mdomo kwa ajili ya matumizi ya baadaye. |
| Mfumo wa kisheria wa kitaifa | • Inajenga utawala wa sheria, inawezesha asasi za kiraia na kuendeleza uwajibikaji.<br>• Inahusisha wataalamu wa sheria na kiufundi katika kufanya maamuzi.<br>• Ina uwezo wa kufanya maamuzi kulingana na sifa ya kesi yenyewe, na pande zote mbili zinabaki sawa mbele ya sheria. | • Mara nyingi haiwahusishi watu maskini, wanawake, makundi yaliyotengwa na wanajamii wanaoishi mbali sana kwa sababu ya gharama, umbali, matatizo ya lugha, vikwazo vya kisiasa, kutokuwa na elimu na ubaguzi.<br>• Unaruhusu ushiriki mdogo wa walalamikaji katika kufanya maamuzi. |
| Njia mbadala za udhibiti wa migogoro | • Hazina vipingamizi katika udhibiti shirikishi wa mgogoro kama ilivyo katika njia nyingine za kibunge, kiutawala, kimahakama na kimila.<br>• Inaendeleza maslahi ya pamoja.<br>• Inajenga makubaliano na umiliki wa mchakato wa suluhisho.<br>• Inasisitiza jamii kujengewa uwezo ambao utawatayarisha watu kuwa wawezeshaji wazuri, watoa taarifa, wataalamu wa mipango na wasuluhishi wa migogoro. | • Unashindwa kufanyia kazi miundo isiyo sawa, na inaweza kuchochea au kuzidisha tofauti za kimadaraka zilizopo.<br>• Ina ugumu wa kutoweza kuwakalisha wadau wote kwenye meza ya majadiliano.<br>• Unatoa maamuzi ambayo yanaweza yasiwe na nguvu kisheria.<br>• Unaweza kutumia mbinu ambazo zilianzishwa katika mazingira na tamaduni nyingine bila ya kuzihusisha na mazingira ya kwao wenyewe. |

wanaoheshimika wanasimamia *sheria za kimila.* Kwa mfano, Kamati za Ardhi za Kijiji za Usuluhishi zinatumia sheria ya kimila ili kufafanua haki za ardhi. Mafanikio ya mfumo huu wa sheria katika kudhibiti migogoro juu ya rasilimali unategemea uhiari wa walalamikaji pamoja na uwezo wa utekelezaji wa mamlaka za kimila.

Mifumo mingine ya kimila hutumia *usuluhishi* – pale ambapo taasisi au watu walio nje ya mgogoro kama vile kamati ya wazee wanawezesha majadiliano na kufanya maamuzi kati ya walalamikaji (kisanduku namba 2). Au wanaweza kutumia njia ya usuluhishi ambapo taasisi au watu walio nje ya mgogoro, waliokubaliwa na pande zote mbili. Msuluhishi anasikiliza kila wazo na anatoa maamuzi ambayo yataleta usuluhishi.

## Mifumo ya kisheria ya kitaifa

Mfumo wa kisheria wa kitaifa unatatua migogoro kupitia kesi katika mahakama za sheria: walalamikaji wanaelezea kesi yao mbele ya jaji au maofisa wengine. Walalamikaji mara nyingi wanawatumia wanasheria. Mahakama inasikiliza malalamiko na kupitia ushahidi kabla ya kuamua nani mshindi – ambapo watasema kwa uhakika nani mshindi na nani ameshindwa.

Mfumo wa kisheria wa kitaifa unaanzia katika kamati za vijiji mpaka katika mahakama za kata na mahakama za wilayani, kimkoa na katika ngazi ya kitaifa. (URT, 1997). Mifumo mingine ya kitaifa pia inahusisha sheria za kimila au maadili ya jamii (FAO, 2005).

Mifumo ya kisheria pia mara nyingine inatambua usuluhishi unaotoa maamuzi ambayo ni ya lazima, pale ambapo taasisi au watu walio nje ya mgogoro wanatoa mamuzi ya mwisho.

**KISANDUKU NAMBA 2: MGOGORO KATI YA MKULIMA NA MFUGAJI WA AFRIKA MAGHARIBI**

Mgogoro juu ya matumizi ya ardhi ni kitu cha kawaida huko Sahel pamoja na Afrika Mashariki. Katika utafiti uliofanyika hivi karibuni katika vijiji vinne vya Niger, wanajamii walisema kwamba uharibifu wa mazao na kuwalisha mifugo mazao yaliyobaki shambani baada ya mavuno usioruhusiwa unachukua asilimia 80 ya migogoro yote iliyotolewa taarifa kati ya wakulima na wafugaji. Migogoro pia huibuka kutokana na matumizi ya vyanzo vya maji, wizi wa wanyama, na upanuzi wa mashamba unaoingilia njia za asili za mifugo.

Licha ya kwamba sababu za msingi za migogoro huwa zina utata sana, migogoro mingi inatatuliwa, kwa kawaida kwa kutumia usuluhishi wa wazee na machifu. Hii hufanyika sana na kufanikiwa katika vijiji ambapo makundi yote ya kijamii yanaheshimu hizi mamlaka.

Utafiti pia uligundua kwamba uhusiano imara na mawasiliano baina ya wakulima na wafugaji yanasaidia watu kuzuia na kudhibiti migogoro. Taarifa zilizopatikana zinathibitisha kwamba migogoro kati ya mikakati tofauti ya maisha inaweza kudhibitiwa ipasavyo na wanajamii.

*Turner, M. et al., 2007*

## Udhibiti wa pamoja wa migogoro, pia huitwa "Udhibiti Mbadala wa Migogoro" (ACM)

Udhibiti wa pamoja wa migogoro ambao pia huitwa "utatuzi wa tatizo" au "Udhibiti Mbadala wa Migogoro" - unaweza kuhusisha wasuluhishi kutoka asasi isiyo ya kiserikali, asasi ya kijamii, au mamlaka ya serikali.

ACM inahimiza ufanyaji wa maamuzi wa pamoja kati ya walalamikaji ili kuleta suluhisho la "kushinda-kushinda". Msuluhishi anasaidia mazungumzo, anasaidia kuweka taarifa pamoja, anahimiza mapatano, anasaidia wote wasikilizane vizuri, na anasaidia kujenga makubaliano ya hiari. Ingawa wadau wanafanya maamuzi yao wenyewe.

ACM hufanikiwa kwa walalamikaji ambao wapo sawa kinguvu, kama vile mkulima na mfugaji wanaogombania ardhi. Iwapo, kwa mfano, Ofisa wa Wilaya atadai kwamba mkulima amevunja sheria, kesi inaweza kupelekwa katika mfumo wa kisheria wa kitaifa.

# Utangulizi

# Hatua kuelekea mafanikio



*Mkutano wa wanakijiji kuhusu mgogoro*

## UDHIBITI MADHUBUTI WA MIGOGORO

### Hatua ya 1: Jiandae kwa ajili ya udhibiti wa mgogoro

Hatua ya kwanza inayopendekezwa ni kuchagua kamati ya kijiji ya udhibiti wa mgogoro. Wanakijiji wanaweza kuandaa miongozo kwa ajili ya sifa wanazozitaka za wajumbe wa hiyo kamati kama vile sifa ya kuwa wa haki, mkweli, na msikilizaji mzuri na kuchagua wajumbe kwenye mkutano wa kijiji.

Hatua ya kuchagua lazima ihusishe wazee, viongozi wa kimila, wanaume, wanawake na vijana, na wajumbe wa taasisi za kitamaduni za udhibiti wa migogoro.

### Kuamua jinsi ya kuendelea

Wakati vijiji tisa vikifikiria huenda vikaanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Burunge, Kaskazini mwa Tanzania, migogoro iliibuka, mingine iligeuka kuwa ya vurugu. Wanakijiji wengine waliitaka Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, na wengine hawakuitaka; wengi hawakujua matokeo yake.

Hatua ya kwanza katika kusuluhisha migogoro ndani ya vijiji ilichukuliwa na viongozi wa kitamaduni na wazee, ambao waliitisha mikutano kwa ajili ya kuelezea malalamiko na kutafuta taarifa kwa hiyo kutumia njia za kitamaduni na kutayarisha mazingira ya kuwa na suluhisho la pamoja. Kwa maelezo ya kina kuhusu jinsi kijiji cha Burunge kilivyotatua mgogoro kuhusiana na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, angalia kiambatanisho 1.

Washiriki lazima wazingatie zile mbinu kuu tano za kutatua migogoro na iwe zitalenga usuluhishi wa pamoja au udhibiti wa aina nyingine (kwa mfano, suluhisho la ushindani kwa kupitia usuluhishi wa mahakama).

### Hatua ya 2: Kuchanganua mgogoro

Kule Burunge, wazee na kamati ya mgogoro walialika asasi isiyo ya kiserikali ili isaidie kusuluhisha.

Hiyo asasi isiyo ya kiserikali ilisaidia washiriki kukusanya taarifa ili kuelezea huo mgogoro, jinsi ulivyoanza na uliyoendelea, nani walihusika, jinsi ulivyoathiri watu, na matatizo gani ya ndani yanayoweza kuonekana.

Hatua ya uchambuzi inahitaji maswali mengi na kusikiliza sana maelezo (kisanduku namba 3). Maoni ya kila mtu lazima yazingatiwe kwa uangalifu. Kwenye kesi ya Burunge, ilikuwa wazi kwamba:

1. pingamizi nyingi kwa ajili ya kuanzisha WMA zilisababishwa na upotoshaji wa taarifa – wadau hawakuelewa jinsi ambavyo WMA ingewaathiri, na
2. wakazi walikuwa na wasiwasi mwingi, wasiwasi ambao unaweza kutatuliwa wakati wa mchakato wa kuanzisha WMA.

# Hatua kuelekea mafanikio



**KISANDUKU NAMBA 3: MASWALI YANAYOSAIDIA KUCHANGANUA MGOGORO**

**Matatizo (sababu kuu na uchanganuzi wa tatizo)**

- Mgogoro unahusu nini?
- Mgogoro ulianzaje?
- Nini vinaweza kuwa vyanzo vya mgogoro? Je vyanzo vyaweza kuwa nje ya uwezo wa wahusika wa mgogoro?
- Matatizo gani yanaweza kuzungumzwa?
- Maadili au maslahi gani yanaweza kuwa na changamoto?

**Makundi yaliyohusika (uchambuzi wa wadau)**

- Nani anahusika katika mgogoro?
- Wahusika wanawakilisha makundi gani?
- Maslahi, malengo, nafasi na mahitaji yao ni yapi?
- Wanaogopa nini?
- Wanajipanga vipi, na wana nguvu zipi kimamlaka?
- Je hayo makundi yana uwezo au yako tayari kufanya kazi pamoja?
- Nini historia ya uhusiano baina ya makundi hayo?

**Cha Kufanya:**

- Nini uzoefu kuhusu kesi kama hizo kwa siku zilizopita?
- Je taasisi au watu walio nje ya mgogoro kutoka nje anaweza kuwa wa msaada?
- Je kuna vikwazo kutoka nje vya kusuluhisha mgogoro?
- Je kuna rasilimali nyingine zinazoweza kusaidia katika kutafuta taarifa au udhibiti?

Katika kuchambua historia ya tatizo na hali ilivyo sasa, kuchambua maslahi, mahitaji, woga na malengo ya wadau ni muhimu (Jedwali numba 3).

## Hatua ya 3: Makubaliano ya awali

Kwa kuwa Burunge ilihusisha vijiji tisa, makundi mengi yalikuwa na majukumu ya kutekeleza katika haya mazungumzo (jedwali namba 4). Hatua za majadiliano zilihusisha:

**Uanzaji:** Wadau, kamati na viongozi walikutana pamoja ili kuijenga nia yao ya kufikia makubaliano. Makundi muhimu na wasemaji wakuu walitambuliwa kutoka pande zote mbili; walihusisha viongozi wa vijiji, viongozi wa kimila, wazee, wanawake na vijana. Halmashsauri ya Wilaya, wawakilishi kutoka makampuni ya uwindaji, wawekezaji katika utalii, Asasi isiyo ya Kiserikali na AWF.

**DONDOO: MISIMAMO DHIDI YA MASLAHI**

Kwa kawaida walalamikaji hujikita sana kwenye "msimamo". Kwa mfano, mwanakijiji mmoja anaweza kumwambia mwenzake "inabidi uache kulima hapa, ambapo kuna ng'ombe wangu." Mwanakijiji mwingine atasema "inabidi uache kulisha mifugo yako hapa ambapo mimi ninalima."

Lakini msuluhishi mwenye utaalamu atajaribu kutenganisha maslahi yao na "misimamo"– kwa hiyo atawaonyesha njia nyingine zinazoweza kumaliza tatizo lao.

Katika mfano huu, maslahi yanaweza kuhusisha kuzalisha au kupatikana kwa chakula na/au mifugo. Kwa hiyo uwezekano mpya unaweza kuwa:

- Je kuna sehemu nyingine ya kuzalisha chakula? Kuna sehemu nyingine ya kuchunga mifugo?
- Je kuna njia nyingine ya kuzalisha kiwango hicho hicho cha chakula kwenye eneo dogo, huku mifugo ikizuiwa kuingia kwenye eneo lenye mazao?
- Je inaleta maana kuendeleza biashara nyingine na kununua chakula badala ya kukizalisha mwenyewe?
- Je inawezekana kuanzisha eneo la kulisha mifugo, ambapo ng'ombe wengi na wenye afya wataweza kufugiwa kwa kutumia eneo dogo?

Kutenganisha maslahi na msimamo kunaweza kuleta suluhisho jipya na lenye ubunifu ambalo hapo awali halikufikiriwa kabisa.

**Kanuni na ajenda:** Makundi yalikubaliana na kanuni kwa ajili ya mawasiliano, mazungumzo na kufanya maamuzi. Wakaweka ajenda na kupendekeza ratiba.

**Mpangilio:** Wadau waliandaa utaratibu kama vile muda na mahali pa kufanyia mkutano. Kikundi kazi na viongozi wa vijiji walichukua muhtsari wa mikutano. Taarifa hii ilisambazwa ili kuwataarifu wadau wote kuhusu maendeleo na malengo ya mikutano ijayo.

**Utafutaji wa taarifa wa pamoja:** Makundi yalikubaliana na taarifa ipi ilikuwa muhimu kwa huo mgogoro na kuipeleka hiyo taarifa kwenye kamati ya mazungumzo. Kutokana na juhudi za utafutaji wa taarifa, kwa mfano safari ya mafunzo na mafunzo mengineyo, wote wanaohusika walijifunza mengi kuhusu WMA ingemaanisha nini, na uzoefu kutoka kwa wanajamii wengine kuhusu WMA. Watu pia walijifunza mengi kuhusu aina ya fursa za biashara ambazo zingeletwa na WMA.

JEDWALI NUMBA 3: **UCHAMBUZI WA WADAU: MAHITAJI NA WOGA WA WADAU WAKUU SABA KATIKA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI (WMA) YA BURUNGE**

| Wadau katika migogoro | Maslahi | Mahitaji | Kutamani/Woga |
|---|---|---|---|
| **Wakulima mmoja mmoja** | • Ardhi kwa ajili ya mazao ya kuuza na chakula<br>• Kuzuia kuporwa ardhi | • Fedha kwa ajili ya kununua ardhi na rasilimali nyingine<br>• Masoko yatakayokuwepo<br>• Ardhi kwa ajili ya kilimo | **Woga:**<br>• Kupotea kwa mazao kutokana na wanyamapori na uharibifu unaofanywa na mifugo<br>**Kutamani:**<br>• Kulipwa fidia kutokana na kupoteza mazao<br>• Kuongeza ardhi kwa ajili ya kilimo |
| **Wafugaji** | • Mifugo kwa ajili ya kipato na chakula | • Miundombinu kwa ajili ya mifugo<br>• Fedha kwa ajili ya kununua dawa za mifugo na pembejeo<br>• Ardhi ya kulishia mifugo wakati wa kipindi cha ukame katika WMA | **Woga:**<br>• Kusambaza magonjwa ya wanyamapori kwa mifugo na wanyamapori kushambulia mifugo<br>• Uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya kilimo<br>**Kutamani:**<br>• Ardhi zaidi kwa ajili ya kulishia mifugo. |
| **Vijiji kimoja kimoja** | • Hifadhi wanyamapori kupitia WMA<br>• Miradi ya biashara inayohusiana na uhifadhi (CBVs) | • Mapato kutokana na wanyamapori<br>• Mapato kutokana na WMA<br>• Uhitaji wa kupanga matumizi ya ardhi<br>• Tathmini ya rasilimali za kijiji | **Woga:**<br>• Mgawanyo wa mapato na vijiji vingine usio sawa<br>• Kuathiriwa kwa biashara ya utalii au maslahi binafsi<br>• Kupanua hifadhi ndani ya ardhi ya kijiji<br>**Kutamani:**<br>• Kupata faida kutokana na WMA<br>• Wawekezaji katika uwindaji na utalii kuchangia miradi/shughuli za maendeleo za vijiji |
| **Vijiji kwa pamoja** | • Kuhifadhi wanyamapori kupitia WMA<br>• Miradi na mapato | • Wanahitaji mapato kutoka WMA<br>• Kuanzisha shughuli za kujiongezea kipato kwa wanawake<br>• Kutengeneza ajira<br>• Kupanga kwa pamoja matumizi ya ardhi<br>• Tathmini ya pamoja ya rasilimali zilizomo vijijini | **Woga:**<br>• Mgawanyo wa mapato hautakuwa wa haki baina ya vijiji washirika<br>• Makampuni ya uwindaji yanaweza kuwinda hata nje ya vitalu vya uwindaji na kuingia ndani ya WMA<br>**Kutamani:**<br>• Faida za kiuchumi kutoka WMA<br>• Ushiriki zaidi katika miradi ya uhifadhi |
| **Wawekezaji wa utalii (hoteli za mahema na kambi, utalii wa kupiga picha)** | • Anzisha miradi ya biashara ya utalii | • Hifadhi wanyamapori<br>• Kuongeza mapato kutoka kwenye uwekezaji kwenye utalii | **Woga:**<br>• Makampuni ya uwindaji yatafukuza au kupunguza wanyamapori<br>**Kutamani:**<br>• Kupendelea kuwepo kwa WMA zaidi vijijini kuliko uwindaji wa wanyamapori |
| **Makampuni ya uwindaji** | • Kuwinda wanyamapori | • Wanahitaji fedha kutokana na shughuli za uwindaji | **Woga:**<br>• Wanakijiji kufuatilia shughuli za uwindaji<br>**Kutamani:**<br>• Wanakijiji kuhifadhi wanyamapori na kuongeza idadi ya kuwinda |
| **Wahifadhi wa wanyamapori/ mamlaka za hifadhi** | • Kupunguza kumegwa kwa maeneo ya malisho ya wanyamapori<br>• Linda rasilimali za wanyamapori | • Anzisha WMA kwenye vijiji | **Woga:**<br>• Kuzuia njia za wanyampori kupita, ujangili au uwindaji haramu<br>**Kutamani:**<br>• Ardhi zaidi kwa ajili ya malisho ya wanyamapori, maeneo ambayo wanyama wanasambaa na wanayozalia<br>• Mifugo iweze kuishi na wanyamapori |

# Hatua kuelekea mafanikio



JEDWALI NUMBA 4: WADAU NA MAJUKUMU YAO WAKATI WA UDHUBITI WA MGOGORO WA BURUNGE

| Na. | Mdau | Cheo/Nafasi | Majukumu |
|---|---|---|---|
| 1. | Maofisa wa Halmashauri ya Wilaya (kwa mfano Afisa Wanyamapori wa Wilaya, Ofisa Ardhi wa Wilaya) | Msuluhishi | • Mkufunzi wa wanajamii juu ya umuhimu wa kuanzisha WMA vijijini kwao |
| 2. | African Wildlife Foundation (AWF) | Msuluhishi | • Kuwezesha mafunzo<br>• Kuandaa vifaa vya mafunzo<br>• Kuandaa usafiri wa wakufunzi<br>• Kuandaa safari za mafunzo za wanajamii |
| 3. | Viongozi wa kijadi na wazee | Mhusika wa mgogoro na msuluhishi | • Kulinda na kuhakikisha amani vijijini<br>• Washauri wakuu wa kijiji<br>• Wafanya maamuzi<br>• Jukumu la usuluhishi |
| 4. | Wanakijiji (wakulima, wafugaji na wafanyabiashara) | Wahusika wa mgogoro | • Watu watafundishwa kuhusu WMA<br>• Wawakilishi kuunda kamati za mgogoro, wataenda kwenye safari za mafunzo<br>• Watekelezaji wa mipango ya kijiji iliyokubalika |
| 5. | Mkuu wa Wilaya | Msuluhishi | • Anahusika katika mkutano mmojawapo wa usuluhishi pale ambapo mgogoro umefikia hatua ya vurugu, kwa hiyo jukumu kuu ni kuhakikisha amani inakuwepo wilayani na vijijini<br>• Kutetea sera juu ya uanzishwaji wa WMA |
| 6. | Wawekezaji katika sekta binafsi | Mhusika katika mgogoro/ wengine kama wasuluhishi | • Kuhakikisha ushiriki wa jamii katika miradi ya uhifadhi (kusimamia na kuendesha biashara ya pamoja) na mgawanyo wa mapato<br>• Kuchangia katika miradi ya maendeleo ya kijiji. |

## Hatua ya 4: Makubaliano

Kuanzisha WMA ya Burunge kulihitaji mazungumzo mengi, yote ndani na kati ya vijiji.

Makubaliano yanalenga kufikia makubaliano ya haki, na ya kudumu, ambayo kila mtu atafaidika. Wasuluhishi wanawaongoza wadau katika kujikumbusha na kujitambua ili kila mmoja atambue maslahi yake ya muda mrefu na kuthamini maslahi ya wengine ya muda mrefu.

### Kutambua maslahi (na sio misimamo)

Maslahi yanahusisha kile unachotamani na woga ambao unampa motisha kila mhusika katika mgogoro. Kwa mfano, "hatutaki WMA Burunge" ulikuwa msimamo wa baadhi, lakini kulikuwa na maslahi mengi ndani ya huo msimamo.

Mengine yalikuwa: "Tunataka umiliki wa ardhi ulio salama, tunataka tuwe na uwezo wa kuendelea kulisha mifugo yetu, tunataka kulinda ardhi yetu kutoka kwa wavamizi; tunataka tuwe na uwezo wa kupata kipato kutoka katika ardhi yetu ..."

Yanapowekwa wazi, maslahi yanaweza kufikiwa kwa njia nyingi, ikiwa ni pamoja na zile ambazo zisingeweza kufikiriwa na hao watu wanaogombana.

**Kuainisha njia mbadala:** Utatuzi wa mgogoro ulio wa mafanikio unahitaji wahusika wa mgogoro na wasuluhishi kubuni njia mbadala kwa ajili ya kuridhisha maslahi mbalimbali. Inasaidia kutengeneza orodha ndefu ya njia mbalimbali zinazowezekana; nyingine zinaweza kuwa hazijawahi kufikiriwa hapo awali, lakini zinaweza kuleta matunda mazuri.

Kwa mfano, hivyo vijiji tisa vya WMA ya Burunge vilitafuta njia mbalimbali za kugawana mapato, pamoja na kumpa kila mtu haki sawa; kuwapa zaidi wale waliochangia zaidi kwenye ardhi, au wale wenye wanyamapori wengi kwenye ardhi yao, kuhamisha wawekezaji waliopo.

**Kutathmini na kuchagua njia mbadala:** Kule Burunge, hatimaye vijiji vilikubaliana kwamba kila kijiji kitapata malipo ya kodi kutegemeana na kiasi gani cha ardhi kilichangia; lakini vijiji vyote vitagawana kwa usawa faida itokanayo na biashara ya wanyamapori katika WMA yao.

Ndani ya vijiji, wakazi walikubaliana kuwe na maeneo ya wazi ambayo wataruhusu au kutoruhusu kilimo au uchungaji, na wale wanaoishi ndani ya eneo ambalo limekuwa WMA waligawiwa ardhi kwenye eneo jingine.

Wakati maamuzi mbalimbali yanafikiwa, wahusika wa mgogoro hawatoi maoni kuhusu maamuzi yoyote mpaka watakapokuwa wamemaliza kuorodhesha maamuzi yote wanayoweza kufikiria. Makundi kwa pamoja yanaamua ni mawazo gani mazuri kwa ajili ya maslahi mbalimbali. Hii inasaidia wadau kupata mikataba yenye uhalisia na ambayo inaweza kusimamiwa.

## Hatua ya 5: Kukubaliana

Makubaliano huisha pale ambapo maamuzi yanakubaliwa kwa pamoja.

**Maidhinisho.** Wasuluhishi wa Burunge waliandaa mkataba wa makubaliano ili kuhakikisha kwamba mkataba utakumbukwa na kuelezewa kwa ufasaha.

Maidhinisho na uwekaji kumbukumbu unasaidia washiriki kuwa na imani kwamba kila mtu atatimiza majukumu yake katika mkataba. Inasaidia washiriki kujadiliana na kukubaliana juu ya mbinu ili kuhakikisha washirika wanaelewa na kutimiza wajibu wao.

**Utekelezaji.** Mkataba ukishakuwepo, wahusika kwa pamoja wanatengeneza mpango wa utekelezaji; mpango huo unahusu nani atafanya nini, lini, rasilimali zipi na matokeo yanayotarajiwa. Katika mgogoro wa Burunge, makubaliano kadhaa ya mikataba yalipelekea moja kwa moja vijiji kusajiliwa, kupanga matumizi ya ardhi, na kuanzishwa kwa WMA. Hiyo WMA nayo imewezesha kuanzishwa kwa biashara kadhaa zinazohusiana na uhifadhi, ambazo sasa zinaingiza kiasi kikubwa cha fedha kwa jamii (angalia Kisa Mkasa mwisho wa Sura hii na Sura ya 4 kuhusu WMA).

Licha ya hivyo, mchakato ulisaidia wanakijiji kujifunza jinsi ya kupanga kwa pamoja, ambacho ni kitu muhimu pale ambapo wanatumia mfumo wa ekolojia kwa pamoja.

## Hatua ya 6: Ufuatiliaji, tathimini na kuondoka kwa wasuluhishi

Timu ya usuluhishi wa mgogoro au wasuluhishi wengine wametengeneza mfumo wa kutekeleza na kufuatilia mkataba unaohusisha wadau na/au msuluhishi wa kijijini anayeaminika (kisanduku namba 4). Timu hiyo inaweza kuhusisha mikakati ya kujenga uwezo wa jamii wa kuzuia au kusuluhisha matatizo ya baadaye.

### KISANDUKU NAMBA 4. MASWALI MUHIMU KWA AJILI YA TATHIMINI, MAJUKUMU NA UTEKELEZAJI

- Wadau watahakikisha vipi kwamba mkataba utafanyiwa kazi?
- Je utekelezaji wa mkataba unahitaji ushiriki rasmi wa wataalamu au makundi, kama vile watawala, viongozi wa makundi ya watumiaji wa rasilimali na viongozi wa kisiasa katika jamii?
- Wahusika watadhibiti vipi matokeo yoyote ambayo hayakutarajiwa kutoka kwenye mkataba?
- Utaratibu gani wa ufuatiliaji utawekwa ili kuhakikisha mkataba unafuatwa?
- Jukumu la timu ya usuluhishi katika ufuatiliaji ni lipi? Je kuna wafuatiliaji wasiofungamana na upande wowote, wanaoaminika kutoka katika jamii?
- Wahusika wataelezea na kutambua vipi hatua zinazofuata kama shughuli zitakazotekelezwa, muda, wanaohusika, rasilimali zinazohitajika, na matokeo yanayotarajiwa (mpango wa utekelezaji).

Hatua hii ni muhimu kwa sababu migogoro inaweza kutokea tena. Sana sana katika mgogoro mkubwa unaohusisha wadau wengi, "makubaliano" yanaweza kutoeleweka vizuri, au watu wanaweza kuhisi kulazimishwa kukubaliana na upande mmoja au mwingine, au wanaweza wakawa wamekosa mikutano muhimu ambapo wangeweza kuelezea kutoridhika kwao.

Kwa hakika, baadhi ya yaliyotajwa hapo juu yanaonekana kutokea katika kesi ya Burunge, na hata kitini hiki kinapoandikwa, vijiji viwili vimekwisha jitoa kwenye WMA, vikidai kwamba havikukubaliana na kuanzishwa kwake. Hakuna shaka mazungumzo yanaendelea ......

Sura ya
5

# Hatua kuelekea mafanikio

# Mambo muhimu ya kukumbuka

1 Mgogoro hauepukiki kama kulivyo kuvuta pumzi. Lakini jinsi unavyosimamiwa unaweza kuamua huenda utakuwa mkubwa au utageuka na kuwa wa madhara, au huenda utakuwa mchakato wa kuboresha mawasiliano na mahusiano baina ya walalamikaji.

2 Suluhusho la pamoja, la kutatua mgogoro na linaloleta faida kwa wote, ndilo linalopendelewa, lakini inaweza kuwa vigumu kupatikana kama wahusika wa mgogoro wana mamlaka au nafasi tofauti, au kama mawasiliano yatabaki kuwa duni.

3 Msuluhishi, kutoka ndani au nje ya jamii, anaweza kusaidia wahusika wa mgogoro kusikilizana na kuja na suluhisho linalowezekana ambalo huenda wasingeliweza kulifikiria wao wenyewe.

4 Mifumo ya kimila ya usuluhishi wa migogoro inatumia mbinu nyingi za kisasa, kama vile utafutaji wa taarifa, uchambuzi wa maslahi na mahitaji ya wadau, na haja ya kurudisha mahusiano.

5 Mawasiliano yakiwa ya mara kwa mara ndipo ushiriki utakuwa mkubwa, na itakuwa ni vizuri pale ambapo wanaohusika watakubaliana. Watu watakapoona kuwa maslahi yao yameachwa, ugomvi unaotokana na hilo unaweza kuibuka.

6 Hatua za kijamii zinaweza kuwa ni zaidi ya kuleta amani. Kwa mfano, mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi (angalia sura ya 2) unaweza kuhakikisha kwamba maslahi ya wadau wote kuhusiana na maliasili yanazingatiwa.

7 Sera zenye utata zinaweza kuchochea migogoro juu ya matumizi ya ardhi. Sera iliyo wazi ambayo inatoa haki kamili ya ardhi na maliasili inaweza kupunguza migogoro kwa kiasi kikubwa kati ya watu, vijiji na biashara.

# Mambo muhimu ya kukumbuka

## KIAMBATANISHO 1
## KISA MKASA: MGOGORO JUU YA KUANZISHA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI BURUNGE

### Hali halisi: Kujaribu kuanzisha eneo la uhifadhi la jamii

Sera ya Tanzania ya Wanyamapori ya mwaka 1998 ilitoa idhini ya kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ili kuhimiza uhifadhi na usimamizi endelevu wa wanayamapori kwenye ardhi ya jamii. Mwaka 2002 Serikali ya Tanzania ilipitisha kanuni na miongozo ya kuanzisha na kusimamia WMA.

WMA zinaruhusu jamii kusimamia, kutumia na kufaidika na wanyamapori kwenye ardhi yao. Jamii inaweza kujipatia kipato na faida nyingine kupitia matumizi ya rasilimali yasiyoathiri wingi wa rasilimali (kama vile kuangalia na utalii wa kupiga picha) na matumizi yaliyodhibitiwa yanayoathiri wingi wa rasilimali (kama utalii wa kuwinda, uwindaji kwa ajili ya kitoweo, kuchunga mifugo na kuvuna mbao).

WMA ya Burunge ipo katika kanda ya utalii ya kaskazini ambako kuna wanyamapori wengi, ambapo ipo kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara. Inapitiliza hadi kwenye njia kuu ya wanyamapori katikati ya hifadhi hizo mbili, na ardhi ya vijiji tisa: Magara, Manyara, Maweni, Minjingu, Mwada, Ngolei, Olasiti, Sangaiwe na Vilima Vitatu.

Mwaka 2002 Serikali ya Tanzania iliitenga Burunge kama moja ya WMA 16 za majaribio nchini. Lakini wakazi mwanzoni walipinga mpango huo na mgogoro mkubwa ukaibuka ndani na kati ya vijiji tisa.

### Migogoro juu ya nani anatoa nini – na mkanganyiko mkubwa

Mwanzoni, wanavijiji hawakupewa taarifa sahihi juu ya faida na gharama za kuanzisha na kusimamia WMA.

Wanavijiji wengi waliamini kwamba WMA itamaanisha kupoteza ardhi ya kijiji kwa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Ijapokuwa ilikuwa potofu, ilikuwa jambo linaloeleweka kwani katika kipindi hicho dhana ya WMA ilikuwa haijawahi kujaribiwa, na uzoefu wa mwanzo juu ya uhifadhi ulimaanisha hifadhi za taifa kuhamisha jamii.

### Migogoro ya aina mbili iliibuka:

**1) Migogoro ndani ya vijiji**

Migogoro ilikua kati ya wanajamii ambao walielewa dhana ya WMA na waliipitisha, na wale ambao hawakuielewa na kuikataa. Waliopinga WMA waliwalaumu viongozi wao kwa "kuuza" ardhi ya kijiji bila ya ridhaa yao.

Kwa nyongeza, watu wengi walielezea wasiwasi wao juu ya udhibiti maeneo ya kuchungia mifugo na kuhusu athari kwa familia zinazoishi kwenye hiyo ardhi ambayo ilikuwa iwe mojawapo ya WMA.

**2) Migogoro kati ya vijiji tisa**

Migogoro hii ilijikita katika jinsi ya kugawanya mapato, kama vile mapato kutoka katika utalii, ambayo wote walipendelea itokane na uanzishwaji wa WMA. Vijiji vingine tayari vilikuwa na mkataba na waendeshaji wa utalii; hawakuwa tayari kugawana mali wala mapato na vijiji vingine. Kwa kuongezea, vijiji vilikuwa na viwango tofauti vya wingi wa wanyamapori. Vijiji vyenye wanyamapori wengi vilitaka kupata sehemu kubwa ya mapato kwa mtazamo wa rasilimali yao na pia uharibifu mkubwa wanaokabiliana nao kutokana na wanyamapori.

Ukubwa wa aina zote mbili za migogoro uliongezeka kutokana na minong'ono iliyokuwa ikienea na wanavijiji zaidi walishawishiwa vibaya kwamba WMA itamaanisha kwamba hifadhi za taifa zitachukua ardhi yao. Wanakijiji waligeukana. Kundi moja lilitishia hata kuchoma moto nyumba za viongozi wao wa kijiji.

### Makubalianao yaliyojikita kwenye udhibiti wa mgogoro kwa njia ya kimila na taarifa mpya

Serikali na viongozi wa kijiji walitambulisha mchakato wa usuluhishi na makubaliano ambao ulianzishwa kusaidia kuleta usuluhishi wa amani wa migogoro.

Hatua ya kwanza ilikuwa ni kusuluhisha migogoro ndani ya vijiji. Mgogoro ulipogeuka na kuwa wa vurugu, viongozi wa kimila na wazee walianzisha mfululizo wa mikutano ya ngazi ya chini. Wakati wa mikutano hii, makundi yote yalitambua umuhimu wa wanakijiji kukubali kwa namna moja au nyingine, na wadau wengine kufuata nyayo zao. Mikutano ilifanikiwa kusitisha vurugu isitokee.

Licha ya hivyo, Asasi isiyo ya Kiserikali iliandaa, na Ofisa Wanyamapori wa Wilaya aliwezesha, mafuzo kwa wanakijiji juu ya faida na hasara za kuanzisha WMA.

Msuluhishi alisaidia kila kijiji kutambua maslahi yake makubwa. Kwa mfano, wafugaji walitaka eneo ndani ya WMA litengwe kwa ajili ya kuchungia wakati wa ukame. Hili lilikubalika. Wanakijiji wengine wanaoishi kwenye eneo ambalo linatarajiwa kuwa WMA waliweza "kubadilisha" ardhi yao na eneo lenye ukubwa na thamani sawa na lile la kwao nje ya njia ya mapito ya

wanyamapori. Vijiji ambavyo viliweza kuchangia kiasi kidogo cha ardhi viliruhusiwa kutumia kwa usawa faida ya kijamii pamoja na wale wanaomiliki ardhi kubwa.

Baada ya hapo ilikuwa changamoto ya kusuluhisha migogoro kati ya vijiji, kwa kuwa kila kijiji kilijaribu kutimiza maslahi yake kwa kufuata kiwango cha ardhi na rasilimali ambazo ingewekeza.

Ili kupata taarifa zaidi, kila kijiji kilichagua mwakilishi kuhudhuria safari ya mafunzo ya WMA mbili nyingine ambazo zilikuwa mbali, ili kushuhudia uzoefu wa wanakijiji wengine.

Mafunzo na safari za mafunzo ziliinua uelewa na kujenga uaminifu. Baadhi ya washiriki wa hiyo safari ya mafunzo walikuja kuwa wawezeshaji ambao wana uwezo wa kuiga walichojifunza wakati wa safari zao kwenye zile WMA. Mafunzo pia yalisaidia kuwepo kwa mikutano iliyotulia na kujadiliana juu ya mgawanyo wa mapato na masuala mengine kama vile ardhi ya kukodi.

## Watu wa aina mbalimbali walishiriki katika mchakato wa usuluhishi na makubaliano

Hawa walikuwa ni pamoja na:

- Wawakilishi wa kijiji waliochaguliwa na jamii
- Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Wilaya na timu yake ya wataalamu
- Viongozi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii
- Viongozi wa kimila na wazee
- Wanakijiji ambao walipata mafunzo
- Wafanyakazi wa African Wildlife Foundation

## Matokeo: Mikataba na usajili wa WMA

- Hatimaye vijiji vyote vilikubaliana kwamba kila kijiji ambacho kilichangia ardhi yake kitapata malipo ya kodi kwa ajili ya kuwekeza katika mradi huo. Vijiji vyote vitagawana mapato yanayotokana na uendeshaji wa utalii au biashara ya sekta binafsi inayoendeshwa na vijiji. Mapato haya yataenda kwenye akaunti ya kawaida ya WMA.
- Inasemekana mkataba umepunguza migogoro, vitisho na vurugu. Wadau wanaweza kushughulikia migogoro kupitia taasisi iliyoidhinishwa kijijini yaani CBO: ikiwa na wawakilishi kutoka kila kijiji, CBO inafanya kazi kama msuluhishi wa ngazi ya chini.
- WMA ya Burunge ilikamilisha mchakato wa usajili kwa mafanikio na ikaipatia CBO haki kamili ya matumizi: *JUHIBU: Jumuiya Ya Uhifadhi Burunge* mwaka 2006. WMA sasa inafanya kazi kikamilifu.

## Matokeo: Biashara na faida zitokanazo na uhifadhi

Tangu kusajiliwa kwake, WMA ya Burunge imepata maendeleo ya kiuchumi, kiuhifadhi na kijamii, ikijumuisha:

- **Mapato mapya kutoka kwa uwekezaji binafsi katika utalii**
  Mwekezaji binafsi, Kampuni ya Kibo Safaris, anasimamia huduma mbili za utalii katika WMA: Maramboi Tented Lodge na Lake Burunge Tented Lodge. Karibu na mwaka wa fedha Juni 2008, JUHIBU na WMA walipata mapato ya shilingi za Kitanzania 63,785,599 ambazo zingegawanywa kwa vijiji tisa.
- **Biashara ndogo za maendeleo za wanawake**
  Ongezeko la watalii wanaotembelea na kulala kwenye WMA imeleta soko kwa baadhi ya makundi ya wanawake wanaojishughulisha na kazi za mikono. Hicho kipato kinachoongezeka kinawafikia baadhi ya wakazi ambao hawafaidiki na huduma nyingi. (Angali Sura ya 3).
- **Kuongezeka kwa uwezo wa kusimamia maliasili**
  Mpaka hivi sasa zaidi ya skauti 40 wa wanyamapori wa vijiji wamepata mafunzo rasmi. Skauti hawa wanasimamia uwindaji haramu na kufanya doria za ufuatiliaji wa wanyamapori, na kuhimiza uhifadhi baina ya WMA ya vijiji tisa. Shughuli za ujangili zimepungua.

*LAKINI ...*

*Kwa uhakika baadhi ya wakazi wanashukuru matokeo ya WMA. Lakini hata tunapoandika sasa hivi, vijiji viwili vimejitoa katika WMA, wanadai kwamba hawajakubali kujiunga. Watafiti wametoa ripoti kwamba wanavijiji wengi wanasema kwamba hawakupewa taarifa kamili na kwa kiasi kikubwa mkataba ulikuwa kati ya viongozi na wawekezaji. Wengine wanaelezea kuhusu ugumu wa kuwasiliana na wanavijiji kutoka vijiji vyote tisa, na kwamba tatizo kubwa ni kuelewa isivyo. Juhudi za udhibiti wa mgogoro zinaendelea ...*

## KIAMBATANISHO 2
## AKRONIMI

| | |
|---|---|
| **ACM** | Alternative Conflict Management |
| **CBVs** | Conservation Business Ventures |
| **CTIC** | Conservation Technology Information Center |
| **DGO** | District Game Officer |
| **DLO** | District Land Officer |
| **FAO** | Food and Agriculture Organization of the United Nations |
| **ETU** | Education and Training Unit |
| **ILRI** | International Livestock Research Institute |
| **LEAD** | Livestock Environment and Development |
| **UDHR** | Universal Declaration of Human Rights |
| **URT** | United Republic of Tanzania |
| **WMAs** | Wildlife Management Areas |

## KIAMBTANISHO 3
## MAANA YA MANENO

### Mgogoro
Mgogoro ni mahusiano yanayohusu watu wawili au zaidi ambao wana maslahi na malengo yasiyoendana (FAO, 2005).

### Uchambuzi wa mgogoro
Uchambuzi wa mgogoro ni kutambua na kulinganisha misimamo, maadili, nia, matatizo, maslahi na mahitaji ya wanaogombana (FAO, 2005).

### Udhibiti wa mgogoro
Udhibiti wa mgogoro ni njia ya kutambua na kushughulikia mgogoro kwa njia yenye kuleta maana, haki na yenye kuwa na mpangilio ambayo inazuia mgogoro kuwa mkubwa na kushindwa kudhibitika na kuwa wa vurugu.

### Usuluhishi wa mgogoro
Usuluhishi wa mgogoro unahusiana na shughuli zinazolenga kushughulikia na kutatua sababu kuu za mgogoro.

### Makubaliano
Kufanya maamuzi kwa makubaliano kunahitaji kila mtu kukubali maamuzi, na siyo tu wengi wao, kama inavyotokea katika mchakato wa utawala wa wengi. Katika mchakato wa makubaliano, watu hufanya kazi pamoja ili kujenga mkataba ambao unafaa (lakini siyo lazima uwe mzuri sana) kwa ajili ya kila mtu kwenye meza aweze kukubali (FAO, 2005).

### Maslahi
Maslahi ni jambo ambalo mtu aliye kwenye mgogoro anajali au anataka. Maslahi ni mahitaji na wasiwasi muhimu ambayo yanawapa watu motisha ya kuchukua msimamo. Wakati misimamo ya watu ni kile wanachosema wanataka (kama vile "nataka kujenga nyumba hapa"), maslahi yao ndiyo sababu wanachukua msimamo fulani ("kwa sababu nataka nyumba karibu na familia yangu"). Maslahi ya watu mara nyingi yanafanana, na kwa hiyo yanazungumzika, hata wakati misimamo yao inapoonekana kuwa inapingana (FAO, 2005).

### Usuluhishi
Usuluhishi unaelezea mchakato wa makubaliano ambao unahusisha taasisi au watu walio nje ya mgogoro. Taasisi au mtu huyu anafanya kazi na wanaohusika na mgogoro ili kuwasaidia kuboresha mawasiliano yao na uchambuzi wa hali halisi ya mgogoro wao, ili waweze kutambua na kuchagua njia mbadala kwa ajili ya kusuluhisha mgogoro ambao utazingatia maslahi au mahitaji yao wote. Tofauti na kusuluhisha mgogoro kwa kuhusisha taasisi au watu walio nje ya mgogoro ambao watasikiliza pande zote mbili na kutoa maamuzi kwa ajili ya wanaohusika na mgogoro, msuluhishi anapaswa kuwasaidia wanaohusika na mgogoro kupendekeza suluhisho lao wenyewe.

### Makubaliano
"Makubaliano ni mfumo wa kufanya maamuzi kwa watu wawili au zaidi kuzungumza katika juhudi za kutatua tofauti zao za maslahi (D.G. Pruit alivyonukuliwa na FAO, 2005).

### Wadau
Wadau ni watu ambao wataathirika na mgogoro au maamuzi ya huo mgogoro. Hawa ni walalamikaji, na ni watu ambao bado hawajahusishwa katika mgogoro lakini ambao wanaweza kuhusika, kwa sababu kuna uwezekano wa wao kuathiriwa na huo mgogoro au matokeo yake siku za usoni.

### Mbinu ya kushinda-kushindwa (uadui)
Mbinu hii inatumiwa na watu ambao wanawaona wenzao kama wapinzani ambao lazima washindwe. Ili mtu mmoja ashinde, ni lazima yule mwingine ashindwe. Hii inatofautiana na ile mbinu ambayo wote wanashinda, mbinu ambayo inaamini kwamba kama wahusika wa mgogoro watashirikiana, suluhisho ambalo linatoa ushindi kwa pande zote mbili litapatikana (Conflcit Research Consortium, 1998).

### Mbinu ya wote kushinda (ushirikiano au utatuzi wa tatizo)
Hii ni mbinu ya mgogoro ambayo inatumiwa na watu ambao wanataka kupata suluhisho ambalo litanufaisha pande zote mbili. Katika kuzungumzia suluhisho la kila mmoja kushinda, wahusika wa mgogoro wanajaribu kushirikiana kutatatua tatizo linalowahusu kwa namna ambayo inaruhusu watu wote "kushinda". Hii ni tofauti na ile mbinu ambayo mmoja anashinda na mwingine anashindwa (njia ya uadui), ambayo inaamini kwamba kila mtu ni adui na ili mmoja ashinde huo mgogoro mwingine anapasha kushindwa (Conflict Research Consortium, 1998).

## KIAMBATANISHO 4
## FAHARASA

**Conservation Technology Information Center (CTIC). 2008**. Managing Conflict A Guide for Watershed Partnerships, [Online]. Available from: <http://www.ctic.purdue.edu/KYW/brochures/manageconflict.html> [11th November 2008].

**Education and Training Unit (ETU).** (2008). Conflict Management, [Online]. Available from: <http://www.etu.org.za/toolbox/docs/building/conflict.html> [11th November 2008].

**Fisher, R and Ury, WL.** 1991. *Getting to Yes: Negotiating Agreement Without Giving In.* New York: Penguin, 1991.

**Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO).** 2005. *Negotiation and Mediation Techniques for Natural Resource Management*, FAO, Rome.

**Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO)** (2006) *Conflict Management Over Natural Resources: Capacity Building Program under the Community-Based Rural Development Project (CBRDP)*, Government of Ghana-World Bank.

**Turner M, Ayantunde AA, Patterson ED, and Patterson KP.** 2007. Conflict Management for Improved Livestock Productivity and Sustainable Natural Resource Use in Niger, West Africa. ILRI Report. ILRI (International Livestock research Institute), Niger. 97pp.

**United Republic of Tanzania (URT).** 1999. *The Land Act No. 4*, Ministry of Lands, Housing and Human Settlement, Dar es Salaam.

**United Republic of Tanzania (URT).** 1999. *The Village Land Ac No. 5*, Ministry of Lands, Housing and Human Settlement, Dar es Salaam.


**United Republic of Tanzania (URT).** 1997. *The National Land Policy, Second edition*, Ministry of Lands, and Human Settlement Development, Dar es Salaam.

**Wehrmann, B.** 2008. *Land Conflicts: A Practical Guide in Dealing with Land Disputes*, GTZ, Eschborn, Germany.

# Viambatanisho

# Namna ya kukabiliana na magonjwa ya mifugo karibu na hifadhi za wanyama Afrika Mashariki

# Utangulizi



Kwa karne nyingi wafugaji wamekuwa wakimudu mifugo yao na nyanda za malisho kwa kuhamahama kufuatana na majira, wakitunza maeneo ya malisho kwa msimu wa kiangazi, wakihifadhi aina fulani fulani za miti, na kujiepusha na maeneo yajulikanayo kuwa na maradhi. Utaratibu huu wa kimila wa mpango wa matumizi ya ardhi ulisaidia mifugo na wanyamapori kusitawi vizuri kwenye nyika za Umasaini, ambazo hadi sasa zina idadi kubwa ya mamalia wakubwa ulimwenguni.

Lakini katika miongo ya karibuni sera za serikali na kukua kwa ongezeko la watu vimesababisha kupungua kwa uhuru wa kuhamahama kwa wafugaji, ukiibana mifugo kwenye maeneo yenye nafasi ndogo.

Kupunguza uhuru huo kunahatarisha vyanzo vya mapato na chakula kwa wafugaji, kusababisha migogoro, na kukua kwa "miingiliano" ya wanyamapori na mifugo. Katika hali hii, mifugo na wanyamapori wanashirikiana malisho, maji, na kuambukizana magonjwa.

Yawe yanatoka kwa wanyamapori au la, magonjwa ya mifugo yanaweza kusababisha hasara kubwa kwenye mifugo na mapato ya kaya. Wafugaji wengi wanapoteza sehemu kubwa ya mifugo yao na kutumia kiasi kikubwa cha mapato yao kudhibiti magonjwa kila mwaka. Baadhi ya vimelea hushambulia binadamu pia.

Kwa madhumuni ya kulinganisha: utafiti uliofanywa hivi karibuni kwenye wilaya ya Isinyi huko Kenya, umegundua kwamba asilimia 60 ya ndama na asilimia 50 ya ng'ombe waliokomaa walikadiriwa kuwa walipata magonjwa ndani ya mwaka mmoja, 2003-04 (Bedelian et al, 2006).

Kuwasaidia wafugaji waweze kumudu afya ya mifugo kunaweza kuongeza kipato kinachohitajika sana na kusaidia kudumisha afya za watu.

## UMUHIMU WA SURA HII

Ugonjwa ni zaidi ya suala la vimelea. Viwango vya ugonjwa vinaongezeka au kupungua kutegemeana na



*Matumizi ya pamoja ya rasilimali kati ya mifugo na wanyamapori*

# Utangulizi



sababu nyingi za kiekolojia na za kijamii. Kwa sasa, jamii na pia wanataaluma wamekwishaona kuwa magonjwa ya mifugo yanaongezeka kwenye maeneo ya wafugaji.

Magonjwa ambayo ni mapya katika maeneo fulani fulani yanaibuka. Magonjwa ambayo yalikwishadhibitiwa huko nyuma yanarudi. Na mengine yanazidi kusambaa.

Watalamu wa mipango na wanajamii wanatakiwa kufahamu mienendo inayochangia kuleta magonjwa ya mifugo, kwa sababu magonjwa yanadhuru maisha ya jamii na mapato yao. Na shughuli za binadamu zinaweza kusaidia kudhibitiwa na hata kufuta kabisa magonjwa mengi.

Mambo yanayochangia ongezeko la magonjwa ya mifugo ni pamoja na ambayo yamejadiliwa kwenye kitini hiki (hasa Sura ya 1 na ya 2). Kwa ufupi ni:

- **Mabadiliko ya tabianchi.** Joto katika Afrika Mashariki, kama ilivyo katika sehemu nyingine nyingi ulimwenguni, linaongezeka taratibu. Licha ya hivyo, mgogoro wa hali ya hewa unasababisha ongezeko la matukio ya hali mbaya ya hewa, ukame kutokea mara kwa mara zaidi, lakini pia mafuriko kutokea mara nyingi zaidi inaponyesha mvua. Mifugo inapodhoofika kwa kukosa malisho au maji, uwezo wa mifugo hiyo kustahimili magonjwa unapungua. Na, katika mzunguko huo wa matatizo, mifugo iliyodhoofishwa na magonjwa inapungukiwa na uwezo wa kustahimili ukame.
- **Wadudu wanaosambaza magonjwa wanaongezeka.** Joto linapoongezeka na mvuke hewani kubadilika, wadudu wasambazao magonjwa wanasambaa kwenye eneo kubwa zaidi na kusababisha mifugo kuugua katika maeneo ambayo hapo awali hayakuwa na magonjwa hayo.
- **Kupungua kwa ardhi.** Kuibadili ardhi iliyokuwa malisho kwa kuilima kunasababisha wafugaji kubanana kwenye maeneo madogo kuliko hapo awali, na kuwanyima uwezo waliokuwa nao wa kuhamahama kufuatana na majira ya mvua na malisho mazuri, na kuwaweka katika hali ambayo miingiliano na wanyamapori ni mikubwa.
- **Kupungua kwa huduma za afya kwa wanyama.** Kujitoa kwa serikali katika kutoa huduma za afya kwa wanyama kunakotokana na kuzidi kupungua kwa bajeti inayotengwa kwa huduma katika sekta za jamii, upungufu wa wataalamu, miundombinu na vitendea kazi, mfumo dhaifu wa kupashana habari na pia ufuatiliaji, vyote hivyo vinaathiri uwezo wa utoaji huduma bora za kiwango cha juu katika maeneo ya wafugaji.

*KUWAKUMBUKA NG'OMBE WAKATI WA KUPANGA MATUMIZI YA ARDHI*

*"Watu wana wasiwasi kuwa tukitenganisha wanyamapori na mifugo, itakuwa kama kuwa na hifadhi nyingine, na hawataki hali hii. Ni muhimu zaidi kusisitiza kushirikiana kwenye ardhi. Lakini wakati mwingine wanyama wanapaswa kutenganishwa kwa kipindi fulani. Kwa mfano, kuweka n'gombe mbali na mazalia ya nyumbu mpaka ndama wao wanapotimiza miezi mitatu. Hii itazuia mifugo kupata Ugonjwa wa Nyumbu (Malignant Catarrhal Fever).*

*Lakini ili kufanya hivyo ni lazima kuwepo na sehemu nyingine iliyotengwa, ambapo ng'ombe watakuwa katika kipindi hicho. Ni muhimu sana kulikumbuka hili wakati wa mchakato wa kupanga matumizi ya ardhi.*

*Moses Neselle,*
*Mganga wa Mifugo na Mtaalamu wa Mipango ya Jamii*

Habari njema ni kwamba baadhi ya magonjwa yanaweza kuzuilika au kudhibitiwa kwa kupanga vizuri matumizi ya ardhi kwenye ngazi ya jamii (angalia sura ya 2). La muhimu katika kupanga ni kuwa mwangalifu kuzingatia mahitaji ya wafugaji na ujuzi walionao, ili mifugo yao iwe katika maeneo yasiyokuwa na magonjwa na yana malisho wakati wa dharura.

Kwa kuongezea, mzigo uliyonayo jamii ya wafugaji utokanao na magonjwa yanayohusiana na wanyamapori unaweza kufidiwa kwa kufungua fursa mpya, kama biashara zinazohusiana na asili. Nchi za Afrika Mashariki zinaruhusu jamii kunufaika na utalii, kufuga nyuki na biashara nyinginezo zinazohusiana na kuwepo kwa wanyamapori na misitu na mapori mazuri (angalia sura ya 3).

Si nia ya yafuatayo kuchukua nafasi ya muongozo wa matibabu ya mifugo ila, kwa ufupi, kutoa mwanga kwa masuala muhimu na maendeleo yaliyopatikana hivi karibuni juu ya magonjwa ya kawaida ya mifugo kwenye maeneo ya wafugaji yaliyo pembezoni mwa hifadhi za taifa.

# Hatua kuelekea mafanikio



*Daktari wa mifugo akimtibu mfugo*

## MAGONJWA MAKUU YA MIFUGO NA MWENENDO WAKE KWENYE MAENEO YA WAFUGAJI

### 1. Kimeta
*(Maa: Engeeya Nairowa; Kiingereza: Anthrax)*

#### Unayopaswa kujua

Ugonjwa wa Kimeta unawashika mifugo na pia mbogo, punda-milia, na wanyamapori wengine walao majani. Vimelea vya Kimeta vinaweza kuishi kwenye udongo kwa muda mrefu. Kuna uwezekano wanyama wakapata ugonjwa wa kimeta mwanzoni mwa majira ya mvua, wakati majani wanayokula yanapokuwa mafupi.

Kutokana na mabadiliko ya matumizi ya ardhi, ambayo yanaifanya mifugo na wanyamapori kukaa pamoja kwenye eneo dogo, matukio ya kimeta yanaongezeka.

Binadamu wanaweza pia kuupata ugonjwa huu, kwa kushika au kula nyama ya mifugo iliyoambukizwa.

#### Dalili za kimeta ...

- Kifo cha ghafla cha mfugo mwenye afya
- Kuwa na uvimbe kwenye shingo, kifua, tumbo, na/au miguu ya mifugo inayougua lakini haifi.

#### Kuwa mwangalifu

Kama watu au wanyama walao mizoga wataupasua mzoga (na kuufanya utumbo kutoka) wa mnyama aliyekufa kwa kimeta, wanaweza kupelekea kuanza mlipuko wa kimeta kwa kusababisha vimelea kusambaa kwenye hewa na udongo. Ardhi ambayo itafikiwa na majimaji kutoka kwenye mzoga wa mnyama aliyeugua kimeta yaweza kuhifadhi vimelea vya ugonjwa huo hata kwa miaka ipatayo 60!

Kama unahisi mnyama amekufa kutokana na kimeta, linda mzoga au ufunike kwa miiba au mawe kuzuia wanyama walao mizoga wasiupasue.

Uchome mzoga baada ya kuunyunyizia mafuta ya taa au petroli. Au ufukie kwenye shimo la urefu wa mita mbili na kuumwagia majivu au chokaa.

#### Kuzuia na kudhibiti

Chanja kwa miezi kati ya tisa na kumi na mbili na chanjo hiyo bora iwe imehusisha juhudi ya jamii au serikali ikilenga kuwachanja ng'ombe wote.

Dawa dhidi ya bakteria (Antibiotics) zinaweza kuwa dawa sahihi iwapo matibabu yataanza mapema, ingawa ni bora kuzuia ambako pia gharama zake ni nafuu.

### 2. Homa ya Bonde la Ufa
*(Kiingereza: Rift Valley Fever)*

#### Unayopaswa kujua

Watu wengi wanafikiri kuwa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa unatoka kwa wanyamapori, si hivyo.

# Hatua kuelekea mafanikio



Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa unaenezwa na panya na mbu. Mbu wanang'ata panya walioambukizwa, na mbu hao wanaiambukiza mifugo ugonjwa huo wanapoing'ata.

Matukio ya ugonjwa yanaongezeka wakati wa kipindi cha mvua panapokuwa na mbu wengi hasa mvua nyingi zinaposababibisha madimbwi ya maji ambayo ni mazalia ya mbu. Mbu wanaongezeka pia mwishoni mwa majira ya mvua, wakati idadi ya panya inapoongezeka.

Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulikuwa haujawahi kusikika kwenye nyanda za umasaini mpaka mwaka 1997, mlipuko ulipotokea kufuatia mvua kubwa za El Nino. Baada ya hapo ilionekana kudhibitiwa mpaka kipindi cha mvua kisichokuwa cha kawaida mwaka 2006, ambapo mlipuko ulisambaa kutoka mkoa wa Rift Valley nchini Kenya. Katika miaka ya 2006 na 2007, ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa uliua maelfu ya ng'ombe na zaidi ya watu 150 nchini Kenya na Tanzania.

Mabadiliko ya tabianchi yanaelekea kusababisha majira zaidi ya mvua nyingi au inayonyesha kwa vipindi virefu zaidi, kwa hivyo milipuko ya ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa inatarajiwa kuendelea kutokea.

### Dalili ...

Kwenye mifugo: Matukio mengi ya mimba kuharibika kwenye ng'ombe, mbuzi au kondoo.

Kwa binadamu: Dalili kama za mafua ikiwa ni pamoja na homa ya ghafla, kuumwa kichwa, na maumivu ya misuli na mgongo. Kama mwili umebadilika na kuwa wa manjano na unatapika, nenda hospitali haraka la sivyo kupungukiwa damu, upofu au kifo vyaweza kutokea mara moja.

### Kuwa mwangalifu

Binadamu wanaweza kupata ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa kutokana na kung'atwa na mbu, kuchinja mnyama mwenye ugonjwa huu bila kuchukua tahadhari au kula nyama ya mnyama mgonjwa bila kuiandaa vizuri, yawezekana kwa kunywa maziwa yasiyochemshwa vizuri, na pia hata kwa kuvuta hewa yenye virusi kutoka kwenye mzoga wa mnyama aliyeugua ugonjwa huu.

Ugonjwa huu huathiri vizazi vijavyo vya mifugo kwa sababu unaingilia uzaaji.

Kama patatokea mlipuko, wanyama kutoka kwenye eneo linalohusika watapigwa karantini. Wakati wa mlipuko na kipindi cha mwezi mmoja baada ya hapo, inazuiliwa kuuza mifugo (ng'ombe, kondoo au mbuzi), na mazao ya mifugo (maziwa, nyama au ngozi).

Ukiona uharibikaji mimba usio wa kawaida, toa taarifa mara moja kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji, au Ofisa ugani au bwana mifugo.

### Kuzuia na kudhibiti

Kwa mifugo: kuchanja mifugo kila mwaka kunasaidia. Juhudi ya jamii au serikali kuchanja n'gombe wote ni mkakati sahihi zaidi.

Kwa binadamu: tumia chandarua kuzuia kuumwa na mbu. Pia jiepushe kugusa mimba iliyotupwa. Jikinge kwa kuvaa mikononi glovu au mifuko ya plastiki. Zika mizoga kwenye shimo refu kiasi ambacho mbwa na wanyama wengine walao nyama hawawezi kufukua.

Mipango ya serikali inaweza kusaidia kwa kujiandaa kuchanja baada ya mvua nyingi. Kwa mafanikio mazuri muda wa kuchanja usirefushwe.

Hakuna matibabu ya ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa yanayofahamika.

## 3. Ugonjwa wa Miguu na Midomo

*(Maa: Oloroibi, English: Foot and Mouth Disease (FMD))*

### Unayopaswa kujua

Ugonjwa wa miguu na midomo unawashika ng'ombe, kondoo, mbuzi, mbogo, swala na wakati mwingine tembo. Unasambaa haraka kwenye kundi ukiua ndama na kusababisha wanyama kupoteza uzito na uzalishaji wa wengine kupungua.

Ugonjwa wa miguu na midomo unaambukiza kwa kugusana kwa mnyama mmoja na mwingine. Unaweza vile vile kusambazwa na upepo kwenye umbali hata wa kilometa 250!

Ni nadra binadamu kupata ugonjwa huu.

Kwa muongo mmoja uliopita, kwa wastani ugonjwa huu ulikuwa unashambulia kundi mara moja kwa mwaka. Kwa sasa, katika sehemu nyingi za Afrika Mashariki, ugonjwa unatokea mara tatu kwa mwaka. Kwa kuongezea, jinsi hali ya hewa inavyokuwa ya joto la juu, yanatokea matabaka mapya ya vimelea visababishavyo ugonjwa huu.

### Dalili ...

- Kuwepo mifugo yenye dalili za mafua, na kuchechemea kwa wakati huo huo.
- Ndama kufa kwa ghafla kutokana na ugonjwa wa moyo.

### Kuwa mwangalifu

Ugonjwa wa miguu na midomo una madhara makubwa kiuchumi. Uzalishaji wa maziwa wa ng'ombe waweza kupungua kwa asilimia 75 kwa maisha yake yote. Kwa kuongezea, badala ya kuzaa kila mwaka au kwa vipindi kama hivyo, ng'ombe anaweza kuzaa kila baada ya miaka miwili au mitatu.

### Kuzuia na kudhibiti

Chanjo inaweza kusaidia lakini gharama yake ni kubwa kwa sababu chanjo zinanunuliwa kutoka nchi za nje na lazima chanjo hiyo iwe ya kufanyakazi dhidi ya aina nyingi za vimelea. Jamii inaweza kupanga, na kununua chanjo kwa kushirikiana. Jamii chache kaskazini mwa Tanzania tayari wanafanya hivyo.

Serikali ina jukumu la kuzuia ugonjwa huu. Kwa mfano, serikali ya Tanzania imeahidi kuchangia gharama za chanjo kwa ajili ya ng'ombe wapatao milioni mbili. Na kwa kuwa Tanzania ina ng'ombe wapatao milioni 20, wote wanaweza kunufaika na mchango wa serikali.

Ugonjwa wa miguu na midomo ni hatari, hasa pale ambapo mifugo inatumia ardhi ambayo pia inatumiwa na mbogo na nyumbu. Kwa hiyo, ugonjwa wa miguu na midomo, na gharama ya chanjo, ni vitu viwili kati ya sababu nyingi ambazo jamii zinapaswa kuzingatia zinapowazia kupanga matumizi ya ardhi na shughuli za biashara zihusianazo na uhifadhi (angalia sura ya 2 na ya 3). Biashara kama hizo zinasaidia jamii kupunguza gharama wanazozipata kwa kuishi karibu na wanyamapori, wakipata kipato kutokana na kuwepo kwa wanyamapori hao.

## 4) Ugonjwa wa Nyumbu

*(Maa: lingati, Kiingereza: Malignant Catarrhal Fever (MCF))*

### Unayopaswa kujua

Virusi aina mbili tofauti husababisha ugonjwa wa nyumbu kwenye ng'ombe. Aina moja ya virusi inasambazwa na kondoo na mbuzi wakati aina nyingine inasambazwa na nyumbu na pofu.

Aina ya pili ni tatizo kubwa hasa wakati na mahali ambapo nyumbu wanazalia. Virusi vinawaachia watoto wanyumbu wanapotimiza miezi mitatu baada ya kuzaliwa.

Kwa karne nyingi, ugonjwa wa nyumbu ulikuwa hauwaletei wafugaji madhara makubwa kwa sababu walikuwa wanahamisha mifugo yao kwenda sehemu nyinginezo kila mwaka katika kipindi ambacho nyumbu wanazaliana.

Mpango huu wa kimila wa matumizi ya ardhi umesambaratika, ijapokuwa ni katika miongo michache iliyopita, kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya kutumia ardhi (hivyo mashindano) na hivyo ng'ombe na nyumbu kulazimika kupata malisho katika eneo moja hata katika vipindi nyeti ambapo nyumbu wanakuwa wanazaa.

Bila kuchukua hatua za tahadhari, ng'ombe na nyumbu wataendelea kula katika eneo moja na hivyo uwezakano wa ugonjwa wa nyumbu kuongezeka pia.

### Dalili ...

Macho ya ng'ombe yanakosa uwezo wa kupitisha mwanga. Baada ya hapo mnyama anapofuka na kufa.

### Kuzuia na kudhibiti

Kwa sasa hakuna chanjo wala tiba.

Udhibiti unawezekana kupitia matumizi mazuri ya ardhi. Mipango ya matumizi ya ardhi inabidi izingatie mahitaji ya wafugaji na uhamaji wa nyumbu na mazalia yao. Mipango inaweza kuweka eneo tofauti la malisho ya mifugo kwenye majira ya nyumbu kuzaa, ambayo kwa wastani yanaanza mwishoni mwa Februari hadi Mei (Angalia Sura ya 2 juu ya mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi).



*Nyumbu wakizaa*


## 5) Ugonjwa wa Ndigana moto

*(Maa: Engeeiya Nairowa, Kiingereza: Corridor Disease (Theileriasis))*

Ugonjwa wa Ndigana moto unahusisha magonjwa mabaya kadhaa ya ng'ombe, ambayo kati yake ndigana (East Coast Fever - ECF) ni ugonjwa ambao unafahamika na ambao ni maarufu.

# Hatua kuelekea mafanikio





*Mtaalam wa mifugo akimchanja ng'ombe*



*Kuogesha ng'ombe kwenye josho*

Ndigana inasambazwa na kupe wa kahawia washambuliao masikio, ambao hushambulia mbogo. Mbogo hupendelea sehemu zenye vichaka – sehemu ambazo kwa hali ya kawaida ng'ombe hupata malisho wakati wa kiangazi.

### Dalili ...

Ugonjwa una dalili chache zinazoonekana, ingawa kwa kawaida vifo hutokana na matatizo ya kupumua.

### Kuzuia na kudhibiti

Dawa za kutibu Ugonjwa wa Ndigana moto zipo lakini gharama yake ni kubwa; ni bora kuudhibiti.

Jamii na watumishi wa serikali wanaweza kuwa na majosho ya kuogeshea mifugo ili kusaidia kuua kupe, ambao ndio wasambazao ugonjwa. Kiutamaduni, wafugaji huchoma majani mara ufikapo mwisho wa majira ya mvua, yaani kinapoanza kipindi cha kiangazi (wakati wanyamapori wahamao kama mbogo huwa wanarudi kwenye hifadhi). Kuchoma kunafanywa pia kwa nia ya kuwezesha majani kuchipua kwa ajili ya malisho katika maeneo haya, hivyo faida ya kuchoma kuwa kubwa zaidi.

Mpango wa matumizi ya ardhi ni suala muhimu. Inapopatikana nafasi kubwa zaidi kwa mifugo na wanyamapori ndivyo uwezekano wa ng'ombe kuchanganyikana na mbogo na kukutana na kupe kunavyozidi kupungua.

## 6) Ndorobo

*(Maa: Entorrobo, English: Trypanosomiasis)*

### Unayopaswa kujua

Ugonjwa wa ndorobo unawashambulia wanyamapori, mifugo na binadamu. Mbung'o ndio wanaoambukiza ugonjwa kutoka kwa mnyama au mtu mmoja ambaye amekwisha shambuliwa kwenda kwa mwingine. Ugonjwa huu unaposhambulia binadamu hujulikana kama "homa ya malale".

Ugonjwa wa ndorobo nao unaongezeka. Katika miaka iliyopita, watu walikuwa wakikwepa maeneo yenye mapori ambapo kwa kawaida mbung'o huishi. Siku hizi wafugaji wanalazimika kwenda kwenye maeneo hayo kwa sababu ardhi inayofaa zaidi kwa kilimo inazidi kulimwa.

Ukiitwa "entorrobo" kwa Kimasaai, ugonjwa wa ndorobo ni mmoja kati ya magonjwa mabaya ya mifugo katika Afrika kwa sababu unashambulia mifugo mingi, unagharimu kuutibu, na unaweza kumshika mnyama huyo huyo kwa kurudia mara kadhaa. Unashambulia na kuua ng'ombe, kondoo, mbuzi, punda, na mbwa.

### Kuwa mwangalifu

Baadhi ya wafugaji katika nchi za Afrika Mashariki wanatumia fedha nyingi kupambana na ndorobo kuliko wanavyotumia kwenye suala jinginelo lolote linalohusu ufugaji.

Utafiti mmoja uliofanyika hivi karibuni umebaini kuwa ng'ombe wanaofikia asilimia 15 sehemu za kusini mwa Kenya huambukizwa "entorrobo" kila mwezi.

Ugonjwa wa ndorobo (homa ya malale) ni hatari kwa binadamu pia. Wilaya za Tarangire na Babati kaskazini mwa Tanzania zinatambulika kuwa maeneo sugu ya ugonjwa wa ndorobo au homa ya malale.

### Dalili

Homa zisizoisha, kuvimba, na kuharibika kwa mfumo wa mishipa ya fahamu. Ugonjwa husababisha kupungua sana uzito, damu kupungua mwilini, na kifo. Utambuzi kamili wa ugonjwa unafanywa kwenye maabara yenye vyombo maalum tu.

Kwa binadamu, ugonjwa wa homa ya malale unasababisha homa, kichwa kuuma, kuumwa viungo na mwili kuwasha. Hatua ya pili inahusisha mfumo wa mishipa ya fahamu, na unaweza kusababisha mawasiliano kati ya sehemu kadhaa za mwili kuharibika, kuchanganyikiwa, na hali isiyokuwa ya kawaida ya kusinzia. Ugonjwa unatibika lakini ni mbaya usipotibiwa.

### Kuzuia na kudhibiti

Njia nzuri zaidi ya kudhibiti ugonjwa huu ni kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi unaowahakikishia wafugaji kuwa na ardhi ya kutosha isiyokuwa na mbung'o.

Maeneo yenye mbung'o mara nyingi yanakuwa na wanyamapori wengi, na hivyo kuwa maeneo yanayofaa kwa utalii na ambayo yanaweza kutumika kama maeneo ya malisho ya dharura wakati wa ukame.

Katika maeneo yaliyo na mbung'o, wenyeji wanawavuta na kuwaua kwa kutandaza kwenye miti au vichaka vipande vya nguo nyeusi, bluu au nyeupe, ambavyo vinakuwa vimetumbukizwa kwenye dawa.

Zipo dawa za kutibu ndorobo, lakini vimelea vya ugonjwa huo vinaweza kuwa sugu kwa dawa. Upangaji mzuri wa matumizi ya ardhi upewe kipaumbele kama namna ya kupambana na ugonjwa huu.

Sura ya
6

# Hatua kuelekea mafanikio

# Mambo muhimu ya kukumbuka

1 Kwa kiasi fulani, kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya ardhi, magonjwa ya kawaida ya mifugo yanaongezeka kwenye maeneo ya wafugaji katika Afrika Mashariki. Kupungua kwa nyanda za malisho kunakokwenda sambamba na kuongezeka kutumia pamoja ardhi kati ya mifugo na wanyamapori, magonjwa yanakuwa mzigo ambao unabebwa na jamii ya wafugaji.

2 Magonjwa ya mifugo yanaweza kupunguzwa kwa kupaga vizuri na kugawana matumizi ya ardhi, ikihakikishwa kuwa wafugaji hawasukumwi ili kufanya shughuli zao kwenye maeneo yanayosifika kwa kuwa na magonjwa. Wafugaji wanahitaji nafasi ya kutosha, kiasi cha uwezo wa kuhamahama na uwezo wa kufanya mabadiliko yanayoweza kuruhusu mifugo kubaki na afya inayostahili.

3 Wakati wa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi, inapasa kuangalia kwa uangalifu maeneo ya wafugaji: mifugo itakuwa wapi, katika majira yapi? Ni maeneo yapi yenye magonjwa ya wanyamapori kwa wingi? Kama jamii inatumia ardhi ya vijiji jirani, kupanga kwa pamoja matumizi ya ardhi kunaweza kuwa kwa manufaa.

4 Kwa kuongezea, inabidi kusisitiza biashara inayohusiana na uhifadhi, na mapato kuelekezwa kwenye jamii. Jamii ya wafugaji inaweza kunufaika sana kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

5 Juhudi za kupunguza athari za matukio ya ukame yanayoongezeka zinaweza vilevile kusaidia, kwa mfano, kuvuna maji ya mvua na kukuza mabwawa ya asili na yaliyochimbwa.

6 Serikali ina jukumu kubwa la kutekeleza katika kuzisaidia jamii kupata chanjo na mipango mingine ya kudhibiti magonjwa. Programu za ugani za wataalamu wa mifugo zinapashwa kuimarishwa na wahitimu wa tiba ya mifugo kutoka kwenye vyuo kama Emboreet, kwa mfano, waajiriwe kufanya kazi kwenye maeneo ya wafugaji na wakulima.

# Mambo muhimu ya kukumbuka

## FAHARASA

**Bedelian, C., Nkedianye, D., Herrero, M.,** 2007. "Maasai perception of the impact and incidence of malignant catarrhal fever (MCF) in southern Kenya," Preventive Veterinary Medicine 78, 296-316.

**Castro, J.J.** 1997. Sustainable tick and tickborne disease control in livestock improvement in developing countries. Elsevier Science B.V.

**FAO.** 1971. Reports of Joint FAO/OIE/CCTA Expert Panel on contagious bovine pleuropneumonia Rome.

**Hall, S.A** 1983. "The diagnosis of contagious bovine pleuropneumonia and other infections with mycoplasma mycoides subspecies mycoides," Document No. EUR 8654 of the commission of the European Communities

**Hudson, J. R.** 1971. Contagious bovine pleuropneumonia. FAO, Agricultural Studies, No. 86.

**Plowright, W.** 1986. Malignant Catarrhal Fever. Revue Scientique et Technique de le l'Office International des epizooties, 5, 897 - 918.

# Viambatanisho